

**MATUMIZI YA LUGHA KATIKA KANISA KATOLIKI: UCHANGANUZI
WA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA MAHUBIRI**

NA

WAWERU TERESIA WANJIRU (SR)

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU
CHA NAIROBI**

2014

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

.....
WAWERU TERESIA WANJIRU (SR)

.....
TAREHE

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri wa mwanafunzi tulioteuliwa na chuo.

.....
PROF. JOHN HABWE

.....
TAREHE

.....
DKT. JEFWA MWERI

.....
TAREHE

TABARUKU

Kwa marehemu babangu George Waweru Ngatia kwa kunifunza dhamana ya masomo tangu utotoni. Nina uhakika unaifurahia mbegu uliyoiotesha tangu utotoni unaponitazama uwinguni ulipo.

Kwa mamangu mpenzi, Susan Kahito Waweru kwa kuwa dira yangu maishani na mwombezi wangu kila mara,

Shirika langu la Mtaktifu Yosefu-Mombasa kupitia kwa wanachama wote chini ya mama Ursula, kwa kunipa fursa ya kusoma na kunifadhili,

Marafiki wa dhati kwa kusimama nami wakati wote.

SHUKRANI

Kwa msaada na nguvu zake Rabuka yote yanawezekana (Mk: 10:27) Sifa na taadhima kwake Maulana. Hakika safari ndefu huanza kwa hatua moja. Safari hii haikuwa rahisi na haingewezekana bila msaada na ushauri wa watu mbalimbali kwani kidole kimoja hakivunji chawa. Hivyo, nina wajibu wa kutoa shukrani za dhati kwa wote walionifaa kwa hali na mali.

Shukrani tele ziwaendee washauri wangu Prof. Habwe na Dkt. Jefwa kwa ushauri wenu wenye busara, subira, hekima na moyo wa kuhimiza hasa nikaweza kupata dira ya kile nilikuwa nalenga katika kazi yote yangu. Asante Prof. Habwe kwa kunifanya nipendezwe na pragmatiki na kwa ushauri wako wenye utaratibu, utulivu na subira bila kipimo cha maelezo. Dkt. Jefwa kwa umakinifu wako, utayari na uvumilivu katika kunielekeza. Mwenyezi Mungu awatimizie mahitaji yenu ya kila siku na kuzidisha vipawa vyenu vya kiakademia.

Wahadhiri wangu wa Idara ya Isimu na Lugha nawashukuru na kuwapa hongera kwa kujitua mhanga katika uwanja wa lugha na kutufikisha kwenye upeo. Asanteni sana kwa kunifanya nijivunie kuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunihusisha vilivyo darasani jambo ambalo liliniweka macho daima na kunisaidia nikaweza kuhusiana nanyi na wenzangu bila tashwishi yoyote. Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa Mwenda Mbatiah, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Evans Mbuthia, Mw. Mungania na Dkt. Amiri Swaleh. Mungu awashushie zake baraka zisizo na kifani. Katu sipuuzi changamoto walizotupa kuwa sio tu kupita mtihani bali kuweza kuelewa kikamilifu na kwa uzamifu unalolifanya. Nakishukuru Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mikakati kabambe na kwa kunifadhili kufanya kozi hii na kuimaliza kwa urahisi na kwa muda uliotengwa. Hongera kwa wahutubu kwa wenu uelekezi na uvumilivu. Shukrani za dhati zimwendee Mw. Mary Ndungu kwa uelekezi wenye subira na upendo na hasa kwa kuwa nyota ingaayo mbele ya safari yangu. Namshukuru Sista Dkt. Elizabeth Nduku kwa kunizindua

na kunihimiza sana masomoni na kunipa changamoto ya kuifuata ndoto yangu ya kiakademia. Padri Clement Karathi kwa ushauri na uelekezi wa dhati hasa mambo yalipokaa magumu. Asante kwa kunipa changamoto kwa njia yenye upendo ya kuwazia zaidi niyatendayo kwa kina na kuyavumilia yote kwa subira.

Namshukuru mkuu wa Chuo cha Walimu cha Machakos Bw. Stephen Nalelia kwa ushauri kwa walimu wake wote kuendeleza masomo wakati ungalipo. Kwa kuwa na moyo wa ubaba na nia njema kwa sote tuliojitosa masomoni. Siwezi kuwapuuza wenzangu ofisini Bw. Kimondiu na Bw. Maingi kwa kunielewa na kunivumilia wakati wa masomo yangu. Shukrani pia kwa Bi. Musau, Bi Kirigwi na Bi. Mutuku kwa kuhimizana kimasomo na kikazi. Asante sana Dkt. Mutua kwa kunipa changamoto ya kuendelea kukienzi Kiswahili lugha yetu na kwa ushauri wako wa kiakademia.

Nawashukuru wenzangu tuliosoma pamoja na kutiana moyo kwamba hakuna refu lisilo na mwisho. Hao ni pamoja na Regina Gitau na Vincent Oiro (wenzangu wa kikundi) tuliofaana katika kila hali ya kimasomo bila chuki wala wivu. Matunda ya fadhila hizi ni ufanisi huu tunaojivunia. Wengine ni Ruth Moraa, Jane Obara, Nahashon Akungah, Julius Kirabi, Duncan Munga, Samuel Tsuma, Mariam Ngome, Grace Njenga, Magdalene Mulwa, Scholastica Waweru, Dorice Kachipela, Jael Akinyi, Margaret Karanja, Margaret Muthoni na Furaha Mbetsa. Ushirikiano na kuhimizana kumetuwezesha kufika umbali huu. Marafiki wote wa nia njema hasa masista dada zangu nashukuru kwa msaada na upendo wa dhati hasa jumuiya ya Anuarite - Nairobi nilikoishi wakati wote nikisoma. Asanteni kwa kunielewa na kunivumilia hasa katika masuala na shughuli za kijumuiya. Mwisho shukrani zangu ziendee familia yangu kwa kunihimiza na kunivumilia hata niliposhindwa kuwaamkua nyumbani kutokana na mahitaji ya masomo yangu. Mlinihimiza na kuniombea siku zote.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
YALIYOMO.....	vi
IKISIRI	ix
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI.....	1
1.0 USULI WA MADA.....	1
1.1 TATIZO LA UTAFITI	4
1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI	6
1.3 HAIPOTHESIA	6
1.4 UMUHIMU WA UTAFITI	6
1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI	8
1.6 MISINGI YA NADHARIA	8
1.6.1 Nadharia ya Grice (1975).....	8
1. 7 YALIYOANDIKWA KUHUSIANA NA MADA	11
1.8 MBINU ZA UTAFITI	15
1.8.1 NJIA ZA UKUSANYAJI DATA	15
1.8.2 AZIMIO LA UTAFITI	15
1. 8.3 ENEO LA UTAFITI.....	16
1.8.4 WALENGWA.....	16
1.8.5 SAMPULI KIELELEZO	16

1.8.6 UCHANGANUZI WA DATA	16
SURA YA PILI.....	17
UBADILISHAJI MSIMBO: MBINU NA MIKAKATI MBALIMBALI.....	17
2.1 UTANGULIZI	17
2.1.1 Lugha katika mahubiri kanisani.....	17
2.2 MSINGI WA UBADILISHAJI MSIMBO	20
2.3 AINA ZA UBADILISHAJI MSIMBO.....	28
2.3.1 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha maneno	29
2.3.2 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha kirai.....	32
2.3.3 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha kishazi.....	33
2.3.4 Ubadilishaji msimbo kati ya sentensi	35
2.3.5 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi.....	37
2.3.6 Ubadilishaji msimbo kihali na kistiari	39
2.3.7 Ubadilishaji msimbo wa viulizi	40
2.4 MAJUKUMU YA UBADILISHAJI MSIMBO	41
2.5 ATHARI ZA UBADILISHAJI MSIMBO.....	48
2.6 UFUNGAMANO WA MISINGI YA UBADILISHAJI MSIMBO NA KANISA KATOLIKI	51
2.7 HITIMISHO.....	54
SURA YA TATU.....	55
UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA NENO NA KIRAI KATIKA MAHUBIRI	55
3.1 UTANGULIZI	55
3.2 WAHUBIRI NA UBADILISHAJI MSIMBO.....	57

3.3 UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA NENO	65
3.3.1 Ubadilishaji msimbo wa neno katika mahubiri	65
3.3.2 Ubadilishaji msimbo katika kirai	75
3.4 HITIMISHO.....	78
SURA YA NNE	79
UCHANGANUZI WA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA SENTENSI.....	79
4.0 UTANGULIZI	79
4.1 UBADILISHAJI MSIMBO KATI YA SENTENSI.....	79
4.2 UBADILISHAJI MSIMBO BAINA YA SENTENSI.....	85
4.3 UHUSISHAJI	90
4.4 UBADILISHAJI MSIMBO NA UHUSISHAJI	92
4.5 HITIMISHO.....	95
SURA YA TANO	96
5.0 HITIMISHO NA MUHTASARI	96
5.1 MAONI NA MAPENDEKEZO	101
MAREJELEO	103
VIAMBATISHO	108
MAHUBIRI YA 1- KANISA LA HOLY SPIRIT - GILGIL (NA ASKOFU)	108
MAHUBIRI YA 2 -KANISA LA HOLY SPIRIT– GILGIL (NA KASISI).....	115
MAHUBIRI YA 3- CONSOLATA WESTLANDS.....	125
MAHUBIRI YA 4 - HOLY FAMILY BASILICA	129

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuangalia matumizi ya lugha katika Kanisa Katoliki kwa kuchanganua ubadilishaji msimbo katika mahubiri. Utafiti ulitumia data iliyokusanywa kwa kurekodiwa katika makanisa teule matatu kwa kutumia nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975). Tuliongozwa na haipotesia zifuatazo; kwanza, kuwa ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu. Pili, wahubiri katika Kanisa Katoliki hubadilisha msimbo. Tatu ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi na nne kiwango cha elimu, tabaka, tajriba, cheo na umri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika. Iithibitika kuwa ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu, na kwamba wahubiri katika Kanisa Katoliki hubadilisha msimbo kwa wingi katika mahubiri ambapo ubadilishaji huu husababisha ukosefu wa urasmi. Aidha elimu, tabaka, tajriba, cheo na umri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia kwa muhtasari kile kinachofanywa katika utafiti huu kwa kutoa mwelekeo jinsi utafiti wenyewe utakavyofanyika. Sura ya pili imeshughulikia ubadilishaji msimbo kwa kuzingatia mbinu na mikakati mbalimbali. Imeshughulikia pia msingi wa ubadilishaji msimbo na aina za ubadilishaji msimbo. Majukumu na athari za ubadilishaji msimbo pia zimezingatiwa. Baadaye ufungamano wa misingi ya ubadilishaji msimbo na Kanisa Katoliki umeshughulikiwa. Sura ya tatu na ya nne zimehusika na uchanganuzi wa data kwa kutumia vijenzi na msingi wa nadharia ya Umaanisho juu ya ubadilishaji msimbo wakati wa mahubiri katika Kanisa Katoliki. Sura ya tano ni hitimisho na muhtasari ambapo tumetoa maoni na mapendekezo.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 USULI WA MADA

Dini na lugha ni vipengele ambavyo vimefungamana sana katika maisha ya mwanadamu kama vinavyotumika miongoni mwa jamii au watu fulani. Mawanda ya matumizi ya lugha huelezewa kama hali ambayo matumizi ya aina fulani ya lugha hutumiwa na kikundi ambacho ni mahsusi kama vile jumuiya ya waumini wa kanisa kwa ujumla. Jambo hili husaidia kukitambulisha kikundi hicho cha waumini kiisimu na kijamii (Pride, 1971). Hivyo kundi lolote lile katika jamii huweza kutambulikana katika misingi yake ya matumizi ya lugha kiisimu na kijamii.

Lugha hutumika tofauti tofauti katika nyanja na matumizi mbalimbali ya kijamii. Tofauti hizi katika lugha zinatufanya kuuliza iwapo matumizi haya yanachangiwa na muktadha husika. Je, mabadiliko haya katika matumizi yanachangiwa na mambo yapi? Kuna uwezekano kuwa elimu, hadhi katika jamii, umri au dini ikasababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika? Swali jingine ambalo huweza kuulizwa ni kwamba, Je, namna mtumizi wa lugha anavyoiwasilisha huchangia jinsi maana inavyopokelewa? Kunayo mikakati yoyote anayoitumia kulifanikisha lengo lake la mawasiliano na upitishaji ujumbe? Na iwapo ametumia mikakati hii, bado anaudumisha urasmi unaotakikana? Hali hizi zinatufanya sisi kama watafiti kuufanya utafiti huu tukijikita katika muktadha wa dini. Tutajiuliza iwapo lugha inavyotumika katika miktadha mbalimbali ya dini kufanikisha mawasiliano inaathiriwa na mambo gani katika kuyawasilisha mahubiri hasa katika Kanisa Katoliki.

Kanisa la Katoliki huweza kubainishwa kwa matumizi yake ya lugha ambayo yana upekee wake. Matumizi haya ya lugha katika kanisa hili mara nyingine yanaweza kupungukiwa katika kukosa ufaafu wa kuelezea masuala muhimu ya kitaaluma au masuala ibuka katika jamii hii ya dini ya Katoliki. Hali hii inatusukuma kuufanya utafiti huu kuangalia jinsi lugha inaweza kufaulu au kutofaulu kutimiza malengo yake katika mahubiri. Dini ya kikatoliki ni dini inayokua kila uchao kama dini yoyote ile katika nyanja zake zote kama vile kijamii, kiimani na kitaaluma. Tutachunguza iwapo ukuaji huu wake unaweza kupelekea uwepo wa matumizi ya ubadilishaji msimbo au uchanganyaji msimbo katika jitihada za kuuwasilisha ujumbe kwa waumini wa kanisa hili kupitia mahubiri.

Ni muhimu kufahamu kwamba matumizi haya ya lugha katika Kanisa Katoliki yana upekee wake tangu wakati lugha kuu iliyotumika katika misa ikiwa Kilatini hasa suala la kubadili msimbo na mitindo yake linapowaziwa. Tokea mwanzo wa karne ya ishirini, lugha rasmi ya Kanisa Katoliki katika ibada ilisisitizwa kuwa Kilatini. Hadi wa leo katika Kanisa Katoliki, katika seminari na vyuo vikuu vya kikatoliki wanaoandaliwa kuwa mapadri hufunzwa lugha za Kilatini na Kigiriki kama lugha asilia zinazodhaminiwa za kanisa hili. Kanisa Katoliki pia huchukulia mahubiri kama kiungo muhimu cha ibada (Turnbull, 1967). Katika mafunzo ya upadri, mojawapo wa kozi zinazofunzwa ni sayansi ya kuhubiri (homiletics). Waseminari hufunzwa namna ya kuitumia lugha pamoja na msisitizo wa kuelewa lugha rasmi za kanisa hili ambazo wanapaswa kuzitumia ikiwa ni pamoja na Kilatini na lugha za kienyeji. Wanapohitimu na kuwa mapadri, wanapaswa kujali wanavyoitumia lugha katika viwango vya maneno, sentensi, vishazi na aya katika mahubiri la sivyo ujumbe uliokusudiwa hautawasilishwa kwa ufaafu (New

Catholic Encyclopedia, 1967:113). Swali ni je elementi hizi za maneno, vishazi na sentensi zina athari gani katika namna lugha inavyotumiwa katika mahubiri?

Matumizi haya ya lugha basi yana utofauti yanavyotumika katika Kanisa Katoliki ikilinganishwa na matumizi yake katika makanisa ya kiprotestanti? Kwa vile Kanisa Katoliki huwa na utaratibu mahsusi wa kuendeleza ibada yake, matumizi ya lugha yake huwa na sheria na kanuni fulani za kuzingatiwa. Upekee wa matumizi ya lugha katika kanisa hili una dhima ipi katika kufanikisha mawasiliano na kupitisha ujumbe katika mahubiri? Ili kuielewa dini yoyote basi, ni muhimu kubaini matumizi yake ya lugha kwani bila lugha mawasiliano hayawezi kufaulu. King'ei (1992) anasema kuwa mtindo wa kidini huwa tofauti sana na matumizi ya lugha ya kawaida. Mara nyingi huwa ni vigumu kufahamika na watu wasioitumia lugha hii ya kidini pamoja na wale hawauelewi muktadha wake wa kimatumizi.

Habwe na Karanja (2004) wanaieleza lugha kama chombo cha mawasiliano ambacho huwawezesha watumizi wake kupashana ujumbe na hisia zao. Kutokana na maelezo haya jamii huitumia lugha kufanikisha mawasiliano. Kwa sababu hii utafiti huu utashughulikia uamilifu wa lugha kwa kutazama namna ubadilishaji msimbo unavyotumiwa kufanikisha mawasiliano katika mahubiri. Utaangalia elementi za kiisimu kama vile matumizi ya msimbo katika maneno, kirai, kishazi au sentensi. King'ati (2002) anasema kuwa mengi yaliyofanywa katika kanisa hili yaliegemea mtazamo wa kiteolojia. Pia anasema kuwa ni machache yaliyomo kuhusiana na diskosi hii kwa mwelekeo wa kiisimu. Ndiposa kuna haja ya kuvitazama vipengele vya dini na lugha katika mwelekeo wa kiisimu. Utafiti huu utachunguza hali ya kuchanganya msimbo na kubadili msimbo. Hizi ni dhana mbili ambazo zinatumiwa na wataalamu wengi kimpishano

(moja inatumika kuelezea nyingine) kama vile Furrakh Abbas na wengine (2011). Katika utafiti huu tutazitumia dhana hizi kimpishano. Stockwell (2002) akinukuliwa na Wanjugu (2010) anatoa maoni yanayooana na haya kuwa baadhi ya watu huashiria ubadilishaji msimbo kama uchanganyaji msimbo. Anaeleza kuwa dhana hizi mbili na nyinginezo bado hazijapata maelezo yaliyoafikianwa. Tutachunguza ubadilishaji msimbo unavyotokea na unapotokea wakati wa matumizi ya lugha katika mahubiri. Aidha tutajiuliza pia aina ya ubadilishaji msimbo unaotumiwa. Ili kufanikisha utafiti huu misingi ya nadharia ya Umaanisho (Grice, 1975) ilitumiwa katika uchanganuzi wa jinsi msimbo unavyotumika kuwasilisha maana. Grice (1975) anasema kuwa kuna uhusiano baina ya maana ya msemaji, maana inayotokana na vipashio vya sentensi na maana inayoibuka kulingana na maneno katika sentensi. Umaanisho basi utatuongoza katika kushughulikia maana inayojitokeza kutokana na maneno yanayotumiwa na mhubiri.

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Linda na Wareing (1999) wanadai kuwa kikundi fulani hutambuliwa kama kikundi cha jamii kilicho tofauti na kikundi kinginecho cha watu kutokana na matumizi yao ya lugha na tabia zingine za kiisimu kama vile matumizi ya msimbo katika mofimu, maneno, kirai, kishazi au sentensi. Hili lina maana kuwa jinsi watu wanavyoitumia lugha kama jamii fulani, ni rahisi kuwatambulisha kwa vile kuna sifa ambazo zitajidhihirisha zilizo tofauti na za jamii nyingine.

Kulingana na Code of Canon Law (1975) Kanisa Katoliki huwa ina upekee wake wa kuitumia lugha. Mapadri wanatakiwa watumie lugha za wenyeji katika kuifundisha dini na katika mahubiri. Lugha hii inafaa itumie misingi ya lugha husika. Inapaswa kuendeshwa katika hali iliyo rasmi kufuatia kanuni zake. Kipengele kinachotiliwa mkazo ni namna vishazi, sentensi au aya nzima zinavyochangia kuiwasilisha maana (New Catholic Encyclopedia, 1967).

Iwapo kanuni hizi hazizingatiwi kuna uwezekano wa kuwa na ukiukaji wa matumizi ya lugha kama inavyotarajiwa katika lugha husika? Je, ukiukaji huu huiathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu kama vile maneno, kirai, kishazi, sentensi kama zinavyotumika katika mahubiri? Inafaa kubaini iwapo aina za ukiukaji kama vile kuchanganya msimbo au kubadili msimbo zinachangia katika maana inavyowasilishwa. Vile vile kuangalia iwapo elimu, tabaka, hadhi na umri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

Lugha na dini vina historia ndefu kimahusiano hasa tunaporejelea umuhimu na uamilifu wa lugha katika Bibilia (Indede, 2007). Indede ametoa mchango wake katika kuitathmini lugha ya kitamathali ya dini. Hadi sasa hakuna mchango bayana ulioshughulikia suala la ubadilishaji msimbo katika Kanisa Katoliki. Utafiti huu utachunguza jinsi lugha inavyotumiwa katika Kanisa hasa katika ubadilishaji msimbo katika mahubiri kwenye ibada ya misa katika Kanisa Katoliki Jimbo kuu la Nairobi na Jimbo la Nakuru.

Ili kubaini ni kwa nini mhubiri amechanganya msimbo huu itabidi kwenda nyanjani kuangalia iwapo matumizi haya ya elementi za mitindo ya kubadilisha msimbo katika viwango mbalimbali yanafanikisha mawasiliano wakati wa mahubiri. Tutatafiti jinsi uchanganyaji msimbo huu, unavyoathiri maana katika kiwango cha ukiukaji wa matumizi ya lugha ya mahubiri na vile vile kujiuliza iwapo kunazo aina kadhaa za ukiukaji. Kutokana na ukiukaji katika mahubiri ndio kuna haja ya kujiuliza iwapo ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi ambacho ni kipengele muhimu kinachofaa kuzingatiwa katika mahubiri ya Kanisa Katoliki na pia kubaini iwapo lengo la matumizi ya lugha kuyafanikisha mawasiliano limefaulu.

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu utaongozwa na madhumuni ya jumla ambayo ni:

Kuchunguza jinsi mahubiri katika Kanisa Katoliki yamejaa wingi wa kuchanganya na kubadili msimbo.

Madhumuni mahsusi ya utafiti huu yatakuwa:

1. Kuchunguza jinsi ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unavyoathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
2. Kubaini ni kwa nini mhubiri huchanganya msimbo.
3. Kubaini iwapo ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi ambacho ni kipengele muhimu kinachofaa kuzingatiwa katika mahubiri ya Kanisa Katoliki.
4. Kuchunguza iwapo elimu, tabaka, tajriba, cheo na umri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

1.3 HAIPOTHESIA

1. Ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
2. Wahubiri katika Kanisa Katoliki huchanganya msimbo.
3. Ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi.
4. Kiwango cha elimu, tabaka, cheo, tajriba na umri wa mhubiri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

1.4 UMUHIMU WA UTAFITI

Dini ni kiungo muhimu katika jamii yoyote ile. Ili kutimiza majukumu yake, dini hutumia lugha katika mawasiliano kukidhi mahitaji ya wafuasi wake (Brown na Yule, 1983). Dini huwa na

lengo la kukuza mahusiano bora na thabiti yenye lengo la kukuza utangamano. Shabaha hizi haziwezi kutimilika bila ngazi maalum ambayo ni mhubiri anayetumika kama kiunganishi cha jamii kwa kuitumia lugha. Msingi huu utatuongoza kuiangalia lugha anayoitumia mhubiri kutimiza malengo yake.

Lugha anayoitumia katika mahubiri huwa na upekee wake unaoitofautisha na lugha ya makundi mengine (Gumperz na Hymes, 1972). Dini husheheni lugha yake iliyo tofauti na ya makundi mengine na hili hutokana na hali za ushirikiano pamoja na misingi ya dini husika. Sio kila binadamu mwenye uwezo wa kutekeleza shughuli hii ya mahubiri ila kasisi au mchungaji na labda aliye na tajriba au mazoea kuweza kuteka makini ya hadhira husika. Hivyo, hubidi anayehubiri kuitumia lugha itakayomwezesha kulitimiza hili. Lugha hii itamwezesha kukuza uhusiano na kuiwasilisha maana kwa kuilenga jamii yake (Hirst, 1986).

Utafiti huu unatazamiwa kuwa na machango mkubwa katika isimu na katika tafiti zilizofanywa awali za isimu. Utawafaa wasomi wengi sasa na baadaye katika kuupanua uelewa wao wa matumizi ya ubadilishaji msimbo katika diskosi ya dini. Jamii nzima kwa jumla itafaidi kutokana na kuelewa matumizi ya msimbo katika mahubiri. Unatazamiwa pia kuwa changamoto kwa wasomi wa baadaye kuonyesha ari yao katika tafiti zijazo katika msingi wa kidini hususan Kanisa Katoliki ambapo machache sana yamefanywa kuhusiana na msimbo na lugha kwa mtazamo wa kiisimu. Utafiti huu unatazamiwa kukuza fahari kwa washiriki wa kanisa hili katika kuona jinsi msimbo unavyofanikisha mawasiliano katika mahubiri.

1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Utafiti huu utajikita katika Jimbo kuu la Kanisa Katoliki Nairobi na Jimbo la Nakuru kwa sababu ya tofauti za hadhi ya majimbo haya mawili (moja ni Jimbo kuu na nyingine ni Jimbo). Utafiti huu utatumia makanisa teule ambayo ni Holy Family Basilica (Nairobi), Consolata Westlands (Nairobi) na kanisa la Holy Spirit - Gilgil (Nakuru) ambapo kuna mikusanyiko mbalimbali ya watu, wenye vyeo mbalimbali, hadhi, kazi mbalimbali, makabila mbalimbali na kadhalika. Tutachunguza mahubiri yatakapokuwa yakiendelea kwenye makanisa haya kwa kuyarekodi ili kuufanya utafiti kuweza kutegemeeka zaidi. Makanisa yaliyoteuliwa yanatazamiwa kuwa kiwakilishi cha matumizi ya ubadilishaji msimbo katika Kanisa Katoliki kwani sio rahisi kutafiti kanisa zima nchini Kenya. Matumizi ya msimbo yataangaliwa katika muktadha unaoangalia msimbo na matumizi yake katika mahubiri. Utafiti huu hautashughulika na sehemu nyinginezo za misa au baada ya misa.

1.6 MISINGI YA NADHARIA

Utafiti utaangalia matumizi ya msimbo katika mahubiri na kwa kufanya hivyo kuangalia maana inayotokana na msemaji. Hivyo tutaongozwa na Nadharia ya Umaanisho (Grice 1975) Tutaangalia yaliyoandikwa kuhusiana na nadharia inayotumika, mada (ubadilishaji msimbo) na kisha maelezo ya diskosi ya dini.

1.6.1 Nadharia ya Grice (1975)

Katika utafiti huu tutaongozwa na Nadharia ya Umaanisho iliyoasisiwa na Paul Grice (1975). Nadharia hii inabainisha uhusiano baina ya maana ya msemaji, maana inayotokana na vipashio vya sentensi na maana inayoibuka kulingana na maneno katika sentensi. Tutatumia nadharia hii kwa vile tunakusudia kuangalia ubadilishaji msimbo unavyotumika katika mahubiri na vile maana inavyowasilishwa kuyafanikisha mawasiliano. Nadharia hii hushughulika na maana

kulingana na msemaji. Umaanisho hushughulika na maana inayojitokeza kutokana na maneno ya msemaji.

Kuna kanuni ya ushirikiano kulingana na Grice ambayo inafafanuliwa katika kanuni nne ili kuyafanikisha mawasiliano. Alielezea kanuni nne za kufanikisha mawasiliano ikiwa ni pamoja na kanuni za idadi, ukweli, uhusiano na namna.

Kaida ya idadi inasema kuwa msemaji anapaswa kusema yanayotosheleza na yasizidi kiasi wala kupunguza taarifa ili kuweza kuwasiliana. Useme habari kamilifu. Nayo kaida ya ukweli inamtaka msemaji aseme kile kilicho cha ukweli. Habari zitakazotolewa ziwe na ukweli na msemaji asiseme habari ambazo anaamini ni za uongo au hana uhakika nazo. Asiseme kile hawezi kuthibitisha. Aseme yale ana ushahidi nayo. Kaida ya tatu ni kaida ya uhusiano inayomtaka msemaji atoe habari zinazohusiana na mada tu inayozungumziwa. Asiseme habari zilizoko nje ya mada au muktadha unaozungumziwa. Asiingize mambo yasiyohusiana na mada anayoshughulikia. Mwisho aliizungumzia kaida ya namna inayosema kuwa ujumbe uwe bayana, wazi na ulio dhahiri bila kuficha chochote. Ujumbe usiwe na utata, uwe na mpangilio na utaratibu mzuri aidha uwe mfupi. Lugha anayoitumia ieleweke na wasikilizaji wake bila tatizo lolote.

Mawazo haya yanaafikiana na ya Malmkjaer (2004:419) anayesema kuwa kanuni za Grice zina uhusiano na sifa kadhaa za diskosi ambazo hutokana na ukweli kuwa kama mazungumzo yatakuwa na urazini basi lazima yawe na matamshi yaliyo na uhusiano. Kinacholeta uhusiano huu ndicho kinajulikana kama kanuni ya ushirikiano inayodai mzungumzaji atoe mchango wake kama inavyotakikana, katika kiwango inapotokea, kwa lengo lifaalo na kwa kuegemea

mwelekeo unaotakikana katika mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa ili kufaulu kuitumia kanuni hii, wazungumzaji inafaa kuzingatia vijikanuni vingine vinne vya idadi, ukweli, uhusiano na namna. Katika kanuni ya idadi inayohusiana na idadi ya ujumbe utakaotolewa, mzungumzaji aufanye mchango wake kuweza kufahamisha iwezekanavyo katika muktadha uliopo wa mazungumzo. Mzungumzaji asifanye mazungumzo yake yazidi yanayotarajiwa.

Katika kanuni ya ukweli, mzungumzaji aufanye mchango wake kuwa wa kweli. Asiseme kile ambacho sio kweli au kile asichokuwa na ushahidi nacho. Nayo kanuni ya uhusiano inamtaka mzungumzaji kudumisha uhusiano. Asiyazungumze yale ambayo yatakuwa nje ya uhusiano uliopo. Kanuni ya nne ya namna inamhitaji mzungumzaji kujali namna anavyoseme aliyonayo. Aepukane na yale yasioeleweka, yenye utata, aseme kwa kifupi na awe na mpangilio wa kile anachokisema. Kaida hizi za Grice ni chukulizi na inatazamiwa msemaji atatoa yale yanayohusu kile kilichokusudiwa kwa njia iliyo wazi na yenye utaratibu. Ni chukulizi pia kuwa wazungumzaji wanapozungumza watazizingatia kaida hizi katika mawasiliano.

Kulingana na Grice, ikiwa mzungumzaji ataenda kinyume na kaida hizi kwa mfano kutopitisha ujumbe kama inavyotakikana, kusema uongo, kusema zaidi ya inavyostahili au pengine apotoke na msikilizaji asiweze kumwelewa kama inavyotakikana, basi itamfanya msikilizaji azue maana ambayo haikukusudiwa na kuzua utata. Umuhimu wa nadharia hii katika isimu unatokana na ukweli kuwa pragmatiki hujihusisha na kuibua maana kulingana na msemaji. Hivyo ni maana inayotokana na maneno ya msemaji.

Nadharia hii itatuongoza kwa sababu itatusaidia katika kuangalia jinsi msimbo unavyotumiwa katika mahubiri kubainisha uhusiano wa maana kati ya msemaji na msikilizaji. Aidha vile maana inavyobainika katika sentensi au kulingana na maneno yanayotumiwa. Utafiti huu utaongozwa na kanuni ya ushirikiano. Tumechagua nadharia hii kwa vile itafaa sana katika kuangalia matumizi ya ubadilishaji msimbo katika mahubiri.

1. 7 YALIYOANDIKWA KUHUSIANA NA MADA

Kama asemavyo Djoko Susanto (2006), kubadili msimbo ni matumizi ya lugha mbili au zaidi katika mazungumzo, na imekuwa ni mada ya kuvutia katika isimu kwa muda mrefu kwa watafiti. Hata hivyo tafiti nyingi za hapo awali zilichunguza msimbo katika diskosi mbalimbali ikiwemo siasa, sheria, falsafa na kadhalika. Ubadilishaji msimbo huu umeshughulikiwa na watafiti wengi kama anavyosema Djoko (2006) katika nyanja mbalimbali kwenye miktadha kama vile kielimu (Martin-Jones, 1995; Cheng, 2003), kortini (Drew, 1990; David, 2003), kifamilia (Williams, 2005), na katika mazingira ya kikazi (Venugopal, 2000). Hata hivyo ni machache sana yaliyofanywa kuhusiana na msimbo katika dini (Spolsky, 2003). Kwa kweli katika siku za karibuni, mwingiliano kati ya lugha ya dini kama mada zifaazo zinazohusiana na uwililugha na wingilugha zimeshughulikiwa kwa kiwango kidogo (Spolsky, 2003:81), ila kunayo michango iliyotambulika ya Barnes na Mahomed (1994) aidha Wong (2000) kuhusiana na dini (wakinukuliwa na Djoko, 2006).

Utafiti huu kinyume na tafiti za awali unalenga kuchunguza msimbo unavyotumiwa katika Kanisa Katoliki ambapo ni machache sana yamefanywa hususan katika mahubiri (Kingati, 2002). Mahubiri mengi yaliyoshughulikiwa yameangaliwa katika mtazamo wa kiteolojia. Scotton (1993) anaangalia msimbo kama somo ambalo halijashughulikiwa kwa mapana nchini

Kenya. Tutaangalia vile kuchanganya msimbo na kubadili msimbo hutumika katika mahubiri kama vipengele vya kiisimu na namna vinavyosaidia kujenga uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

Hata hivyo, licha ya umuhimu wake huu mtazamo wa diskosi ya dini umechukuliwa kimzaha (Chilton, 2004) na ni machache sana yanayojulikana kuhusiana na sifa za diskosi hii. Tafiti chache kama vile Neumann na wengine (2001); Muchnik (2005) wameangalia diskosi ya dini, wakijikita katika vipengele kama vile kejeli na masimulizi kama wanavyonukuliwa na Shaimaa (2012). Utafiti huu wao utatufaa sana kwa vile kama huu unashughulikia diskosi ya dini. Hata hivyo, utakuwa tofauti na huu kwa vile unashughulikia kejeli na masimulizi ambayo ni masuala tofauti na ubadilishaji msimbo tunaouangalia.

Bailey (2000) anaangalia Majukumu ya Kijamii ya Kuchanganya Msimbo miongoni mwa wana Dominiko wa Kiamerika. Alijikita katika kiwango cha wanafunzi wa shule za Sekondari. Uchunguzi wake utatufaa kwa vile tunaangalia kiwango ambacho ubadilishaji msimbo unatumika katika mahubiri ambapo kanisa ni kiungo muhimu cha jamii ila hatutajikita katika kiwango cha wanafunzi kama alivyofanya ila ibada kanisani. Muthuri (2000) anaangalia Majukumu ya Kubadili Msimbo miongoni mwa wanafunzi wenye wingilugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Utafiti huu utatuongoza kuangalia majukumu ya kubadili msimbo lakini utatofautiana kimaeneo kwa vile wao ulichunguza wanafunzi ilhali huu utatafiti wahubiri kanisani.

Uchunguzi mwingine ni wa Kanana (2003) ambaye ameangalia matumizi ya msimbo katika soko moja la 'Village Market' jijini Nairobi. Utafiti huu utatufaa kwa vile unafanywa eneo lililo sawa

la jiji la Nairobi lakini utafiti huu utalenga makanisa mbalimbali wala sio sokoni. Blom na Gumperz (1972) katika Djoko (2006) wanachunguza kuchanganya msimbo Norway. Utafiti huu utatofautiana na huu kwa vile tunaoufanya uko nchini Kenya aidha unahusu dini. Utafiti huu utatufaa kwa vile wameshughulikia kuchanganya msimbo ambalo ndilo lengo la utafiti huu isipokuwa tutajikita katika Kanisa Katoliki.

Romaine (1994) alitathmini kuchanganya msimbo na nafasi yake katika mawasiliano ya utendaji ya uwililugha. Alichunguza matumizi ya msimbo katika jamii moja ya Punjabi Uingereza. Aliangalia aina mbili za msimbo 'sisi' na 'hao'. Utafiti huu utatofautina na huu kimaeneo na msimbo utakaoshughulikiwa ila utatufaa kwa vile tunaangalia jamii ya waumini jinsi wanavyotumia ubadilishaji msimbo. Uchanganuzi wa kimtindo wa Lugha ya Wachuuzi na Lugha ya Matangazo umeshughulikiwa na Michira (1993) katika Kingati (2002). Aliangalia kuchanganya msimbo na matumizi ya lugha ya Kiswahili sahihi ya wachuuzi katika soko la Gikomba. Utafiti huu unafanana na tunaoufanya kimaeneo lakini unatofautiana kwa vile unahusu wachuuzi na huu unahusu lugha ya dini. Utatusaidia kwa vile kama yeye sisi pia tunaangalia uchanganuzi msimbo lakini katika mahubiri.

Kingati (2002) alishughulikia muwala na mshikamano katika mahubiri ya Kanisa Katoliki jijini Nairobi. Utafiti huu utatufaa sana kwa vile ni mojawapo ya zile chache zilizofanywa kwa mtazamo wa kiisimu zinazoshughulikia mahubiri ila utakuwa tofauti kwa vile huu unashughulikia ubadilishaji msimbo katika mahubiri. Msimbo nchini Kenya kutoka Ekugusi, Kiswahili, Kiingereza na Sheng umeshughulikiwa na Ogechi (2002). Utafiti wake utatufaa kwa

vile tutachunguza ubadilishaji msimbo ambao unaweza kutokea baina ya lugha mbili kama vile Kiswahili na Kiiingereza ila unatofautiana na huu kwa vile ni wa kidini.

Lugha ya siasa imeshughulikiwa na Habwe (1999). Anatahmini hotuba za kisiasa na kuziona changamano kwa vile huhusisha hadhira na mzungumzaji kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha mawasiliano. Anaiona hadhira kama yenye kuathiri mwelekeo wa yanayojadiliwa katika hotuba. Utafiti huu utatufaa katika kuangalia uhusiano kati ya msemaji na msikilizaji ila unatofautiana na huu kwa vile tutachunguza ubadilishaji msimbo katika mahubiri ambapo mhubiri hutumia hata majibu na maswali kuwasilisha ujumbe wake. Utafiti wake utatusaidia kuangalia matumizi ya lugha hususan ubadilishaji msimbo ambao ni tofauti na wake wa kisiasa.

Nguvu katika Diskosi ya Dini ilishughulikiwa na Andreia (2002). Aliangalia mahubiri mawili katika kanisa la kiprotestanti la 'Universal Church of the Kingdom of God'. Ameangalia nafasi ya ushawishi katika mazungumzo yaliyotolewa na mhubiri mmoja. Mtazamo wake utatusaidia sana katika kuangalia hali hii ya ushawishi ijapokuwa utakuwa tofauti kwa vile unalenga Kanisa Katoliki na wake ni wa kiprotestanti. Untener (1999) akinukuliwa na Kingati (2002) aliangalia hali ambayo mhubiri anahitaji kuikuza kati yake na hadhira yake. Anaangalia namna mahubiri yanavyokuwa na mshikamano. Utafiti huu utatufaa kuangalia uhusiano wa mhubiri na hadhira lakini hatutaangalia kipengele cha muumano. Djoko Susanto (2006) alishughulikia kubadili msimbo katika diskosi ya dini ya Kiislamu. Huu ni mchango mkubwa katika utafiti huu kwa vile una mwelekeo wa kidini kama huu isipokuwa umejikita katika dini ya Kiislamu tofauti na huu wa Kikatoliki.

1.8 MBINU ZA UTAFITI

Tutachanganua data ambayo tutakusanya kutoka nyanjani katika makanisa yaliyoteuliwa katika Jimbo kuu la Nairobi na Jimbo la Nakuru wakati wa mahubiri ambapo mkusanyaji data atashiriki ibada. Ibada ikiendelea, atajaribu kurekodi mahubiri. Mtafiti ataangalia ishara anazozitoa mhubiri na kuziandika na baadaye kuzichanganua. Mahubiri haya yatakusanywa Nairobi na Nakuru kwa vile makanisa mengi yana mchanganyiko wa makabila na hivyo lugha zinazotumika zitaufaa sana utafiti huu na kuufanya ufaulu. Mji wa Nairobi una mchanganyiko wa hali ya juu ya watu wanaozungumza Kiswahili na Kiingereza hata kuliko Nakuru hivyo kuna haja ya ulinganishi wa miji hii. Vile vile Kanisa Katoliki linatazamiwa kuwa na asilimia kubwa sana ya watu wanaojihusisha katika shughuli nyingi za kijamii. Aidha kujikita katika Kanisa Katoliki kuepukana na mbinu mbalimbali za mahubiri zinazopatikana katika madhehebu mbalimbali hali ambayo inaweza kuleta utata katika kuichanganua data. Tutayapanga mahubiri yalivyotolewa na kuuangalia ubadilishaji msimbo kama ulivyotokea na hatimaye kuchanganua kwa njia ya kutoa maelezo.

1.8.1 NJIA ZA UKUSANYAJI DATA

1.8.2 AZIMIO LA UTAFITI

Utafiti huu utafanywa nyanjani katika Jimbo kuu la Kanisa Katoliki la Nairobi na Jimbo la Nakuru kuangalia matumizi ya ubadilishaji msimbo katika mahubiri. Mtazamo utakaotumiwa ni mshiriki - mtazamaji. Mtazamo huu umechukuliwa kwa vile Jiji la Nairobi na Nakuru lina mchanganyiko wa watu na hivyo kuna matumizi ya lugha zaidi ya moja. Vile vile kuna uwezekano wa kupata watu wa tabaka na vyeo mbalimbali. Tumeamua kutumia majimbo mawili pia kwa vile miji hii ni tofauti katika hali zake za hadhi na mchanganyiko ya makabila ila kanisa

ni lile moja la Katoliki. Katika misingi ya kikanisa, hadhi za majimbo haya ni tofauti kwani kanisa la Nairobi lina hadhi ya juu (Jimbo kuu) ilhali la Nakuru ni la chini kidogo (Jimbo).

1.8.3 ENEO LA UTAFITI

Utafiti utafanyiwa katika makanisa teule ya Katoliki katika Jimbo kuu la Nairobi na Jimbo la Nakuru.

1.8.4 WALENGWA

Walengwa ni kikundi chochote cha watu au vitu ambavyo vina sifa zilizo sawa (Ogula, 1998). Makasisi watatu watachunguzwa namna wanavyotumia ubadilishaji msimbo katika mahubiri na pia askofu mmoja. Utafiti huu utafanyika katika makanisa ya Holy Family Basilica (Nairobi), Consolata Westlands (Nairobi) na Kanisa Katoliki la Holy Spirit-Gilgil (Nakuru) ambapo kuna mikusanyiko mbalimbali ya watu, wenye vyeo mbalimbali, hadhi, kazi mbalimbali, makabila mbalimbali na kadhalika. Tumeyateua makanisa haya matatu kama kiwakilishi cha kanisa zima la katoliki lenye mwongozo ulio sawa.

1.8.5 SAMPULI KIELELEZO

Kwa vile Kanisa Katoliki ni pana sana, haitakuwa rahisi kulitafiti kwa ujumla wake. Hivyo tutatumia kiasi kidogo cha kanisa hili zima cha wahubiri na wasikilizaji kutoka makanisa yaliyoteuliwa ili kuwakilisha kanisa zima. Tutatumia sampuli ya makusudi (Ogula, 1998) ambayo ni njia ya kuchagua kwa makusudi vitu au watu walio na habari anazohitaji.

1.8.6 UCHANGANUZI WA DATA

Baada ya kukusanya data tutazihifadhi katika kanda za sauti kisha kuzisikiliza kanda na kunakili yaliyomo kwenye karatasi. Baadaye data itachanganuliwa, kutafsiriwa na kutolewa maelezo ili kufikia mapendekezo na maoni ya mada ya ubadilishaji msimbo. Data itawasilishwa kwa kuzingatia malengo na nadharia ya utafiti.

SURA YA PILI

UBADILISHAJI MSIMBO: MBINU NA MIKAKATI MBALIMBALI

2.1 UTANGULIZI

Sura hii inazungumzia mbinu na mikakati mbalimbali katika ubadilishaji msimbo. Inaeleza lugha kama chombo muhimu katika mahubiri chenye mchango mkubwa katika namna ubadilishaji msimbo unavyotekelezwa. Vile vile tutaelezea msingi wa ubadilishaji msimbo na kuangalia maana na umuhimu wake kulingana na maoni ya wanaisimu mbalimbali na maoni ya mwenye kuufanya utafiti. Tutachunguza sababu zinazowafanya wahubiri kubadilisha msimbo na kuangalia aina za ubadilishaji msimbo hasa kwa kuzingatia mahali ambapo zinajitokeza kisarufi hususan katika kiwango cha neno na sentensi. Vile vile tutaelezea majukumu ya ubadilishaji msimbo pamoja na athari zake.

2.1.1 Lugha katika mahubiri kanisani

Wakati wa ibada, mhubiri hujipata katika hali ambayo inambidi kuwasiliana na hadhira yake kupitisha ujumbe alionao. Kufanikisha hili inabidi atumie mikakati mingi. Lazima awatosheleze waumini wake kwa kuwalisha neno la Mungu na kuhakikisha kuwa waondokapo kanisani wameelewa na wako imara kuendelea na shughuli zao kwa juma zima lijalo. Mhubiri inafaa aichangamshe hadhira yake na kuteka makini yao la sivyo watapotoka na kuelea anapoendelea na mahubiri.

Kilicho cha maana sana ni jinsi anavyoitumia lugha yake kuhakikisha kuwa wanaohubiriwa wanayafuata mahubiri ili kuridhisha hamu yao ya kuunganika na Mungu. Ni vema auzingatie muktadha na kuzingatia kanuni na sheria za lugha ya mahubiri. Mahubiri yake yanafaa

yadhihirishe upekee wa lugha unaofaa kuwoko katika lugha ya mahubiri kama anavyosema Brown na wenzake (1963: 158) kuwa matumizi mazuri ya lugha yanaweza kutofautisha mhubiri mmoja na mwingine. Aidha mahubiri yake yanatakiwa yadhihirishe kuwa anayazingatia mafunzo ya sayansi ya dini aliyofunzwa katika seminari. Mahubiri haya yanatakiwa kuwa tofauti na mengineyo kutoka kwa madhehebu mengine ili kutimiza malengo ya ibada ya misa ya Kanisa Katoliki.

Katika mahubiri mhubiri anaweza kusema waziwazi au akatumia lugha fiche kutegemea malengo mbalimbali. Matumizi haya yanakuwa na athari kwa wasikilizaji wake katika mahubiri anayoyawasilisha au kwa hadhira husika. Mhubiri anapohubiri anaweza kutumia mikakati kama vile ubadilishaji wa msimbo. Hali hii husababisha ukiukaji wa lugha kwa kutozingatia kanuni na sheria za lugha husika. Ukiukaji huu unaweza kuwa na athari katika namna ujumbe unavyoeleweka na kuwasilishwa.

Lugha ni chombo muhimu; sio tu kama njia ya kuwasilisha mawazo na elimu lakini pia kuujenga urafiki, utangamano wa kitamaduni na kiuchumi kwa washiriki katika maongezi. Katika historia yote ya mwanadamu, watu wengi wameangazia umuhimu wa lugha. Kanisa lahitaji lugha hii kwa vyovyote vile kwani ndio ngazi ya kuunganisha mhubiri na hadhira yake. Lugha huelezea mawazo na hisia kwa kubainisha kwa yakini mtazamo wa mtu. Lugha hii hutofautiana jinsi matumizi yake yalivyo tofauti. Hivyo, lugha huundwa kwa namna ya kuashiria kile mawasiliano huhusu. Huonyesha pia mahusiano kati ya washiriki ambayo huongozwa na majukumu ya kijamii na mahusiano kati ya washiriki katika mazungumzo na pia majukumu ambayo lugha inatekeleza katika mahusiano (Halliday 1973, 1994).

Uhusiano kati ya lugha na wazungumzaji ni kwamba hautenganishiki. Kila neno analolizungumza mtu huwa kifaa cha kumfunza kuhusu mazingira yake na jinsi binadamu anavyoyakabili katika harakati zake za kujiendeleza katika maisha. Lugha hutumiwa ili kuleta umoja katika jamii fulani. Lugha hufungua na wakati huo huo ikasisimua hisia za muungano wa kikabila au kitaifa pale inapojitokeza na kujidhihirisha kama chombo cha umoja miongoni mwa wazungumzaji wake. Mahali lugha yoyote inapotumiwa na watu wengi, huibuka matumizi ya lugha kwa namna tofauti tofauti (Mghambi, 1991).

Mawazo haya pia yanaelezwa na Crystal (1965) kuwa lugha ndicho chombo cha mawasiliano ambacho kimefungamanishwa na mahitaji mengi ya kijamii, huwa na sehemu kubwa katika jukumu la kanisa la kuwasilisha dini na kuonyesha washiriki jinsi ya kuwasiliana na Mungu. Hivyo, lugha inachukuliwa kama sehemu kubwa ya dini tangu mwanzo. Ukristo huitumia lugha katika majukumu yake. Ni dini yenye mwelekeo na inayoangazia maisha na mafundisho ya Yesu Kristo aliye mwana wa Mungu kama inavyoelezwa katika Biblia kwenye Agano Jipya. Imani hii ya Kikristo imetekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na kukuza ustaarabu. Haya yote hutekelezwa kwa kuitumia lugha yenyewe.

Hivyo lugha hutokea kutumiwa kwa njia tofauti ili kufanikisha mawasiliano. Mawasiliano huenda yakaegemea lugha ya uchanganyaji msimbo au ubadilishaji msimbo. Ubadilishaji msimbo huu unaweza kuhusisha elementi za kiisimu katika kiwango cha mofimu, neno, kirai, kishazi na sentensi. Sura hii imedhamiria kuangazia baadhi ya vipengele hivi kwani matumizi ya lugha hutokea kuegemea maswala kama haya wakati jamii mbalimbali wanapoitumia lugha.

2.2 MSINGI WA UBADILISHAJI MSIMBO

Habwe (1999) anasema kuwa msimbo umeelezwa katika fasiri ya kiisimu kama ubadilishaji kutoka lugha moja hadi nyingine katika tukio la kiuzungumzaji (Tazama; Oduol 1987; Richards na wengine 1985; Saville- Troike 1989). Bentahila na Davies (1982) wakinukuliwa na Oduol wanasema kuwa katika ubadilishaji msimbo tamko linalohusika hudhihirisha sifa za lugha tofauti zinazohusika. Kuchanganya msimbo ni tukio ambalo ni la kawaida nchini Kenya (Habwe; 1999, Romaine; 1989). Misimbo inayochanganywa mara nyingi ni Kiswahili na Kiingereza ingawa wakati mwingine watu huchanganya msimbo wakitumia lugha zao za kiasili kama vile Kijaluo, Kimaasai, Kikamba na kadhalika. Ubadilishaji msimbo huu aidha waweza kuwa ni kutoka lugha za kiasili hadi lugha za Kiswahili na Kiingereza.

Wazungumzaji hutumia lugha ya Kiingereza ambayo ni lugha rasmi, lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rasmi na pia ya kitaifa na lugha za kiasili. Hivyo, mazingira ni ya uwingilugha. Katika mazingira kama haya ubadilishaji msimbo hutokea. Vile vile ubadilishaji msimbo ni jambo ambalo hujitokeza kanisani kwa vile yapo mazingira ya uwililugha. Aghalabu wahubiri wengi hubadilisha msimbo kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili au lugha ya Kiswahili hadi Kiingereza. Hata hivyo wakati mwingine wao hubadilisha msimbo hadi lugha za kienyeji (Flannery, 1975). Katika utafiti huu tutazingatia ubadilishaji msimbo kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza au Kiingereza hadi Kiswahili. Tutachunguza sababu zinazowafanya wahubiri kubadilisha msimbo, ni aina ipi ya kubadilisha msimbo hujitokeza kanisani wanapobadilisha msimbo na ni kwa kiwango kipi ambacho wao hubadilisha msimbo.

Baadhi ya sababu zinazowafanya wahubiri kubadilisha msimbo ni kama vile kutaka kutumia muda au maneno machache kueleza jambo fulani, kunukuu, wahubiri kuwa na mielekeo hasi kuhusu baadhi ya istilahi za Kiswahili na pia wao hubadilisha msimbo wanapotaja majina ya kiteolojia ambayo hawana kisawe chake. Katika utafiti huu pia tutachunguza aina mbili za kubadilisha msimbo ambazo hujitokeza katika sentensi. Aina ya kwanza ni ubadilishaji msimbo unaotokea baina ya sentensi na aina ya pili ni ubadilishaji msimbo ambao unatokea kati ya sentensi. Vile vile kuna ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno na kirai.

Dhana ya ubadilishaji na uchanganyaji msimbo au ndimi ni tofauti kwani ubadilishaji msimbo huhusiana na kutumia lugha moja kwa muda na kuiendea ya pili baada ya muda ilhali uchanganyaji huhusiana na kuzitumia lugha mbili au zaidi kwa wakati mmoja. Hali zote hata hivyo hutokana na umilisi wa lugha mbili au zaidi walionao wazungumzaji. Kuchanganya msimbo ni dhana iliyopatiwa fasiri ya kiisimu kuwa na maana ya kuchopeka maneno au sehemu ya lugha moja katika usemi ambao uko katika lugha nyingine (Richards na wengine 1985, Saville –Troike 1989) wakinukuliwa na Ndungu (2001). Kwa mfano,

Mfano [1]

Tusiwe kama Wayahudi ambao walisema Mungu ni wetu, *‘we can not share our God’*.

(Tusiwe kama Wayahudi ambao walisema Mungu ni wetu, hatuwezi kugawana Mungu wetu).

(Ndungu, 2001).

Katika mfano huu wa [1] sentensi hii moja imegawanywa mara mbili na lugha husika za Kiswahili na Kiingereza. Kila sentensi imeundwa kwa kuzingatia sheria za utunzi za lugha husika.

Wataalam kama Fasold (1984) na Milroy (1987) katika Ndungu (2001) wamefanya ufafanuzi wa tofauti kati ya kuchanganya na kubadili msimbo. Hata hivyo, tutazitumia dhana hizi kimpishano (moja kuwakilisha nyingine) kama dhana zilizo na maana sawa. Kuchanganya msimbo hurejelea uhamishaji wa elementi za kiisimu kutoka lugha moja hadi nyingine na elementi hizi zaweza kuwa mofimu, maneno, kirai, kishazi au sentensi (Kachru, 1983). Kwa mfano,

Mfano [2]

Dunia hii *'for sure has many things; si you see'* jinsi mambo yalivyo mengi.

(Dunia hii kwa kweli ina mambo mengi, si unaona jinsi mambo yalivyo mengi).

Sentensi hii inaonyesha uhamishaji kutoka Kiswahili hadi Kiingereza katika viwango mbalimbali vya elementi za kiisimu. Uhamishaji huu hudhihirika pia katika mahubiri kanisani ukiwa na malengo mbalimbali. Katika mahubiri ubadilishaji msimbo ni kawaida kati ya Kiswahili na Kiingereza kwa sababu ya matatizo yatokanayo na majukumu ya lugha hizi mbili zinazotambulika kama lugha rasmi. Katika mahubiri ubadilishaji msimbo husaidia waumini hata wa kiwango cha chini kuuelewa ujumbe. Mhubiri hutumia Kiswahili katika mahubiri kwa lengo la kuwafikia waumini wake wote. Hata hivyo hujipata amezungumza Kiingereza katika muktadha ule ule.

Kwa mujibu wa Habwe, (1999) ubadilishaji msimbo ni ukiukaji wa kanuni ya namna ya Grice inayomtaka mzungumzaji azungumze kwa njia iliyo wazi kwa kutegemea sheria za uzungumzaji mahsusi. Mfano mzuri ni wakati mtu anayetaka kuonyesha kuwa ameelimika anazungumza Kijerumani mahali ambapo wengine waliopo hawaiielewi lugha hii. Kwa namna hii atakuwa anakiuka kanuni inayosisitiza uwazi katika uwasilishaji wa mawazo yake. Msimbo ni kipengele cha utamkaji ambacho kinapaswa kuwa kidogo kama mofimu au pana na changamano kama mfumo mzima wa lugha (Ayeomoni, 2006 katika Furrakh, 2011). Kwa kuzingatia msimbo basi tutajihusisha na kuchanganya msimbo na kubadili msimbo. Yee Ho (2000) akinukuliwa na Furrakh (2011) anaafikiana na hayo kwa kusema kuwa kuchanganya msimbo ni mchanganyiko wa elementi wa lugha moja au mifumo miwili ya lugha katika utamkaji sawa katika viwango mbalimbali.

Kubadilisha msimbo ni matumizi ya mifumo miwili au zaidi katika mawasiliano au mahusiano yaliyo sawa (Scotton na Ury, 1977 katika Furrakh, 2011). Nayo mawazo ya (Poplack, 1980) ni kuwa kubadilisha msimbo ni matumizi ya ubadilishaji wa lugha mbili katika diskosi moja kama ilivyodhihirishwa hapo awali. Tutaangalia kuchanganya msimbo na kubadili msimbo kama vipengele muhimu katika uwasilishaji wa mahubiri pamoja na sababu za matumizi yake katika kuiwasilisha maana. Wasemaji aidha hubadili msimbo kama njia ya kudumisha mawasiliano, uwajibikaji na pia kukuza mwingiliano wa kijamii (Akinyi na Kwach 2012).

Malmkjaer (2004) anasema kuwa wana umojalugha wanapowasikia wana wingilugha wakibadili msimbo, huwaangalia kwa mtazamo hasi wakiamini kuwa hali hiyo inadhihirisha hali ya kupungukiwa katika uelewa wa lugha zote mbili. Wana uwililugha wenyewe wanajitetea au

kuomba msamaha, na kuhusisha ubadilishaji msimbo na tabia zisizofaa za matumizi ya lugha. Hata hivyo, ubadilishaji msimbo ni jambo lenye dhamana na urazini na ni mkakati wa kiisimu unaofuata kanuni. Huwa kuna lengo na umantiki katika kubadilisha lugha.

Matumizi ya msimbo katika lugha ni jambo la kila siku na la kila mahali ambapo zaidi ya lugha moja huzungumzwa katika mawasiliano ya kila siku. Tutaangalia namna msimbo huu unavyotumika katika mahubiri aidha kuelewa unavyotumika na athari zake katika mahubiri unapotokea wakati wa matumizi ya lugha katika mahubiri. Kwa mfano wakati wa mahubiri mhubiri anaweza kusema kuwa,

Mfano [3]

‘Jesus will come’ kama mwizi.

(Yesu atakuja kama mwizi).

Katika mfano huu wa [3] mhubiri amebadilisha msimbo kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili kwa lengo la kufanikisha mawasiliano. Mfano mwingine pia ni;

Mfano [4]

Tumesikia katika somo la pili, Paulo *‘saying’*, akituambia ya kwamba *‘our talents are many’*.

(Tumesikia katika somo la pili, Paulo anasema, akituambia ya kwamba talanta zetu ni nyingi).

Ubadilishaji msimbo huu unachangia katika uelewa wa ujumbe kwa kuufanya uwe na mnato zaidi na kurahisisha uelewaji wake. Unasaidia pia katika namna ujumbe unavyopokelewa.

Scotton (1993) anaangalia msimbo kama somo ambalo halijashughulikiwa kwa mapana nchini Kenya. Haja yetu ni kujihusisha na kuchanganya msimbo na kubadili msimbo kama zinavyotumika katika mahubiri kama vipengele vya kiisimu na namna vinavyosaidia kujenga uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Ipara na Maina (2008:78) wanasema kuwa kuchanganya ndimi au msimbo ni hali ambapo wazungumzaji wanazungumza kwa lugha moja kisha hapa na pale, wakatoka kidogo katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na kisha kurejelea lugha ya awali. Kila mtu ambaye huongea, amejifunza kuhamisha ndimi kwa kutegemea hali na mahali alipo. Katika muktadha wa usomi kuchanganya ndimi kunaelezwa kama mazoea ya kuhamisha lugha baina ya lugha ya msingi na ile ya pili. Buliba na wenzake (2006: 73) wanasema uchanganyaji msimbo ni hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha mbili katika hali moja ya mazungumzo. Msemaji anaweza kuchanganya Kiingereza na Kiswahili;

Mfano [5]

'Seriously', huu ni mchezo mkubwa! *'Hakumind!'*

(Hakika, huu ni mchezo mkubwa! Hakujali!).

Mfano huu unadhihirisha matumizi ya lugha mbili katika sentensi moja ambapo kuna matumizi ya maneno ya lugha mbili katika mazungumzo na kuonyesha kuwa kuna umilisi wa lugha mbili. Buliba na wenzake (2006) wanaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo ni ile hali ya kubadilisha lugha wakati wa mawasiliano. Wanashikilia kuwa hili hutokea pale ambapo msemaji wa lugha ana umilisi wa zaidi ya lugha moja. Msemaji huweza kubadilisha mazungumzo yake

kutoka lugha moja hadi nyingine anapotokea kuathiriwa na hali iliyopo na mtindo; kimsingi hali hii hutegemea washiriki, mada na mandhari.

Madhumuni ya kubadilisha msimbo hutokana na haja ya mzungumzaji kusisitiza kile anachokisema. Inawezekana vile vile kubadilisha huku kukafanywa ili kudhihirisha hisia fulani. Wazungumzaji huenda wakatamia Kiswahili pamwe na Kiingereza. Kwa mfano;

Mfano [6]

'Congratulations', nilijua ungefaulu.

(Hongera, nilijua ungefaulu).

Mfano huu unatoa athari ya kusisitiza huku ukitoa hisia za kusikitisha katika kuonyesha hali ya kutojali na kuonyesha dhana ya mzaha.

Ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha kwa ujumla na huelezea tukio ambalo linaonyesha sarufi ya lugha zote mbili zikifanya kazi kwa pamoja. Hutokea wakati ambapo kuna wana uwililugha ambao huzitungumza lugha zote mbili (Fromkin and Rodman, 1998). Ni hali ambapo mzungumzaji huzungumza lugha mbili au zaidi na anaamua ni ipi atakayoitumia. Mambo kadhaa huathiri ubadilishaji msimbo. Crystal (1997) anauangalia upungufu wa uelewa wa lugha wa mzungumzaji kama mojawapo wa sababu pale ambapo mzungumzaji baada ya kushindwa kujieleza vilivyo na kikamilifu katika lugha moja, hubadilisha msimbo ili kuboresha lugha husika. Aidha anaelezea haja ya ushirikiano na kikundi maalum kama sababu nyingine. Ubadilishaji msimbo huu unaweza hata kuwatenga wengine katika kikundi fulani ambao hawaiielewi lugha husika.

Hali hii ndiyo Fasold (1997) katika (The Herald Online, 2011) anaita hali ya mwingiliano ya Herman, pale ambapo katika hali fulani, mzungumzaji anaweza kutaka kuonekana kama mmoja wa watu wenye asilia fulani ya kikundi kisichokuwepo au akataka kujitenga na kikundi fulani na hivyo basi hubadilisha msimbo. Crystal (1997) akinukuliwa na (The Herald Online, 2011) anaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo pia unaweza kuathiriwa na mtazamo wa mzungumzaji kumhusu msikilizaji ikiwa ni pamoja na kuwa na uhusiano wa kirafiki, kuchukizwa, kujitenga, kejeli, mzaha, kutilia mkazo au kutoridhika. Edwards (1983) naye anasema kuwa ubadilishaji msimbo huchangiwa na mambo kadhaa ya kisaikolojia kama vile kusitasita pamoja na mambo ya kisosiolojia kama vile mada, wahusika na muktadha.

Musyken na Appel (1987:117) akinukuliwa na Wanjugu (2010) wanaeleza ubadilishaji msimbo kuwa ni matumizi ya sarufi na leksia ya lugha mbili au zaidi katika usemi. Spolsky (1989:49-50) katika (Wanjugu, 2010) anaeleza ubadilishaji msimbo kuwa ni kuhama kutoka kwa lugha moja hadi nyingine katika mazungumzo, jambo ambalo hufanywa na watu wenye umilisi wa lugha. Zaidi anatoa ufafanuzi kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea kati ya sentensi mbili au zaidi au hata katika sentensi zenyewe katika kiwango cha virai na maneno.

Wales (1990, 2001:63) akinukuliwa na Wanjugu (2010) anaeleza ubadilishaji-msimbo kuwa ule uhamishaji unaotawaliwa na wazungumzaji katika lahaja moja na nyingine na pia katika vikao mbalimbali vya mawasiliano. Maelezo haya kuhusu ubadilishaji msimbo nakubaliana nayo kuwa ni hali ya kutumia lugha mbili au zaidi katika mazungumzo, lahaja na kadhalika ambapo msemaji anajadili juu ya mada fulani kwa lengo la kusisitiza au sababu nyinginezo.

2.3 AINA ZA UBADILISHAJI MSIMBO

Katika sehemu hii aina za ubadilishaji msimbo zitashughulikiwa kwa lengo la kuelewa msimbo unavyotokea na unapotokea wakati wa mahubiri katika Kanisa Katoliki. Saville (1989) akinukuliwa na Habwe (1989) anabainisha aina mbili za kubadilisha msimbo. Ubadilishaji katika kiwango zaidi ya kishazi (Intersentential) na ubadilishaji katika sentensi (Intrasentential) ambayo mara nyingine hujulikana kama uchanganyaji wa msimbo.

Naye Poplack (1981) anaeleza kuwa kuna aina tatu za ubadilishaji msimbo. Ubadilishaji msimbo unaotokea nje ya kishazi au sentensi, unaotokea kati ya sentensi au kishazi pamoja na ubadilishaji msimbo wa kiungo. Ubadilishaji msimbo unaotokea nje ya kishazi au sentensi ni ule unaotumia zaidi ya lugha moja katika sentensi au vishazi tofauti na hutokea mipakani mwa sentensi.

Mawazo haya ni sawa na ya Wanjugu (2010) anayesema kuwa aina za ubadilishaji msimbo zimeelezwa kutokana na mahali unapotokea katika daraja mbalimbali za sintaksia. Anaeleza aina zifuatazo; ubadilishaji msimbo katika kiwango cha maneno, ubadilishaji msimbo katika kiwango cha sentensi, ubadilishaji msimbo baina ya sentensi na ubadilishaji msimbo wa viulizi. Naye Romaine (1989) akinukuliwa na Ndung'u (2001) anasema kuwa, kuna aina tatu za kuchanganya msimbo; aina ya kwanza ni uambatishaji wa kiungo, uchopekaji wa maneno kati ya sentensi ni aina ya pili ilhali uchopekaji wa maneno miongoni mwa sentensi ni mfano wa tatu.

2.3.1 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha maneno

Huu hujitokeza katika kiwango cha maneno ya kategoria mbalimbali. Inaweza kuwa ni katika nomino, vitenzi, vivumishi na kadhalika. Hata hivyo, kama anavyoeleza Myers-Scotton (1993: 106-108) katika Wanjugu (2010) ni kuwa sio vijenzi vyote vya sarufi vinavyokubali hali ya ubadilishaji msimbo katika lugha fulani. Jambo hili ni kwa maana kuwa, lugha moja inaweza ikubali ubadilishaji msimbo wa kategoria fulani za maneno inapotumika na lugha nyingine, lakini kategoria nyinginezo zisikubali.

Kwa mfano, katika kanisa la Holy Family Basilica kasisi anasema;

Mfano [7]

‘*nikaconnect*’ kwa maana ya ‘nikaunganisha’.

Mfano [7] hapo juu unaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili inakubali ubadilishaji msimbo wa kiwango hiki ujitokeze katika kategoria ya kitenzi. Kitenzi ‘*connect*’ kina kubadili ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno.

Mfano mwingine wa Kishona unaoonyesha ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno ni;

Mfano [8]

“Dhewa usavanda *nedance*, unoda rubatsiro iwe...” (*The Herald online*, 15.09.11). Kitenzi ‘*dance*’ kinakubali ubadilishaji msimbo wa kiwango cha neno katika sentensi.

Mfano mwingine ni;

Mfano [9]

Chatinoziva chamunotaura chokwadi papepa penyu ‘*idate, day*’, zita renyu ‘*nemaclassifieds*’, pamwe ‘*nesport*’ zvayo...” (*The Herald online*, 15.09.11).

Sentensi hii imekubali ubadilishaji msimbo katika viwango vya nomino na kitenzi. Nomino ‘*date*’, ‘*day*’ na ‘*sport*’ pamoja na kitenzi ‘*classified*’ zimedhihirisha hili.

Kategoria ya vihusishi vya Kiswahili haikubali ubadilishaji msimbo wa aina hii. Kwa mfano,

Mfano [10]

The prayers started ‘*kabla*’ ya saa sita usiku.

(Maombi yalianza kabla ya saa sita usiku).

Kihusishi hiki ‘*kabla*’ cha wakati hakiwezi kukubali ubadilishaji msimbo kama inavyofanyika katika vitenzi. Mfano mwingine wa kihusishi cha mahali ni,

Mfano [11]

The Bible is good ‘*kuliko*’ any other book.

(Biblia ni nzuri kuliko kitabu kingine chochote).

Kategoria nyinginezo zinakubali kwa kiwango kidogo sana ikilinganishwa na aina nyinginezo za maneno. Maoni ya Myers-Scotton (1993) katika Chun (2001:4) kama anavyonukuliwa na Mwandije (2004) anasema kuwa ubadilishaji msimbo hautokei tu katika kirai, kishazi au sentensi bali pia katika neno. Scotton alitumia mifano ya lugha jozi kama vile Kiingereza na Kiswahili. Naye Romaine (1989) katika Ndung’u (2001) anasema kuwa, aina ya kwanza ya ubadilishaji msimbo ni uambatishaji wa kiungo. Kwa mfano:

Mfano [12]

'Me!' Natumaini hutaki kunituma huko ni mbali.

(Mimi! Natumaini hutaki kunituma huko ni mbali).

Uambatishaji huu hujumuisha uchopekaji wa kiungo au mshangao wa lugha moja katika usemi mwingine ambao umo katika lugha nyingine. Kuchanganya msimbo huonyesha sifa ya sentensi ambayo ni lugha moja kuweza kuwa na ulumbi (Poplack, 1980).

Katika lugha ya Kiswahili, neno linaweza kutumiwa katika ubadilishaji wa msimbo chambilecho Malmkjaer (1991: 62) kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea katika kiwango cha sentensi, kishazi, kirai na maneno. Kwa mfano,

Mfano [13]

Walipokutana jana 'church' waliamuaje?

(Walipokutana jana kanisani waliamuaje?)

Mfano huu umetumia ubadilishaji msimbo wa neno. Ubadilishaji huu unahusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza ambapo neno 'church' la Kiingereza limechopekwa katika sentensi ya Kiswahili.

Poplack (1980) anaeleza kuwa mara nyingi watu huingiza neno moja kutoka lugha nyingine kwa sababu wamesahau au hawajalijua lile neno katika lugha ya msingi ambayo inatumika katika sentensi hiyo. Kwa mfano,

Mfano [14]

Mkutano wa ‘*Episcopal*’ ulipitisha mambo mengi jana.

(Mkutano wa Baraza la Maaskofu ulipitisha mambo mengi jana).

Neno ‘*Episcopal*’ limetumika kwa sababu ya kutolijua neno hili katika lugha ya Kiswahili na hivyo linatumika katika lugha ya Kiingereza. Hili linatokana na kuwa hana kisawe cha neno hili katika lugha ya Kiswahili. Mhubiri pia huweza kukumbwa na hali hii pale ambapo anatazamia kuelezea dhana fulani na akakosa kisawe cha neno analokusudia kulitumia na hivyo basi anaishia kuchanganya au kubadili msimbo.

2.3.2 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha kirai

Oduol (1987), akinukuliwa na Habwe (1999:95) anasema kuwa ubadilishaji msimbo unaotokea katika mipaka ya sentensi au kishazi hutokea pia katika kiwango cha neno, kirai, kishazi na uchanganuzi wake unatambulikana kutokana na matumizi yake katika neno, kirai na kishazi.

Kwa mfano,

Mifano [15]

‘*This preacher*’ anachangamsha sana.

(Mhubiri huyu anachangamsha sana).

Ubadilishaji msimbo huu umetokea katika kiwango cha kirai ambacho ni ‘*This preacher*’.

Unahusu ubadilishaji msimbo katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

Mfano mwingine ni,

Mifano [16]

Kumfuasa Kristo *'is necessary'*.

(Kumfuasa Kristo ni jambo muhimu).

Mfano huu umetumia kirai cha Kiingereza *'is necessary'* ambacho kimetumiwa katika sentensi ya Kiswahili. Kishazi hiki kinaonyesha kuwa ni muhimu kwa anayemwamini Kristo kumfuasa katika maisha yake. Mifano iliyotajwa ina ubadilishaji msimbo wa kuchanganya lugha za Kiswahili na Kiingereza katika kiwango cha kirai. Spolsky (1989) akinukuliwa na Wanjugu (2010) anasema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea kati ya sentensi mbili au zaidi au hata katika sentensi zenyewe katika kiwango cha virai na maneno.

2.3.3 Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha kishazi

Huu ni ubadilishaji msimbo unaotokea katika kiwango cha kishazi katika sentensi.

(Oduol 1987) akinukuliwa na Habwe (1999:95) anasema kuwa ubadilishaji msimbo unaotokea katika mipaka ya sentensi au kishazi hutokea pia katika kiwango cha neno, kirai na kishazi.

Uchanganuzi wake unatambulikana kutokana na matumizi yake katika neno, kirai na kishazi.

Ametoa mfano wa kubadilisha msimbo kutoka lugha ya Kindonesia hadi Kiingereza katika kiwango cha kishazi. Kwa mfano,

Mfano [17]

Batuuuuuk! Minum obat apa ya? *'Suggestion please'*.

(Cough! What medicine should I take? Suggestion please).

Anabadilisha msimbo kutoka Kindonesia hadi Kiingereza. Anatumia kishazi cha Kiingereza kuuliza maoni kwa yule wanayezungumza naye kuhusu dawa ya kukohoa anayotakiwa kuitumia.

Kwa kubadilisha msimbo hadi Kiingereza, anautilia mkazo ujumbe wake ili kupata maoni kutoka kwa marafiki zake. Hii ni aina ya ubadilishaji msimbo unaotokea mipakani mwa sentensi.

Mfano mwingine ni;

Mfano [18]

Bales '*comment*' orang bisa tapi bales '*message*' penting gue ga bisa. '*Get a life*'.

(You can reply the other's comments but you cannot reply my important message. Get a life).

(Poplack,1980).

Kishazi cha Kiingereza '*get a life*' katika mfano [18] ni nahau ya Kiingereza cha Kiamerika. Kishazi hiki '*get a life*' kinamaanisha kitendo ambacho kinahitaji au chenye uhusiano wa mtu mwenyewe. Kinamaanisha pia msukumo wa kuwa mtu mbunifu katika mahusiano yote. Kishazi hiki kinatakiwa kuwadhihaki watu ambao hawajali kuhusu matukio muhimu. Mzungumzaji amebadilisha msimbo kudhihirisha hasira aliyonayo na ubadilishaji huu umetokea bila kukusudia ili kutoa hisia zake.

Romaine (1994) anasema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kuwa ndani ya neno, ubadilishaji katika sentensi, au ubadilishaji msimbo katika kiwango zaidi ya kishazi. Ubadilishaji msimbo ndani ya neno hutokea katika neno lenyewe kwa mfano katika mpaka wa mofimu. Ubadilishaji katika kiwango zaidi ya kishazi (Intersentential) hutokea nje ya kishazi au sentensi, yaani katika mipaka ya kishazi ilhali ubadilishaji katika sentensi (Intrasentential) hutokea katika mipaka ya sentensi au kishazi.

2.3.4 Ubadilishaji msimbo kati ya sentensi

Unajitokeza katika kiwango cha virai, vishazi na sentensi ambapo lugha mbili au zaidi zinatumika katika sentensi moja. Musyken na Appel (1987:118) wakinukuliwa na Wanjugu (2010) wanaeleza kuwa ubadilishaji msimbo wa aina hii hutokea katikati mwa sentensi na mara nyingi huitwa uchanganyaji msimbo. Aina hii ya ubadilishaji msimbo umejitokeza sana katika mahubiri yaliyorekodiwa kama itakavyodhihirishwa baadaye. Ni ubadilishaji ambao maneno ya Kiingereza na Kiswahili yanabadilishana nafasi katika sentensi. Sridhar na Sridhar (1980:203-215) akinukuliwa na Mwandije (2004:22) wanasema ubadilishaji katika sentensi ni ule ambao elementi ngeni ambazo zina muundo wake wa ndani hutokea katika sentensi ya lugha pokezi na kufuata sheria za uwekaji za lugha ya wenyeji. Kwa mfano;

Kasisi wa Holy Family Basilica anasema,

Mfano [19]

Kuna sherehe tatu za umuhimu sana; kwanza kuzaliwa kwake Kristo ‘*incarnation*’, pili kufufuka ‘*resurrection*’ na tatu ‘*pentecost*’.

(Kuna sherehe tatu za umuhimu sana; kwanza kuzaliwa kwake Kristo, pili kufufuka na tatu , ujio wa Roho Mtakatifu).

Katika mfano huu, maneno ya Kiingereza na Kiswahili yanabadilishana nafasi katika sentensi. Maneno ‘*incarnation*’, ‘*resurrection*’ na ‘*pentecost*’ yametokea katika sentensi ya lugha ya Kiswahili na kufuata sheria za uwekaji za lugha hiyo. Mfano mwingine ni;

Mfano [20]

Lakini mimi *'I will never forget my teacher'*.

(Lakini mimi sitawahi kumsahau mwalimu wangu.)

Huu ni mfano wa ubadilishaji msimbo katika kiwango cha kishazi ambacho ni *'I will never forget my teacher'* na ambao umetokea katika sentensi moja katika lugha tofauti.

Poplack anaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo unaotokea nje ya kishazi au sentensi hupatikana sana katika uchanganuzi wa data. Hutokea katika kiwango cha neno, kishazi au kirai katika sentensi moja katika lugha tofauti. Mfano mwingine ambao umetokea katika lugha tofauti ni;

Mfano [21]

(Kindonesia na Kiingereza),

Padahal uda *'spare'* waktu yg lmyan buat kumpul *'project'* hari ini, tp ttp aja kurang ini itu! *'Next'*-ny ga deh...huhu...

(Though already spared enough time to collect today's project, but there is always something missing! The next will not be like that ...huhu...) (Poplack, 1980).

Ubadilishaji msimbo katika mfano [21] pia hutokea katika kirai na kishazi ndani ya sentensi. Umebadilisha msimbo kati ya Kiingereza na Kindonesia. Naye Romaine (1989) akinukuliwa na Ndung'u (2001) anasema kuwa, uchopekaji wa maneno kati ya sentensi ni aina ya pili ya ubadilishaji msimbo.

Mfano [22]

'Alienda mjini kutafuta kazi' And you know what- 'hakuwa na mtu wa kumsaidia'.

(Alienda mjini kutafuta kazi, na unajua nini? Hakuwa na mtu wa kumsaidia). (Ndungu, 2001).

Sentensi hii imetumia uchopekaji wa maneno kati ya sentensi kwa kubadili msimbo kutoka Kiswahili hadi Kiingereza. Kishazi cha Kiingereza kimetokeza katikati ya vishazi vya Kiswahili.

Mfano mwingine kama huu ni;

Mfano [23]

Yeye aliuliza, na inawezekana wakati mmoja jina langu liingie kwa *'record ya guinness?'*

(Yeye aliuliza, na inawezekana wakati mmoja jina lake liingie katika rekodi ya wenye vipaji maalum?)

Ubadilishaji katika mfano [23] una kuchanganya Kiswahili na Kiingereza hasa kufanya maana ya Kiingereza kuchukua muundo wa Kiswahili katika upatanishi wa kisarufi.

2.3.5 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi

Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi hujitokeza baina ya sentensi mbili au zaidi katika usemi.

Sentensi moja au zaidi inakuwa katika lugha moja na kisha hiyo au hizo nyingine zinazofuata zinakuwa katika lugha nyingine katika usemi au matini fulani. Kwa mfano katika mahubiri ya Holy Spirit Gilgil kasisi anasema,

Mfano [24]

Na basi siku hiyo kama kanisa tukaona rehema za Mungu zilitushukia kupitia kwa watu mia tatu arubaini na sita waliopewa sakramenti ya kipaimara. *'This is a sign of growing church'.*

(Na basi siku hiyo kama kanisa tukaona rehema za Mungu zilitushukia kupitia kwa watu mia tatu arubaini na sita waliopewa sakramenti ya kipaimara. Hiyo ni dalili na ishara ya kanisa linalokua).

Poplack anaendelea kusema kuwa kishazi na sentensi zinafaa katika ubadilishaji msimbo mipakani mwa sentensi. Ametoa pia mfano katika kiwango cha sentensi.

Mfano [25]

'Suddenly I really miss "grocelix16"... ' kangen kangen kangeen.

(Suddenly I really miss "grocelix16"... miss miss miss)

Mfano [25] unaonyesha ubadilishaji msimbo unatokea wakati mpangilio wa elementi uko sawa katika lugha zote mbili. Maneno 'miss' na 'kangen' yana maana sawa. Urudiaji wa maana ya maneno haya unaonyesha hamu ya hali ya juu ya "grocelix16". Sentensi ya kwanza imeandikwa kwa Kiingereza na ya pili inaonyesha kuwa urudiaji mara tatu wa neno la Indonesia 'kangen' umefanywa katika lugha ya Indonesia. Ubadilishaji msimbo huu unatokea mipakani mwa sentensi ya kwanza na ya pili. Huu basi ni ubadilishaji msimbo mpakani mwa sentensi. Romaine (1989 katika Ndung'u 2001) anaelezea uchopekaji wa maneno miongoni mwa sentensi kama mfano wa tatu wa ubadilishaji msimbo. Kwa mfano,

Mfano [26]

Tafadhali uje tuonane kesho bila kukosa. *'Will you keep our promise?'*

(Tafadhali uje tuonane kesho bila kukosa. Utaweka ahadi yetu?)

Ubadilishaji katika mfano [26], hujumuisha kubadilisha sentensi kwa namna ambayo kila kishazi au kila sentensi huwa katika lugha moja. Sentensi moja hugawanywa mara mbili na lugha zinazohusika. Kila sehemu ya sentensi huundwa kwa kuzingatia sheria za utunzi wa sentensi wa lugha husika. Kwa mfano,

Mfano [27]

Amejenga kwa siku nyingi, haonyeshi kumaliza karibuni... *'maybe he lacks some materials'*.

(Ameanza kujenga kwa siku nyingi, haonyeshi kumaliza karibuni labda amepungukiwa na vifaa vingine).

Mfano huu unaonyesha ubadilishaji msimbo mpakani mwa sentensi ambapo kila kishazi kiko katika lugha moja. Kishazi cha Kiingereza *'maybe he lacks some materials'* kinatilia mkazo wazo kuwa ukosefu wa vifaa ndio ambao umechangia ujenzi kuendelea kwa siku nyingi.

2.3.6 Ubadilishaji msimbo kihali na kistiari

Wardhaugh (1998:99-113) akinukuliwa na Mwandije (2004) anasema kuwa kuna aina mbili za ubadilishaji msimbo; ubadilishaji msimbo kihali na ubadilishaji msimbo kistiari. Ubadilishaji msimbo kihali ni wakati lugha inayotumika hubadilika kutokana na hali waliyonayo wazungumzaji. Wao huzungumza lugha moja katika hali moja na nyingine katika hali tofauti lakini hakuna kubadilika kwa mada. Ikibidi kubadilika kwa mada kuhitaji kubadilika kwa lugha basi itajulikana kama ubadilishaji wa kiistiari.

Mfano [28]

Sote tunaelewa mgonjwa alizidiwa kwa ukosefu wa uwajibikaji wa daktari. *'Lack of enough experience'*.

(Sote tunaelewa mgonjwa alizidiwa kwa ukosefu wa uwajibikaji wa daktari. Ukosefu wa ujuzi wa kutosha).

Ubadilishaji huu wa Kiswahili na Kiingereza unaonyesha hali ya mgonjwa inayosababishwa na ukosefu wa uwajibikaji. Hakuna kubadili mada ila kuna kuzungumza lugha tofauti katika hali tofauti.

2.3.7 Ubadilishaji msimbo wa viulizi

Hujitokeza katika sehemu ya viulizi ambapo viulizi vya lugha moja kati ya zile zinazotumika katika usemi hutumiwa katika kuuliza swali. Musyeken na Appel (1987:118) wakinukuliwa na Wanjugu (2010) wanaeleza kuwa aina hii huhusisha viulizi, vihisishi au sehemu nyingine yoyote ya sentensi ambayo huja baada ya maelezo na hutambuliwa kwa kuwepo na koma au kistari kifupi baada ya maelezo hayo. Haugerud na Njogu (1991; 11) wakinukuliwa na Habwe (1999) wanasema kuwa hata wazungumzaji walio chini katika uelewa wao wa Kiingereza wanajitahidi kubadilisha msimbo katika Kiingereza ili kujiinua hata katika viwango vya juu nchini Kenya na vyenye mamlaka ya juu. Saville –Troike (1989) katika Habwe (1999) wanasema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutumika katika kiwango cha mtu binafsi kujieleza.

Wardhaugh (1998:99-113) akinukuliwa na Mwandije (2004) anaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo unamwezesha mzungumzaji kufanya mambo mengi kama vile kusema kwa nguvu, kuweka msimamo usioegemea upande wowote wakati wa matumizi ya misimbo yote miwili, kujitambulisha na kudumisha utangamano. Licha ya majukumu haya yote mzungumzaji hukiuka kaida za uhusishaji kwa kutenda na kusema zaidi ya yale aliyotakiwa kuyatenda. Hali hii inaweza kuathiri uhusiano baina yao. Kutokana na mifano hii ni kuwa kunazo aina tofauti za ubadilishaji msimbo. Utafiti huu utajikita katika ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno,

kirai na sentensi huku tukitoa mifano kutoka mahubiri yaliyorekodiwa. Hili litashughulikiwa katika sura zifuatazo.

2.4 MAJUKUMU YA UBADILISHAJI MSIMBO

Watafiti wengi wameshughulikia suala la ubadilishaji msimbo kwa mapana kama inavyodhihirishwa na Gumperz (1982), Sert (2005) na Holmes (2008) katika Poplack (1980). Mawazo haya yanaoana na ya Kanahouse katika Jones na wenzake (1971:131) akinukuliwa na Wanjugu (2010) anayeeleza kuwa kila kitendo katika hali ya kawaida kinaweza kuhusishwa na sababu tofauti. Anatoa maelezo zaidi kwamba huko kuhusishwa au maelezo ya kutokea kitendo fulani hufanyika kwanza iwapo kitendo huchukuliwa kwa ujumla. Kutokea ubadilishaji msimbo huchangiwa na mambo mengi. Anaeleza kuwa mambo haya yamejadiliwa na wanaisimu wengi kama vile Blom na Gumperz katika Gumperz na Hymes (1972:424-426), Buliba na wenzake (2006, Myers – Scotton (1993), Trudgil (2000) na wengineo katika Wanjugu (2010).

Katika sehemu hii tutaangalia baadhi ya sababu za ubadilishaji msimbo kuona yanayochangia kutokea kwake. Hatimaye katika sura zifuatazo tutatoa mifano kama ilivyodhihirika katika utafiti tuufanyao. Baadhi ya sababu za ubadilishaji msimbo ni kubadilisha mada, kukazia ujumbe, kutaniana, kutoa hisia, kunukuu, kuonyesha utangamano, kutafsiri, kulinganisha, kuhanikiza (interjection) na urudiaji, kuelezea sifa, kupasha habari, matumizi ya tasifida, kuhimizana na kuonyesha shukrani.

➤ Kubadilisha mada

Mzungumzaji hubadilisha msimbo ili kujadili mada fulani.

Mfano [29]

‘Tafadhali sema mambo mengine, *‘am tired of gossips’*.

(Tafadhali sema mambo mengine, nimechoka na masengenyo).

Ubadilishaji msimbo huu unaonyesha kuwa mada iliyokuwa inajadiliwa ni masengenyo na kuna haja ya kuachana nayo ili kujadili mambo mengine. Ubadilishaji msimbo umetumiwa ili kutoa dhana hii.

➤ **Urudiaji**

Maneno au virai hurudiwa katika sentensi kwa lengo la kusisitiza hoja au kuelezea zaidi.

Inaweza pia kutumiwa kuteka nathari ya msikilizaji. Kwa mfano,

Mfano [30]

Tubuni dhambi na kuamini injili, *‘repent and again I say repent so as to be forgiven’*.

(Tubuni dhambi na kuamini Injili, tubuni nasema tena tubuni ili kusamehewa dhambi).

Msisitizo ulioko hapa ni kutubu dhambi ndio maana kuna kurudia neno la Kiingereza *‘repent’*.

➤ **Kutilia mkazo ujumbe**

Katika kutilia mkazo, mzungumzaji harudii rudii maneno au virai lakini hubadilisha msimbo ili kudhihirisha ujumbe unaokaziwa.

Mfano [31]

‘Since I live at boarding house, my signal is always up. Is it a sign that soon I will have a girlfriend’. *Haidhuru*.

(Kwa vile naishi nyumba ya kukodisha, ishara yangu daima inaonekana, ni ishara kuwa hivi karibuni nitapata mwenzi. Haidhuru.)

Mzungumzaji anatilia mkazo hoja kuwa hivi karibuni atapata jiko kwa kutumia kirai ‘*Haidhuru*’.

➤ **Kutania /mzaha**

Mzungumzaji hutumia namna hii wakati anataka kuelezea mawazo na hisia zake kwa njia isiyo ya kawaida hivyo hubadilisha msimbo katika lugha nyingine. Hutumia msimbo kutoa athari za kuchangamsha. Mzungumzaji huwa na nia ya kuburudisha au kuchangamsha.

Kwa mfano,

Mfano [32]

‘*Marvellous,*’ sikujua wewe ni hodari wa mlo hivyo!

(Makuu hayo, sikujua wewe ni hodari wa mlo hivyo!)

Ubadilishaji huu unatoa athari ya kutania pamoja na kuchangamsha kuonyesha msikilizaji mmoja anavyodhamini kula.

➤ **Kuelezea hisia**

Mzungumzaji hubadilisha msimbo kuelezea hisia nyingi. Anaweza kuonyesha huzuni, furaha, hasira, kukata tamaa, kuchusha au hisia nyinginezo. Ubadilishaji huu huwa sio wa kimaksudi.

Mfano [33]

‘Nataka kuwauliza nyinyi wakristo, mnaelewa athari za ‘*mortal sins?*’

‘Nataka kuwauliza nyinyi wakristo, mnaelewa athari za dhambi za mauti?’

Ubadilishaji msimbo huu unaonyesha kuwa mzungumzaji ana hasira au huzuni kuhusiana na dhambi za mauti ambazo anauliza wakristo kama wanajua athari yake.

➤ **Kufurahisha marafiki**

Mzungumzaji hubadilisha msimbo kwa nia ya kufurahisha marafiki.

Mfano [34]

Furaha yangu ‘*dear friends*’ ni kuwa nanyi hapa leo.

(Furaha yangu marafiki zangu ni kuwa nanyi hapa leo).

Ubadilishaji msimbo huu unaonyesha raha ya kuwa pamoja na marafiki.

➤ **Kunukuu**

Mzungumzaji hubadilisha msimbo kwa nia ya kuonyesha hadhi au cheo au kunukuu maneno kutoka kwa wengine, kutoka kwa nyimbo au Biblia. Mawazo haya yanaoana na ya Saville-Troike (1989) akinukuliwa na Habwe (1999) anayesema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutumiwa katika kunukuu.

Mfano [35]

‘*You will be a blessing.*’ ‘Wewe utakuwa baraka’, Bwana akasema.

(Utakuwa Baraka. Wewe utakuwa baraka, Bwana akasema). (Ndungu, 2001)

Mzungumzaji amenukuu maneno ya Biblia kuonyesha kuwa yale si maneno yake lakini kama yalivyo katika Biblia.

➤ **Kuonyesha utangamano**

Katika ubadilishaji huu mzungumzaji hutaka kujitambulisha na kuonyesha uhusiano kati ya washiriki. Hubadilisha msimbo kutoka lugha moja hadi nyingine kama ishara ya kuonyesha umoja wa kuwa katika kundi husika.

Mfano [36]

‘All of us here are not new’, tunaelewa mambo haya *‘comrades’* tangu mwanzo na inabidi tuendelee na mipango kama kawaida.

(Sote hapa sio wageni, tunaelewa mambo haya wenzangu tangu mwanzo na inabidi tuendelee na mipango kama kawaida).

Mzungumzaji katika ubadilishaji msimbo huu anaonyesha kuwa wanaelewana na wana utangamano ishara kuwa huwa wanafanya mambo kwa pamoja.

➤ **Kupasha habari**

Ubadilishaji huu unatumika kupashana habari kati ya mzungumzaji na wasikilizaji hivyo lengo huwa ni kupashana habari au kuelezea kwa uwazi zaidi.

Mfano [37]

‘You know what’, kuna mkutano wa dharura kesho kwa waumini wote.

(Unajua nini, kuna mkutano wa dharura kesho kwa waumini wote).

➤ **Kutafsiri**

Mzungumzaji hubadilisha msimbo ili kuitafsiri lugha ili kufanya neno lieleweke.

Mfano [38]

Neno katoliki linamaanisha ulimwengu wote, '*that is universal*'.

(Neno katoliki linamaanisha ulimwengu wote, ulimwengu wote).

Neno Katoliki limeelezwa kwa lugha ya Kiingereza ili lieleweke.

➤ **Kuonyesha shukrani**

Mzungumzaji hubadilisha msimbo ili kutoa shukrani kwa mtu kwa jambo alilotendewa ikiwa ni kwa Mwenyezi Mungu pia. Kwa mfano,

Mfano [39]

Vema kabisa, '*feel appreciated*'.

(Vema kabisa, jisikie umetolewa shukrani).

Mfano [40]

Akhirnya dapat juga no nyaaa....! '*Thank God*'

(Finally, I get the number..! Thank God)

➤ **Tasifida**

Tasifida ni matumizi ya neno au kirai ili kubadili na neno ambalo linaonekana la kuudhi kuliko lile linalowekwa mahali pake. Ubadilishaji msimbo huu hutumiwa kupunguza hali ya ukali katika neno.

Mfano [41]

'*Excuse me*', naenda pembeni.

(Samahani, naenda pembeni).

Sentensi hii imebadilisha msimbo kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kupunguza makali kwa kusema '*kwenda pembeni*' ambayo inatoa hali ya matumizi lugha ya adabu.

➤ Kulinganisha

Ubadilishaji msimbo huu huhusisha kubadilisha msimbo hata katika lugha za mama ili kukazia uelewa wa jambo.

Kwa mfano,

Mfano [42]

Ukweli ni kwamba: unapotakikana, utaambiwa chochote. Babangu husema, "*nyako kapodi idwari, gimoramora itimoni!*"

(The truth is that when you are wanted, you will be told anything. My father says, "if a lady is wanted then she is given anything she wants.") (Akinyi na Kwach, 2012).

Ubadilishaji msimbo huu unakazia ujumbe wa mwanamke anayependwa kwamba anaweza kupewa chochote ili akubali upendo kutoka kwa mwanamume.

Malmkjaer (1991:57-65) anasema kuwa wana uwililugha hubadilisha msimbo na kuchanganya msimbo wakati wa kuwasiliana na kila mmoja wao wanaozungumza lugha sawa. Anaeleza sababu mbalimbali za kubadilisha msimbo kama vile; wazungumzaji wanaweza kusahau msamiati katika lugha anayoizungumza na hivyo hulazimika kubadilisha msimbo katika lugha

tofauti. Wakati mwingine neno ambalo linakaribiana kimaana na jingine linaweza kuwa sababu ya kubadilisha msimbo. Mzungumzaji pia anaweza kunukuu usemi wa mtu mwingine katika lugha mzungumzaji alikuwa anaizungumza. Anaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutumiwa kutoa hisia alizonazo mtu, kuonyesha mahusiano ya karibu, utangamano na pia kumtenga mtu katika mazungumzo yanayoendelea.

Mawazo haya yanaoana na ya Finlayson na Slabbert (1997:123) katika Mwandije (2004) anayaeleza kuwa jukumu kubwa la ubadilishaji msimbo ni kuweza kumjali msikilizaji ikiwa ni pamoja na; kujali kile msikilizaji anadhamini na kubadili msimbo kulingana na hali, kuweza kuanzisha uhusiano ulio sawa wa kuweza kukubaliana na msikilizaji katika matumizi ya lugha, kuwa tayari kuelewa na kujihusisha na lugha nyinginezo katika hali ya mawasiliano kwa kiwango cha hata kufanya bidii zaidi ya inavyotakikana, kuweka mikakati ya kuweza kujitahidi kuelewa, na kuyafanya mazungumzo kuweza kueleweka kama iwezekanavyo. Kwa kuziangalia sababu hizi tunaona wajibu mkubwa unaotekelezwa na mzungumzaji hata katika kukuza kaida ya uhusishaji wa Grice na kuzitimiza kanuni za ushirikiano.

2.5 ATHARI ZA UBADILISHAJI MSIMBO

Kila tendo huwa na athari ambazo hufuatia baada ya kutokea kwake (Wanjugu, 2010). Athari hizo huenda ziwe hasi au chanya. Zaidi tendo fulani huenda likasababisha tendo lingine. Ubadilishaji msimbo kama tendo linalotokea katika matumizi ya lugha, bali na kuwa na sababu mbalimbali zinazochangia hali yenyewe, vile vile huwa na athari zake. Hili linapotokea linasababisha mazungumzo zaidi iwapo ilikusudiwa kujenga uhusiano wa karibu. Hali hii italeti ukiukaji wa kanuni ya idadi ya Grice inayodai kuwa msemaji aseme yanayotosheleza na yasizidi wala kupunguza taarifa ili kuwezesha mawasiliano. Ubadilishaji msimbo ukitokea katika kikundi

fulani na uwe ulilengwa kuwashirikisha watu wote , basi mtu hujihisi kuwa na uhuru wa kushiriki na kuwasiliana bila wasiwasi. Kwa njia hii huwa msemaji na msikilizaji wanajenga uhusiano na kuimarisha ushirikiano ambao ni kaida mojawapo ya nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975).

Kwingineko, ubadilishaji msimbo unaweza kuyasimamisha mazungumzo iwapo matumizi ya hali yenyewe ilikusudiwa kujenga mpaka au uhusiano wa mbali kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Iwapo katika usemi wa watu wawili kutatokea mtu mwingine asiyehitajika kupata kile kinachozungumzwa, ubadilishaji msimbo utatokea. Hali hii ikitokea itakuwa imevunja kanuni ya uhusiano ya Grice inayomtaka mzungumzaji kutoa habari zinazohusiana na mada tu. Ajiopushe kuingiza mambo yanayohusiana na mada tu. Katika hali kama hii watu wengine huachwa kando na hivyo basi mazungumzo yanaweza kutoenda mbali. Aidha ubadilishaji msimbo huenda umetokea kuashiria kuwa mada iliyokuwa ikizungumziwa imebadilika. Uwepo wa mada mpya huenda ukakatisha mazungumzo na hata watu wengine kujitoa hivyo kuuharibu uhusiano.

Katika Kanisa Katoliki kama ilivyodhihirika katika utafiti huu, kunayo matumizi ya ubadilishaji msimbo kwa wingi. Wahubiri wanapohubiri wanayaingiza maneno ya Kiingereza, Kiswahili na hata lugha nyinginezo kama Kilatini na Kiitaliano kama itakavyodhihirika katika sura zifuatazo. Hali hii ya kukosa kumakinika katika lugha moja inaweza kuvunja kaida za ushirikiano za Grice na hata kubadilisha msimbo mahali pasipofaa kubadilishwa. Vile vile mazoea haya ya ubadilishaji msimbo yatawafanya wahubiri hawa kuubadilisha msimbo wakati wowote hata katika hali zinazohitaji uwepo wa urasmi.

Kwa mfano,

Askofu anatumia neno lililo sawa la Kiswahili na Kiingereza kudhihirisha hili.

Mfano [43]

Kwa hivyo ninyi, kila mmoja wenu, anaitwa ‘*mroho*’ ‘*spiritan*’, si ndio?

(Kwa hivyo ninyi, kila mmoja wenu, anaitwa mroho, mroho, si ndio?)

Ubadilishaji huu [43] ungehitaji urasmi ambapo askofu angeelezea walio na Roho Mtakatifu hata kwa lugha ya Kiswahili na ingeeleweka lakini ametumia lugha ya Kiingereza kusisitiza anachokisema.

Wakati mwingine inabidi kuzieleza dhana zinazohusiana katika lugha zaidi ya moja kama ilivyodhihirika katika utafiti huu ili kudumisha mawasiliano. Mara nyingi itabidi mhubiri ayaeleze kwa lugha inayoeleweka zaidi iwapo alikuwa ametumia lugha tofauti na hivyo ukiukaji wa kanuni ya idadi unatokea unaomtaka asiseme zaidi ya kile anapaswa kusema. Vinginevyo, ubadilishaji msimbo kama ilivyojitokeza katika utafiti huu unaweza kusababisha uelewa wa rahisi pale ambapo inabidi kuelezea kwa mapana kwa kutumia zaidi ya lugha moja huku akitoa athari ya kusisitiza ijapokuwa kuna ukiukaji wa kaida za ushirikiano. Athari nyinginezo ambazo zinaweza kujitokeza ni kama ukopaji. Mzungumzaji anaweza kutumia lugha zaidi ya mbili kwa pamoja, wakati mwingine dhana zilizo mpya katika lugha moja huingia katika lugha hiyo na jina la kuiashiria dhana hiyo pia likaingia, hivyo kupelekea ukopaji. Ubadilishaji msimbo unaweza pia kusababisha mabadiliko ya baadhi ya kaida zilizoko katika lugha husika ya jamii fulani kama ilivyojitokeza katika lugha ya mahubiri ya Kanisa Katoliki ambapo kunapaswa kuwa na sheria zake zinazodhihirisha upekee wake wa matumizi ya lugha.

2.6 UFUNGAMANO WA MISINGI YA UBADILISHAJI MSIMBO NA KANISA KATOLIKI

Lugha ni chombo muhimu katika uwasilishaji wa mahubiri. Katika utafiti huu imedhihirika kuwa bila lugha Kanisa Katoliki haliwezi kufua dafu katika kuyatekeleza majukumu yake ya kuwaunganisha waumini wake na Mungu na kuwalisha neno lake takatifu linalowapa tumaini na utulivu moyoni. Hivyo, bila lugha lengo hili halitaafikiwa vilivyo kwani uhusiano uliopo kati ya lugha na wazungumzaji wake hautenganishiki. Katika harakati hizi za kuwalisha waumini kwa neno la Mungu, wahubiri katika kanisa hili kama ilivyodhihirika hutumia mikakati mingi ikiwa ni pamoja na ubadilishaji wa msimbo. Ubadilishaji wa msimbo huu huchochewa na mambo mengi kama vile kutaka kuudumisha uhusiano uliopo kati ya msikilizaji na mzungumzaji na pia haja ya kuiwasilisha maana ya msemaji vilivyo na kuifanya ieleweke.

Katika jitihada hizi ubadilishaji msimbo huu hutokea katika viwango mbalimbali na hata kuutoa utofauti wa mahubiri mbalimbali ya jinsi wanavyoitumia lugha kama ilivyojitokeza katika utafiti huu. Ubadilishaji msimbo huu ulitokea katika viwango mbalimbali vya neno, kirai, kishazi na sentensi. Aidha ulidhihirisha matumizi ya lugha mbalimbali kama vile Kiswahili, Kiingereza, Kiitaliano na Kilatini.

Katika kanisa hili pia ubadilishaji msimbo huu ulijitokeza kutimiza majukumu mbalimbali. Makasisi waliotafitiwa walibadilisha msimbo kwa lengo la kubadilisha mada ili kujadili jambo alilokusudia mhubiri.

Kwa mfano, kasisi wa Holy Spirit - Gilgil katika kuonyesha umuhimu wa kutoa zaka na kufanya watu waliwazie hili anasema;

Mfano [44]

It is important to sanctify ourselves and present our offertory to God in faith and dignity. Inspired by the words of our Lord Jesus Christ during the institution of the Holy Spirit when he said, *‘Twaeni mle wote, huu ndio mwili wangu utakaotolewa kwa ajili yetu’*.

(Ni muhimu kujitakasa na kutoa zaka yetu kwa Mungu kwa imani na heshima. Tukielekezwa na maneno ya Yesu Kristu wakati wa kuwekwa Ekaristia aliposema, *‘Twaeni mle wote, huu ndio mwili wangu utakaotolewa kwa ajili yetu’*).

Kasisi huyu wa Gilgil anabadilisha msimbo kutoka Kiingereza hadi Kiswahili na anazungumzia mambo mawili ya kutoa zaka na pia kupokea mwili na damu ya Yesu Kristo.

Jukumu la kusisitiza na kutilia mkazo lilijitokeza sana katika mahubiri yaliyorekodiwa ya kanisa hili. Wahubiri hawa walikuwa na nia ya kuelezea zaidi walichokisema.

Kasisi wa Basilica anasema,

Mfano [45]

Kwa nini mwanadamu anatoa matamshi ambayo yanatenganisha watu? *‘Why?eh Why?’* Kwa nini? Tunatenda dhambi. Kwa nini familia zinavunjika? *‘Why?’*

(Kwa nini mwanadamu anatoa matamshi ambayo yanatenganisha watu? Kwa nini? eh Kwa nini? Tunatenda dhambi. Kwa nini familia zinavunjika? Kwa nini?)

Ubadilishaji huu wa mfano [45] pia unakazia ujumbe anaokusudia kuupitisha kasisi huyu wa watu kutenda dhambi. Pamoja na kutekeleza haya jukumu linalotekelezwa na ubadilishaji msimbo huu pia ni kuelezea hisia tofauti tofauti katika kupitisha ujumbe kama vile hasira. (Kwa nini familia zinavunjika?) na kadhalika. Utani au mzaha ni jukumu linalotekelezwa na

ubadilishaji msimbo na linajitokeza katika mahubiri ya Kanisa Katoliki. Kasisi wa Holy Spirit – Gilgil alisema;

Mfano [46]

‘What a hell is that?’ Si msembe hiyo pepo mbaya ishindwe (ishindwe)!

Pepo gani huyo? Si msembe hiyo pepo mbaya ishindwe (ishindwe)!

Kasisi huyu anatumia maneno ya Kiswahili kuonyesha hali ya utani ijapokuwa anatumia njia hiyo kupitisha ujumbe alionao wa kukemea tabia mbaya za kujihusisha na tabia zilizo kinyume na maisha ya mkristo.

Ubadilishaji msimbo pia unaweza kutekeleza jukumu la kunukuu. Kwa mfano,

Mfano [47]

Yohana *‘seventeen twenty one (17:21)’*,

(Yohana kumi na saba, ishirini na moja.)

Mnukuu huu umetumika kunukuu maneno kutoka Biblia. Mnukuu huu umetumika kurejelea kifungo cha Biblia.

Mfano [48]

Leo tunasherekea sikukuu ya Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa Kilatini tunasema, *‘Corpus Christi’*, kwa Kiingereza *‘The Body and the Blood of our Lord Jesus Christ’* kwa Kiitaliano ni *‘Il Santissimo Corpo e Sangue di Cristo’*.

Katika mfano [48] kasisi anatafsiri lugha kutoka Kilatini na Kiitaliano hadi Kiswahili na Kiingereza. Lengo lake ni kukazia umuhimu wa sikukuu ya Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Mfano mwingine unaokazia analolisema kasisi wa Holy - Spirit Gilgil ni;

Mfano [49]

..... utaona logo ya Jimbo la Katoliki la Nakuru iliyo na maandishi ya Kilatini, *'ut unum sint'*, meaning, *'that all may be one'*.

Kutokana na mifano hii ni wazi kuwa ubadilishaji msimbo katika Kanisa Katoliki unayo majukumu mengi ikiwa ni pamoja na athari kubwa katika jinsi ujumbe unavyopokelewa na kueleweka kupitia kwa maana ya msemaji kama anavyodai Grice (1975) na hivyo kukuza ushirikiano na utangamano.

2.7 HITIMISHO

Sura hii imezungumzia maswala muhimu ya kimsingi yanayoendana na matumizi ya lugha katika Kanisa Katoliki. Kwanza suala la ubadilishaji msimbo limezungumziwa ambapo imedhihirika kuwa mtumiaji wa lugha huenda akachagua kubadili msimbo wakati wa mahubiri. Aina za ubadilishaji msimbo zimeangaziwa pia na kuonekana kuwa kuna aina mbalimbali za ubadilishaji msimbo ikiwa ni pamoja na katika kiwango cha neno au sentensi. Kisha majukumu yanayotekelezwa na ubadilishaji msimbo yameangaziwa na baadaye takajadili athari za kuutumia ubadilishaji msimbo katika mahubiri kanisani Katoliki.

SURA YA TATU

UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA NENO NA KIRAI KATIKA MAHUBIRI

3.1 UTANGULIZI

Kubadilisha msimbo ni swala ambalo tumeliangazia hapo awali kwa mapana na linavyotokea katika viwango mbalimbali katika lugha. Katika sura iliyotangulia, tuliona kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kuwa katika kiwango cha neno, kirai, kishazi na hata pia katika sentensi. Ubadilishaji msimbo kama unavyoeleweka kulingana na utafiti huu ni swala ambalo limejitokeza katika mahubiri yaliyotafitiwa na limeshirikisha kuwa kuna wingi wa ubadilishaji msimbo na unaochangiwa na ushirikiano baina ya kasisi na waumini wake.

Imedhihirika kuwa, nchini Kenya wazungumzaji hutumia lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili katika ubadilishaji msimbo na wakati mwingine hata lugha za kiasili. Ubadilishaji huu unatokea katika mazingira ya uwingilugha. Mazingira haya yanachangia kutokea kwa ubadilishaji msimbo. Ubadilishaji msimbo huu pia hujitokeza kanisani kwani kunayo mazingira kama haya ya uwililugha yanayomsukuma mzungumzaji kubadilisha msimbo. Hili pia huwapata wahubiri ambao hubadilisha msimbo kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili au lugha ya Kiswahili hadi Kiingereza. Ubadilishaji huu umezoeleka na kuonekana kama jambo la kawaida kanisani Katoliki.

Katika sura hii ubadilishaji msimbo kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza uliangaziwa. Suala la ubadilishaji msimbo liliangaziwa ili kudhihirisha linavyochangia katika uwasilishaji wa mahubiri katika Kanisa Katoliki. Lililotiliwa maanani ni jinsi wahubiri hubadilisha msimbo, aina za ubadilishaji msimbo unaojitokeza kanisani wanapobadilisha msimbo na ni kwa kiwango kipi ambacho wao hubadilisha msimbo.

Wahubiri walionekana kubadilisha msimbo katika viwango mbalimbali wakiwa na sababu zilizowafanya kubadilisha msimbo kama vile kutaka kutumia muda au maneno machache kueleza jambo fulani, kunukuu kifungu fulani kutoka lugha nyingine, wahubiri kuwa na mielekeo hasi kuhusu baadhi ya istilahi za Kiswahili wanazozitumia na kadhalika. Katika lugha ya dini pia kunaweza kuwa na msamiati wa kiteolojia ambao hawana kisawe chake na hivyo kulazimika kuitumia lugha tofauti. Ubadilishaji msimbo mwingine huwa si wa kimaksudi au unaolenga wasikilizaji bali huweza kutokea kwa vile mzungumzaji hana mbinu nyingine yoyote ya kuwasiliana.

Ubadilishaji msimbo katika kanisa hili ulidhihirisha matumizi ya lugha ya Kilatini na Kiitaliano japo kwa kiwango cha chini kama cha asilimia 5% tu. Mhubiri kwa kutumia ubadilishaji msimbo huu alidhihirisha upekee wa lugha ya dini ya Kikatoliki ambapo hili ni mchango mkubwa katika utafiti huu. Buliba na wenzake (2006:73) wanaeleza kuwa ubadilishaji msimbo ni hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha mbalimbali katika hali moja ya mazungumzo. Katika utafiti huu sababu za ubadilishaji msimbo zilionyesha utofauti wa wahubiri katika matumizi ya lugha huku wengine wakiwa na wingi wa ubadilishaji msimbo ilhali wengine ulijitokeza katika uchache wake.

Utafiti huu ulitumia watafitiwa wanne; askofu mmoja na makasisi watatu. Watafitiwa hawa walikuwa na sifa nyingine zilizokaribiana na kuoana sana na pia nyingine zilizotoa utofauti wao. Watafitiwa watatu (askofu, kasisi wa Holy Family Basilica na kasisi wa Holy Spirit - Gilgil) wana kiwango sawa cha elimu cha uzamifu ilhali yule wa Westlands ana kiwango cha uzamili.

Kasisi wa Holy Spirit - Gilgil na yule wa Holy Family Basilica wana vyeo sawa; wote wawili ndio viongozi wa makanisa yao (Paroko) na hivyo ndio wachungaji wakuu katika makanisa yao ilhali askofu ni kiongozi wa Jimbo, hivyo ni mchungaji wa waumini na mapdri wote wa jimbo lake. Kicheo yeye yuko juu ya makasisi waliotafitiwa.

Askofu pamoja na kasisi wa Holy Spirit – Gilgil wamesomea uzamifu na uzamili Italia. Tofauti ya kasisi wa Holy Spirit na askofu ni kuwa kasisi huyu licha ya kusomea Italia pia amefanya kazi huko na pia Uingereza. Hili limemfanya kuwa na ulumbi wa lugha. Umri wa watafitiwa hawa ni tofauti ila hawajaachana kwa kiwango kikubwa. Askofu ana umri wa miaka arobaini na mitano, kasisi wa Holy Spirit miaka arobaini na mitatu sawia na yule wa Consolata Westlands ilhali yule wa Basilica ana zaidi ya miaka arobaini na mitano. Watafitiwa hawa wote ni wananchi wa Kenya isipokuwa yule wa Consolata Westlands mwenye asili ya nchi ya Uganda. Asilia yake ilidhihirika jinsi alivyobadilisha msimbo. Tofauti hizi za watafitiwa zimejitokeza katika namna walivyobadilisha msimbo.

3.2 WAHUBIRI NA UBADILISHAJI MSIMBO

Wahubiri ni sehemu muhimu ya jamii katika kutekeleza mawasiliano. Katika utafiti huu wahubiri waliochunguzwa walielekea kutumia ubadilishaji msimbo katika mahubiri yao. Ubadilishaji msimbo huu ulidhihirisha kuwa na athari kubwa jinsi ujumbe ulivyopokelewa na waumini. Ubadilishaji wao ulihusu lugha za Kiswahili, Kiingereza, kwa kiasi kidogo Kilatini na Kiitaliano. Dell (1974) akinukuliwa na Bazerman (2008) anasema kuwa ubadilishaji msimbo ni mpishano wa matumizi ya lugha mbili au zaidi na pengine pia katika mitindo ya uzungumzaji. Kiitaliano na Kilatini kilijitokeza kwa kiwango cha chini ikifahamika kuwa ni lugha ambazo hadhi yake ni ya chini nchini Kenya ikilinganishwa na Kiswahili na Kiingereza. Kiswahili na

Kiingereza ndizo lugha kuu zinazotumika katika ibada kwa vile kuna watu kutoka makundi tofauti ya lugha mbalimbali wanaoishi pamoja mijini (Magesa, 1993). Hata hivyo kujitokeza kwa matumizi ya Kilatini na Kiitaliano ni mchango mzuri kwani lugha kama ya Kilatini ndiyo msingi au lugha asilia katika mahubiri katika Kanisa Katoliki na inayosaidia kutoa upekee wa matumizi ya lugha katika kanisa hili (Canon 828). Matumizi ya lugha hizi mbili yalijitokeza kwa kasisi mmoja wa Gilgil ambaye kiwango chake cha elimu ni cha juu aidha msukumo alio nao baada ya kujifunza kuzitumia lugha hizi katika usomaji wake ambapo anaonekana kupendelea kuzitumia. Kasisi huyu ana ulumbi wa lugha unaojitokeza katika uzungumzaji wake.

Halliday (1964:76) akinukuliwa na Ndungu (2001) anaeleza kuwa lugha hudhihirika katika tajriba za kijamii (na wala si katika ombwe). Na papo hapo ndipo inapata misingi, sura na ruwaza zake. Uamilifu mkubwa wa lugha kama tukio la kijamii ni matumizi yake kama tukio la mawasiliano baina ya wanajamii. Tamko la lugha haliwezi kueleweka ipasavyo ikiwa litafasiriwa pekee pasipo kuhusishwa na maswala mengine ya muktadha na hali ya watu waliohusika, ujuzi wao, mahusiaono kati yao, mada inayozungumziwa, uwanda wa taaluma, mahala au mazingira waliyomo na masharti mengine mengi.

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa cheo, hadhi, elimu, tajriba, umri na tamaduni zinachangia sana jinsi mhubiri anavyoitumia lugha yake kama itakavyodhihirika katika mifano hapo baadaye. Waliotafitiwi walikuwa na vyeo mbalimbali kama vile askofu, kiongozi wa dekania ambaye pia ni paroko , paroko na padri wa kawaida asiye na cheo katika parokia husika. Baadhi yao pia ni wasomi wa viwango vya juu na hata wana shahada za uzamifu. Utofauti wao ulijitokeza katika namna walivyoitumia lugha na katika ubadilishaji wao wa msimbo.

Kama ilivyo kawaida ya Kanisa Katoliki, kila Jumapili huwa na lengo mahsusi la kile kinachohubiriwa kwani kuna utaratibu unaofanana katika uendeshaji ibada ulimwenguni mote. Utaratibu huu ndio uliomsukuma mtafiti kutaka kuona utofauti uliopo katika makasisi walioteuliwa pamoja na askofu mmoja. Kama ilivyodhihirika ni kuwa kila mhubiri anapoanza ana utangulizi. Kasisi wa Consolata Westlands anasema kuwa,

Mfano [50]

Ndugu wapenzi hamjamboni tena? *‘God is good?’*

(Ndugu wapenzi hamjamboni tena? Mungu yu mwema?)

Mhubiri huyu anatanguliza ibada kwa kubadilisha msimbo wakati wa kuwasalimia wakristo na kuwakaribisha kanisani. Mwongozo uliopo katika kuendesha ibada ndio unaopelekea jambo hili kutumia mpangilio sawa wa ibada. Utafiti huu umedhihirisha hili katika makanisa matatu yaliyotafitiwa isipokuwa waliotafitiwa ni wanne (makasisi watatu na askofu mmoja). Hata hivyo, licha ya kuwa na utaratibu huu, ilidhihirika wazi kuwa kila mhubiri ana utofauti wake wa jinsi anavyoitumia lugha (Brown na wenzake, 1963: 158). Mtafiti hata alijitahidi kurekodi Jumapili moja mahubiri matatu katika makanisa mbalimbali na kwa makasisi watatu na askofu mmoja wenye vyeo mbalimbali. Hili liliwezekana kwa vile makanisa haya yana ibada nyingi. Holy Family Basilica huwa na ibada tano siku ya Jumapili, Consolata- Westlands misa sita ilhali Holy Spirit Gilgil ibada tatu. Misa hizi huendelea siku nzima na katika makanisa mengine hadi saa kumi na mbili jioni. Hili lilimfaa sana mtafiti kuweza kujumuika ibada moja hadi nyingine.

Ilidhihirika kuwa hadhi, kiwango cha elimu, tajriba, tabaka, uhusiano kati ya kasisi na waumini wake na umri wa wahubiri vimechangia sana jinsi uwasilishaji unavyofanywa. Makasisi waliotafitiwa pamoja na askofu walikuwa na umri, viwango vya juu vya elimu na tajriba mbalimbali maishani. Jambo hili lilichangia kuboresha uwasilishaji wa mahubiri yao hivyo kuvutia zaidi kwa wasikilizaji wao. Walionekana kujiamini, wenye maandalizi mema, kufurahia walichokifanya ila walijipata wamebadilisha msimbo kulingana na mada na msukumo wa kukuza uhusiano na ushirikiano miongoni mwao na waumini wao kama kanuni ya Grice ya ushirikiano inavyotaka hata bila wao kugundua.

Bourhis (1979, 1985) akinukuliwa na Akinyi na Kwach (2012) anasema kuwa umri ni kipengele muhimu cha ubadilishaji msimbo miongoni mwa wazungumzaji kama ilivyo hadhi yake. Sifa za mtu kando na mpangilio uliopo, lengo la mazungumzo na mada ya mazungumzo ndicho Bourhis anaita sifa za kidesturi (Normative Factors) ambazo huathiri namna mtu anavyoitumia lugha, na kwa njia hii umri na cheo ni vipengele muhimu vinavyodhihirika jinsi mtu hubadilisha msimbo. Katika makanisa yaliyotafitiwa vipengele hivi vilichangia jinsi wahubiri walivyobadilisha msimbo.

Katika Jimbo la Nakuru parokia ya Holy Spirit- Gilgil, ibada moja iliyorekodiwa ilikuwa ya askofu. Cheo chake na hadhi aliyonayo katika kanisa ilidhihirika wazi wazi namna alivyoitumia lugha. Kiwango chake cha ubadilishaji msimbo kilitofautiana kwa kiasi kikubwa na cha Paroko wa kanisa hilo ambaye umri wake ni miaka arobaini na mitatu ambao ni mdogo kuliko wa askofu mwenye miaka arobaini na mitano pamoja na utofauti wa vyeo vyao katika kanisa ambavyo vilichangia namna ubadilishaji msimbo ulivyojitokeza. Hata hivyo, wote wawili wana viwango

sawa vya elimu (uzamifu). Kasisi huyu pia ana ulumbi wa lugha kama ilivyodhihirika katika mahubiri yake (Poplack, 1980). (Tazama, mahubiri ya pili kwenye viambatisho). Lugha anazozitungumza zilichangia sana katika uwasilishaji wa maana kama asemavyo Mackey katika Suwito (1985:65) kuwa mzungumzaji ambaye ana uwezo wa kutumia lugha nyingi atakuwa na nafasi kubwa katika ubadilishaji msimbo kwa vile anavyozungumza huongozwa na uhiari wake wa kuchagua lugha atakayoitumia.

Kiwango cha umri wa miaka arobaini na mitatu wa kasisi wa Gilgil, ukilinganishwa na wa askofu wa miaka arobaini na mitano kilidhihirisha utumiaji mwingi wa ubadilishaji msimbo. Alibadilisha msimbo kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na jinsi askofu alivyobadilisha. Askofu alionekana kuuzingatia urasmi uliopo katika kanisa hili sawia na cheo chake cha uaskofu na hadhi aliyonayo kama mchungaji wa jimbo hili. Canon (772) inasema kuwa katika shughuli ya mahubiri, kila mtu anatakiwa kuzingatia sheria zilizowekwa na askofu wa jimbo husika. Hii ni kaida ya namna inayachunguza namna au mtindo wa kusema kitu (Habwe, 1999). Kuwa kitu lazima kisemwe kwa njia iliyo wazi ili hadhira ifuate na kufurahia ujumbe. Mahubiri ya askofu yalikuwa na mwegemeo mkubwa wa kiteolojia ikilinganishwa na ya makasisi na hili lilichangia namna alivyobadilisha msimbo. Kama itakavyodhihirika katika mifano baadaye, alipobadilisha msimbo msukumo wake mkuu ulikuwa kwa vile hakuwa na kisawe pamoja na hali ya kutaka kuudumisha uhusiano na kukuza ushirikiano.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa askofu alitakiwa kuwa kielelezo kwa makasisi wake. Askofu alikaa kubadilisha msimbo kiwango cha chini kama cha asilimia 10% kinyume na

Paroko wa kanisa lilo hilo ambaye asilimia yake ni 50%. Hivyo askofu alidhihirisha kuwa na urasmi mwingi akilinganishwa na makasisi waliotafitiwa.

Katika kanisa la Holy Family Basilica kasisi ambaye ndiye Paroko alibadilisha msimbo kama kiwango cha asilimia 40%. Kasisi huyu ana tajriba ya juu, kiwango cha juu cha elimu (mwanafunzi wa uzamifu) na hadhi ya Paroko wa kanisa hili. Alionekana kufurahia sana anachokifanya na kuwa na uhusiano mwema sana na waumini wake. Katika Parokia ya Consolata- Westlands, kasisi alitumia pia kiwango cha chini cha ubadilishaji msimbo kiwango sawa na askofu cha asilimia 10%. Hili lilichangiwa na asili yake na lugha anazoitumia. Mackey katika Suwito (1985:65) anaeleza kuwa sifa mahsusi za mzungumzaji ni pamoja na maisha ya awali katika jamii, kiwango cha elimu na maeneo alikotoka. Kasisi aliyetafitiwa ambaye ni mwenye asili ya Kiganda alionekana kuathiriwa na alikotoka katika jinsi alivyoitumia lugha hii ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kiwango cha ubadilishaji msimbo jambo ambalo lilipelekea yeye kubadilisha msimbo kwa kiasi kidogo sana ikilinganishwa na wenzake ambao ni Wakenya. Vile vile lugha yake ya Kiswahili ilidhihirisha pia asilia yake alivyoitumia. Alionekana aliyeng'ang'ana sana kuitumia lugha ya Kiswahili na hili lilichangia namna alivyobadilisha msimbo kwa hofu ya kwenda nje ya mada ya siku. Kanisa hili lina watu wa makabila mbalimbali, matabaka mbalimbali, vyeo mbalimbali ikiwa ni pamoja na watu wa mataifa na mabara mbalimbali.

Sehemu hii ya Westlands ina watu wengi hususan watawa na makasisi wengi ambao ni wa mataifa na mabara mbalimbali. Hii ni kwa vile sehemu hii ina makazi mengi ya makasisi na watawa wanaolitumikia Kanisa Katoliki katika Jimbo la Nairobi katika huduma mbalimbali. Pia

kuna wanafunzi wengi wanaosoma vyuo vikuu na seminari kutoka mataifa na mabara mbalimbali ikiwa pia ni pamoja na wafanyakazi wa makabila, mataifa na mabara mbalimbali. Hadhi ya lugha katika kanisa hili pia inadhihirika ambapo katika ibada zake sita ni misa moja tu ya Kiswahili nyingine zote zikiwa ni Kiingereza. Hivyo lugha ya Kiingereza inatawala ya Kiswahili (Magesa,1993). Kanisa hili linakuwa na takribani waumini 1000 katika kila ibada ishara kuwa sehemu hii ina watu wengi. Katika matumizi haya ya ubadilishaji msimbo mhubiri alidumisha kanuni za ushirikiano za Grice ikiwa ni pamoja na uhusiano, namna na idadi kwa kuyasema yanayofaa kusemwa na kudokeza namna washiriki katika mazungumzo wanazungumza kwa kuegemea kanuni hizi kwa njia inayofaa.

Yule (1996: 40) akinukuliwa na Kariithi (2010) anasema kuwa dhana ya kimsingi katika maongezi ni kuwa washiriki lazima wazingatie kanuni za kushirikiana na mikakati iliyopo. Lililo muhimu kujua ni kuwa ni mzungumzaji ambaye huwasiliana kupitia uhusishaji, na ni msikilizaji anayeng'amua maana kutokana na yale yaliyowasilishwa. Uchaguzi wa yale yaliyosemwa huegemea yale ambayo yana uwezo wa kudumisha malengo ya kushirikiana. Kanuni za ushirikiano za Grice (1975) hudokeza namna mtu huweza kuusimbua ujumbe kulingana na wengine wanavyosema, ili mtu aweze kusimbua habari ya mzungumzaji vizuri.

Kanuni hizi hudokeza namna washiriki katika mazungumzo wanaweza kwa kuegemea kanuni kisawasawa, kirazini na kwa njia ya kushirikiana, wazungumze kwa kuegemea ukweli, kwa kuegemea uhusiano wa kile kinasemwa na kwa njia ya wazi ili kuitoa habari toshelevu. Katika mazungumzo yao, wahubiri waliotafitiwa ilionyesha kuwa waliongozwa na kanuni hizi ila hawakuzitambua. Ubadilishaji msimbo walioutumia makasisi kwa kiasi kikubwa ulidhihirisha

ukiukaji wa kanuni hizi za ushirikiano; ikitokea hili halizingatiwi basi kanuni hizi huenda zikawa zimekiukwa hivyo basi yaliyokuwa yakitarajiwa katika mawasiliano yakatokea kutoafikiwa. Hofman (1993: 287) anasema kuwa kukiukwa kwa kanuni za maongezi hudhihirisha kuwa wazungumzaji wanalifanya jambo lingine na sio tu kutoa ripoti kuhusu ukweli: wanayosema huenda yakaangaziwa kupitia ufasili mzuri wa sheria. Kimsingi maswala kama haya yataashiria kuzingatiwa kwa kanuni za ushirikiano ikiwa ujumbe unaolengewa msikilizaji utafasilika. Kwa mfano, katika mahubiri ya kanisa la Holy Spirit -Gilgil; askofu anatanguliza kwa swali la balagha,

Mfano [51]

'Hi!' Hamjui Ndingi aliondoka?

(Hi! You do not know Bishop Ndingi left?)

Swali hili linadhihirisha kuwa askofu alivunja kanuni ya namna inayomtaka msemaji kutoa ujumbe ulio bayana na wazi bila kuficha lolote. Katika swali hili msikilizaji inafaa aanze kujiuliza analomaanisha. Msikilizaji basi ataanza kufikiria analomaanisha askofu na kuzua maana yeye mwenyewe. Kutokana na swali hili, ni kwamba askofu anamrejelea Askofu Ndingi aliyeliongoza jimbo hili ila huenda waumini wake wasielewe hivyo na kuzua maana nyingine. Kuna uwezekano pia kuwa hata baadhi ya waumini hawa hawamjui Askofu Ndingi kwa vile alistaafu kitambo. Vile vile waumini wengine wanaweza kuwa hawajakaa sehemu hii kwa muda kwa vile wengi wa wakazi wa sehemu hii ni wafanyakazi na wana biashara ambao huja na kuondoka. Kwa mujibu wa Grice, anachomaanisha msemaji katika usemi huweza kugawanywa katika kile msemaji anasema na kile msemaji anamaanisha. Wakati mwingine watu husema kile ambacho hawamaanishi na hii ndiyo

Grice anaita kujaribu kusema na kusema kimchezo ambalo huzua utata kwa sababu ya uhusiano uliopo baina ya kile msemaji anakisema na maana ya usemi wake anaousema.

3.3 UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA NENO

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa makasisi na askofu waliotafitiwa walibadilisha msimbo katika kiwango cha neno. Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno ulidhihirika katika makanisa zaidi ya moja yaliyotafitiwa. Ubadilishaji msimbo unaweza kuwa mfupi au mwepesi kama neno moja kutoka lugha nyingine uliotumiwa katika matamshi, au unaweza kujitokeza kama vipengele vikubwa vya diskosi na uwe mtindo imara au mazoea kama vile matumizi ya mara kwa mara ya Kilatini katika Kanisa Katoliki na hivyo kudhihirisha sababu za utumiaji wa ubadilishaji msimbo (Hancock, 1997) akinukuliwa na Bazerman (2008). Fasold (1997) katika Bazerman (2008) anakubaliana na hayo kwa kusema kuwa utumiaji wa neno au kirai kutoka lugha nyingine hudhihirika kama ubadilishaji msimbo. Anatoa mfano wa ubadilishaji msimbo kati ya Kiingereza na lugha ya Kishona.

Mfano [52]

Chasara kupera *'fuel'* iri mumhepo. Zvakaoma zvatinoitirwa. (*The Herald online*, 17.09.11). Mfano alioutoa uko katika lugha ya Kishona lakini mzungumzaji ametumia neno moja tu la Kiingereza, *'fuel'* na hivyo ubadilishaji msimbo umetokea.

3.3.1 Ubadilishaji msimbo wa neno katika mahubiri

Katika mahubiri tuliyoyarekodi hali hii ilijitokeza pia. Kasisi katika kanisa la Holy Family Basilica anauliza waumini wake swali la balagha,

Mfano [53]

Sasa ‘*imagine*’ na angekuwa amekufa?

(Sasa fikiria, na angekuwa amekufa?)

Anatumia lugha ya Kiswahili na papo hapo anabadilisha msimbo na kutumia neno la Kiingereza, ‘*imagine*’. Matumizi haya ya ‘*imagine*’ yanatoa hisi alizonazo mzungumzaji pamoja na kuujenga na kuudumisha ushirikiano kati yake na msikilizaji. Hivyo anatumia kaida ya ushirikiano kama inavyodokezwa na Grice. Uhusiano pia kati yao unadumishwa. Swali hili lilidhamiriwa pia kuteka nathari ya hadhira yake na kuwafanya wamsikilize. Mifano zaidi,

Mfano [54]

Basi wakristo karibuni katika tafakari ya leo tukisherekea sikukuu ya ‘*Pentecost*’.

(Basi wakristo karibuni katika tafakari ya leo tukisherekea sikukuu ya Pentekoste).

Neno lili hili ‘*Pentecost*’ lilitumika na kasisi wa kanisa la Consolata - Westlands anayesema,

Mfano [55]

Kwa hivyo ‘*Pentecost*’, ilikuwa sherehe ya kukumbuka kupokea sheria, amri ya Mungu.

(Kwa hivyo Pentekoste, ilikuwa sherehe ya kukumbuka kupokea sheria, amri ya Mungu.)

Askofu pia amelitumia katika kanisa la Holy Spirit- Gilgil anaposema kuwa,

Mfano [56]

Leo tunasherekea sikukuu ya ‘*Pentecost*’ vile nilisema mwanzo wa misa.

(Leo tunasherekea sikukuu ya Pentekoste vile nilisema mwanzo wa misa).

Licha ya matumizi ya neno hili kudhihirisha ubadilishaji msimbo ulio sawa kwa wahubiri hawa, pia linadhahirisha usawa katika utaratibu ulioko katika Kanisa Katoliki wakati wa ibada ya misa. Kuwa kanisa hili ladhahirisha mpangilio au utaratibu wake wa misa ni sawa kote ulimwenguni. Tofauti ni lugha zinazotumika ijapokuwa pia kama tulivyotaja awali kuna lugha zilizopendekezwa kutumiwa wakati wa misa ikiwa ni pamoja na lugha asilia za mahali husika (Mroso, 1995). Ubadilishaji msimbo huu unadhahirisha kuwa wahubiri hawa hawakuwa na neno la Kiswahili na hivyo wakasukumwa na haja ya kuendeleza mazungumzo na kwa haraka wakatamia lugha ya Kiingereza walio na uelewa wake wa neno hili. Ametumia neno ‘*prolife*’ pia;

Mfano [57]

Hao ambao huwa wanazungumzia ‘*prolife*’, wanaitwa ‘*prolifers*’.

(Hao ambao huwa wanazungumzia utunzaji wa uhai, wanaitwa watunzaji wa uhai).

Ubadilishaji msimbo wa kasisi wa Holy Spirit – Gilgil unadhahirisha hili pia;

Mfano [58]

Huyu ni ‘*Mrs*’ Kariuki.

(Huyu ni Bi. Kariuki.)

Mfano [59]

Have you seen beautiful person, have you seen beautiful person? ‘*Nyinyi?*’ Are you beautiful?

(Ushaona mtu mrembo, umeshaona mtu mrembo? Nyinyi? Nyinyi ni warembo?)

Uhusishaji katika mfano huu ni kuwa, kasisi huyu anatoa dhana ya urembo katika mahubiri yake. Anauelewa uzuri wa mwenyezi Mungu na kuuhusisha na maisha ya kila siku. Anataka waumini wake kuona uzuri huo. Hivyo, kama Mungu ni mzuri basi hata sisi viumbe wake ni wazuri na kila mmoja anafaa kuufurahia uzuri huo wa Mungu na kushukuru kwa uzuri huo. Uelewa wa awali unahitajika hapa kati ya mhubiri na wafuasi wake.

Mifano zaidi ya kasisi wa Holy Spirit- Gilgil,

Mfano [60]

Ulikuwa kwa ‘*ministry?*’

(Ulikuwa kwa utume?)

Mfano [61]

Tuimarishwe na ‘*Eucharist*’ hiyo ili tukae ndani ya Kristu na kuwa na uzima wa milele.

(Tuimarishwe na ekaristia hiyo ili tukae ndani ya Kristu na kuwa na uzima wa milele).

Mfano [62]

Nakumbuka siku moja mwalimu aliyetufunza ‘*seminary*’.

(Nakumbuka siku moja mwalimu aliyetufunza seminari).

Kama tulivyotaja awali, kasisi huyu ndiye aliyetumia ubadilishaji msimbo wa hali ya juu zaidi. Utofauti wake na wa askofu ambaye walifanya misa katika kanisa moja ijapokuwa katika Jumapili tofauti unadhihirika. Hili linachangiwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na uhusiano alionao kasisi huyu na waumini wake, yeye ndiye Paroko wa kanisa hili na uhusiano wake na

hadhira yake unadhihirika kuwa wa karibu sana na hata anawaita wengi kwa majina yao anapohubiri (Huyu ni Mrs Kariuki, Evaline, Gladys na kadhalika). Kwa kiasi kikubwa ubadilishaji msimbo wake ulitoa msukumo wake mkuu wa kutumia ubadilishaji msimbo au lengo lake kama vile kutaka kuisitiza hoja, kukazia jambo fulani alilosema, kuteka nathari ya waumini wake kwa kuwafanya wawe makini na hivyo kuboresha uhusiano wake na wakristo wake (Massey, 1980). Licha ya kuwa alitumia mikakati hii hakuelewa, lakini alizingatia kaida za Grice za kiasi, namna, uhusiano na ukweli na hivyo kuboresha uwasilishaji wake na ushirikiano na waumini wake katika ibada hii.

Uhusishaji uliopo hapa ni kuwa, katika mfano huu kasisi huyu anaoutumia wa kurejelea, kaida ya ukweli inaweza kukiukwa na waumini wasimwone mhubiri kama mwongo. Hii ni kwa sababu chochote kinachosemwa na hadithi iliyo kando na msikilizaji, ni funzo lenye uhusiano. Kaida ya ukweli basi inatawala ile ya namna. Dhana hii inaathiriwa na kanuni za Grice . Katika mfano [40], kasisi anaanza kwa kurejelea mwalimu wake katika seminari aliyewaambia hajaona kitu kirembo kama mwanadamu. Katika maelezo yake mhubiri anaelezea kile yeye mwenyewe anataka waumini wake waelewe lakini anamwacha mwenye kumsikiliza kuiwazia maana anayoipata. Kaida za idadi na namna zinatoa habari kamili na kuepukana na utata. Kasisi huyu anaona hadhira yake ikiwa na uwezo wa kutafuta maana wenyewe na kuwa kuelezea kila kitu huenda ikachukua muda mwingi na kuvunja kaida ya idadi na kuishia hata kuchosha wasikilizaji wake.

Kasisi wa Holy Family Basilica pia anasema,

Mfano [63]

Kuna sherehe tatu za umuhimu sana; kwanza kuzaliwa kwake Kristo ‘*incarnation*’, pili kufufuka ‘*resurrection*’ na tatu ‘*pentecost*’.

(Kuna sherehe tatu za umuhimu sana; kwanza kuzaliwa kwake Kristo, kuzaliwa kwake Kristo, pili kufufuka, kufufuka na tatu pentekoste).

Mfano [64]

Nilienda nikamwekea ‘*socket*’ zote kwa kuwa niliona haelewi.

(Nilienda nikamwekea soketi zote kwa kuwa niliona haelewi).

Mfano [65]

Godoro yake ilishika moto akaniambia ‘*father*’ si ni nyinyi hamkununua ‘*socket*’.

(Godoro yake ilishika moto akaniambia padri si ni nyinyi hamkununua soketi).

Mfano [66]

‘*Anyway*’ tuombe sana ndugu zangu, tuombe sana ndugu zangu.

(Haidhuru, tuombe sana ndugu zangu, tuombe sana ndugu zangu).

Kasisi huyu licha ya kwamba alikuwa hana visawe vya maneno haya, ameyatumia pia kuepukana na kutoa maelezo mengi ili kutumia muda au maneno machache kuelezea aliyokusudia kusema. Hata hivyo anatimiza kaida ya ushirikiano ya namna kwani anasema kwa njia inayoeleweka vile vile kaida ya uhusiano kwani anasema wakati ufaao. Kasisi huyu pia ana msukumo wa hadhi aliyo nayo katika kanisa hili. Yeye ndiye Paroko kumaanisha kwamba

anafahamiana vema na waumini wake hivyo anapobadilisha msimbo linakuwa ni jambo la hiari la kuudumisha uhusiano wake. Kiwango chake cha elimu pamoja na tajriba yake pia kinachangia uwasilishaji wa ujumbe. Yeye ni mwanafunzi wa uzamifu. Kasisi katika kanisa la Consolata ambapo kasisi anayehubiri ni padri wa kawaida na ambaye asili yake sio Mkenya, anawaambia waumini wake kuwa;

Mfano [67]

Mungu Baba kwa njia ya kipekee ni muumba wetu, '*creator*'.

(Mungu Baba kwa njia ya kipekee ni muumba wetu, muumba).

Anatumia lugha ya Kiswahili na papo papo anabadilisha msimbo hadi Kiingereza. Lengo lake ni kutilia mkazo kazi ya Mungu ya kuumba. Aidha anatumia kanuni mojawapo katika mahubiri ya Kanisa Katoliki ya kulenga mada ya siku kama mpangilio katika kanisa hili unavyopendekeza. Ulingaji huu unatumia bila kuelewa kuwa wanazitimiza kaida za Umaanisho ikiwa ni pamoja na uhusiano, namna, idadi na ukweli. Vile vile wanaudumisha uhusiano uliopo kati yao na wasikilizaji wao. Habwe (1999) anasema kuwa wahubiri hujitwalia kiasi kikubwa cha habari ambazo wao na hadhira hushirikiana. Hili hupelekea mitazamo mbalimbali ya kujieleza. Wazungumzaji humaanisha zaidi ya kinachoeleweka katika hali ya kawaida kisemantiki (Leech, 1983). Kwa mfano katika mahubiri yaliyotolewa na askofu alitanguliza kwa swali la balagha, (rejelea mfano wa 51)

Naye kasisi wa Holy Family Basilica anasema;

Mfano [68]

Kuna roho mbaya katika ‘*minds*’ zetu.

(Kuna roho mbaya katika akili zetu).

Hadhira basi inabidi kutumia habari za awali kutafuta kinachomaanishwa. Hili linadhihirisha kutawaliwa na kaida ya ushirikiano ya Grice yenye kanuni nne kama tulivyokwisha kuzitaja awali. Katika sentensi hizi ni wazi kuwa kasisi na waumini wake wanaelewa vema Ndingi ni nani aidha uelewa wa kuwa zipo roho mbalimbali.

Askofu pia alibadilisha msimbo kwa kusema kuwa,

Mfano [69]

Katika Kanisa Katoliki kuna kikundi kinaitwa ‘*prolife*’ wale watu wanaotunza uhai.

(Katika Kanisa Katoliki, kuna kikundi kinaitwa watunzaji uhai, wale watu wanaotunza uhai).

Askofu anajaribu kutoa maelezo ya ‘*prolife*’ baada ya kutaja. Hii ni kwa vile katika utamkaji wa neno hili, hakuwa na kisawe chake kwa vile ubadilishaji mwingine huwa si wa kimaksudi au unaolenga wasikilizaji bali huweza kutokea kwa vile mzungumzaji hana mbinu nyingine yoyote ya kuwasiliana. Mawazo pia ya Poplack (1980) yanaoana na haya kuwa mara nyingi watu huingiza neno moja kutoka lugha nyingine kwa sababu wamesahau au hawalijui lile neno katika lugha ya msingi.

Hivyo askofu alisukumwa na hali ya kutaka hadhira yake kuelewa anachokisema. Ijapokuwa ana urasmi mwingi lakini alisukumwa na hali ya kudumisha kaida ya ushirikiano hata bila yeye kuelewa.

Ametumia pia,

Mfano [70]

'new nation' katika sentensi;

Siku ya Pentekoste kunaundwa taifa jipya, *'new nation'*, taifa la Roho Mtakatifu, taifa la uzima wa milele.

(Siku ya Pentekoste kunaundwa taifa jipya, taifa jipya, taifa la Roho Mtakatifu, taifa la uzima wa milele).

Askofu anarudiarudia taifa jipya na ndio sababu hata akaingiza Kiingereza kwa nia ya kusesitiza anachokisema. Lengo lake pia ni kumleta msikilizaji wake karibu naye na bila kuelewa kaida za Grice za namna, uhusiano, ukweli na kiasi zinatimizwa na kukuza ushirikiano wa hali ya juu miongoni mwake na hadhira yake. Kaida za Grice ni kanuni ambazo hufanya mazungumzo kufaulu. Grice alitaka mazungumzo yawe wazi na kamilifu na hivyo yakuze utangamano na ueleweno kati ya washiriki. Chapman (1994:253) anaeleza kuwa kwa njia ya matendo, maneno na ishara zinazounda muundo wa ibada, roho huweka waumini na wahubiri katika uhusiano unaodumu na Kristo, neno na sura ya Baba ili waweze kuishi maana kamilifu ya kile wanakisikia, kutafakari na kufanya katika ibada.

Mifano zaidi,

Kasisi wa Consolata Westlands anasema,

Mfano [71]

Leo basi tumesikia kutoka somo la kwanza iliyotoka katika kitabu cha matendo ya mitume ati kuna ishara ya Roho Mtakatifu. Ya kwanza ni nguvu ya upepo '*wind*', ya pili ni ndimi za moto, '*tongues of fire*', tatu ni njiwa '*dove*' na ya nne ni maji '*water*'.

Hili limechangiwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na asilia yake ambayo inachangia pakubwa uzungumzaji wake wa lugha ya Kiswahili. Vile vile umechangiwa na eneo ambalo kanisa hili lipo. Kanisa hili lina misa sita kwa siku ya Jumapili na ni moja tu ambayo ni ya Kiswahili. Hili ladhihirisha hadhi ya lugha ya Kiswahili katika eneo hili. Aidha eneo limetawaliwa na watu wa matabaka mbalimbali, kazi mbalimbali, makabila mbalimbali, mataifa mbalimbali, mabara mbalimbali na asili mbalimbali miongoni mwa mengine. Pia mapadri wanaofanya kazi katika parokia hii wana mchanganyiko kwa vile ni wa shirika la kimisionari la Consolata, hivyo ni mapadri kutoka mataifa mbalimbali. Kasisi huyu ana mwelekeo wa kudumisha urasmi pia kama alivyofanya askofu. Licha ya kuwa ni padre wa kawaida anapolitembelea kanisa hili (sio paroko), yeye ana cheo katika kanisa kwani ni msimamzi mkuu (Regional Superior) katika nyumba ya makao makuu ya kimaeneo huko Westlands, hivyo basi ni kielelezo cha matumizi ya urasmi katika misa. Hoja hizi basi zimechangia kiwango cha chini cha ubadilishaji msimbo ikilinganishwa na kanisa la Holy Family Basilica lililo ndani ya mji mkuu wa Kenya.

Kama kanuni za Grice za ushirikiano zinavyopendekeza kuwa kuwe na uhusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji, uhusiano kati ya kasisi huyu na waumini wake na uelewa wa awali ni tofauti katika kanisa la Consolata- Westlands kwani kasisi huyu kinyume na yule wa Gilgil na Basilica, hajakuwa na waumini hawa kwa muda mrefu kwani yeye hutembelea kanisa hili mara

chache sawia na askofu ambaye pia alikuwa ametembelea kanisa la Holy Spirit- Gilgil siku hii ya Jumapili. Tunaweza kujiuliza swali la uhusishaji wa kipragmatiki kuwa, kwa nini askofu na kasisi huyu wa Westlands- Consolata wametumia wingi wa ubadilishaji msimbo katika kiwango cha neno ikilinganishwa na makasisi wale wengine wawili? Wote wawili wana sifa za kutaka kudumisha urasmi wao katika mahubiri yao. Vile vile kutokana na uelewa wao wa lugha ya Kiswahili, wanabadilisha msimbo kwa vile hawana kisawe chake. Hadhi zao na kazi wanazozifanya ni za hali ya juu, wote ni viongozi katika maeneo mbalimbali. Hivyo basi wanasukumwa na hali ya kudumisha hadhi hii na uhusiano wao na wafuasi wao. Wanajua vizuri maeneo waliyomo na kiwango cha uelewa cha wale wanaowasikiliza.

3.3.2 Ubadilishaji msimbo katika kirai

Huu ni ubadilishaji msimbo unaotokea katika kiwango cha kirai. Kwa mfano,

Mfano [72]

How pathetic of the police to leave the car running!!! *'Kana fuza chairo' will drive off (The Herald online, 17.09.11).*

Mfano huu uko katika Kiingereza lakini mzungumzaji ametumia kirai cha Kishona na hivyo kudhihirisha ubadilishaji msimbo. Ubadilishaji msimbo huu pia ulijitokeza kwa wingi katika utafiti huu. Kasisi wa kanisa la Holy Spirit- Gilgil anasema;

Mfano [73]

Kwa Kilatini tunasema *'Corpus Christi'*.

(Kwa Kilatini tunasema Mwili na Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo).

Mfano [74]

Kwa Kiitaliano ni *'il Santissimo Corpo e Sangue di Cristo'*.

(Kwa Kiitaliano tunasema Mwili na Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo).

Mfano [75]

Baba Mtakatifu , Yohane Paulo 2 ameandika kitabu kiitwacho; *'Theology of the body'*.

(Baba Mtakatifu , Yohane Paulo 2 ameandika kitabu kiitwacho; 'Teolojia ya mwili').

Kasisi huyu ametumia virai hivi kwa kuwa hakuwa na visawe vya maneno aliyoyatumia isipokuwa baadaye anajaribu kuelezea maana yake. Katika mfano wa [73] na [74], kasisi huyu amebadilisha msimbo kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kilatini na pia Kiitaliano. Mfano huu unadhihirisha umuhimu wa lugha hii ya Kilatini inayochukuliwa kama lugha rasmi ya Kanisa Katoliki. Uhusishaji hapa au swali ambalo tunaweza kujiuliza ni kwa nini kasisi huyu anatumia lugha ya Kilatini. Kasisi huyu ni msomi wa kiwango cha juu aliye na ulumbi wa lugha. Aidha amefanya hata kazi ng'ambo Uingereza na Italia. Pia shahada zake zote amezipata kutoka vyuo vikuu vya Italia. Msukumo huu unaweza kuchangia matumizi yake ya lugha. Pamoja na msukumo huu ni kuwa anataka kutilia msisitizo anachokisema ikiwa ni pamoja na kudhihirisha cheo chake cha kiusomi, hadhi yake ya paroko pamoja na uhusiano wake na wafuasi wake.

Kasisi wa Consolata anasema;

Mfano [76]

Ndugu wapenzi hamjamboni tena? *'God is good?'*

(Ndugu wapenzi hamjamboni tena? Mungu yu mwema?)

Mfano [77]

Na kwa sababu hiyo wewe na mimi kama wakristo wakatoliki, tunaamini Mungu mmoja katika Utatu Mtakatifu. *'Holy Trinity'*.

(Na kwa sababu hiyo wewe na mimi kama wakristo wakatoliki, tunaamini Mungu mmoja katika Utatu Mtakatifu. Utatu Mtakatifu).

Naye kasisi wa Holy Family Basilica ametumia ubadilishaji huu kwa wingi;

Mfano [78]

Kwa nini mwanadamu anatoa matamshi ambayo yanatenganisha watu? *'Why eh why?'* Kwa nini?

(Kwa nini mwanadamu anatoa matamshi ambayo yanatenganisha watu? Kwa nini eh kwa nini ? Kwa nini?)

Mfano [79]

Si unaona *'little knowledge'* si angechomeka hapo ndani kwa sababu tunajifanya wajuaji sana katika maisha...

(Si unaona ujuzi kidogo, si angechomeka hapo ndani kwa sababu tunajifanya wajuaji sana katika maisha...)

Inavyodhihirika ni kuwa makasisi katika Kanisa Katoliki wanatumia aina hii ya ubadilishaji msimbo. Hili liko wazi katika makanisa yaliyotafitiwa. Jambo linalojitokeza ni kuwa makasisi hawa wanapobadilisha msimbo katika kirai wanaishia kusisitiza hivyo kutoa dhana ya takriri. Hali hii inaleta ukiukaji wa kanuni ya idadi inayosema kuwa msemaji anapaswa kusema

yanayotosheleza na yasizidi kiasi wala kupunguza taarifa ili kuweza kuwasiliana. Aseme habari kamilifu. Katika hali ya kusisitiza makasisi hawa wanaweza kusema zaidi ya yanayotakikana. Hata hivyo ukiushi huu unachangia jinsi ujumbe unavyomfikia msikilizaji na katika hali ya msisitizo msikilizaji inafaa aliwazie jambo ambalo kasisi anasema.

3.4 HITIMISHO

Katika sehemu hii, tumeanza kwa kuelezea kuhusu ubadilishaji msimbo na baadaye kuangalia jinsi umetumiwa na wahubiri tuliowatafiti. Tumeangalia jinsi walivyoutumia katika kiwango cha neno na kirai. Utafiti umedhihirisha kuwa wahubiri hutumia ubadilishaji msimbo ili kuhakikisha kuwa uhusiano unadumishwa kati yao na waumini. Uhusiano huu ni mojawapo ya kaida za nadharia ya Umaanisho ya Grice inayomtaka mzungumzaji adumishe uhusiano uliopo kati yake na msikilizaji. Ubadilishaji msimbo huu ulihusiana na mada husika katika matumizi ya lugha.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA KIWANGO CHA SENTENSI

4.0 UTANGULIZI

Sehemu hii tutachanganua ubadilishaji msimbo kama ulivyojitokeza katika utafiti huu. Tutaangalia katika kiwango cha sentensi. Baadaye tutatoa maelezo kidogo kuhusu uhusishaji na hatimaye kuelezea uhusishaji na ubadilishaji msimbo.

Ubadilishaji msimbo katika kiwango cha sentensi ndio uliojitokeza kwa kiwango cha juu sana hasa katika Parokia za Holy Family Basilica na Holy Spirit –Gilgil. Ubadilishaji msimbo huu unaweza kutokea kati ya sentensi au ukatokea miongoni mwa sentensi. Makasisi hawa waliotafitiwa hasa waliotajwa (Holy Spirit - Gilgil na Holy Family Basilica), walikuwa na ubadilishaji msimbo mwingi katika sentensi ikilinganishwa na askofu na kasisi wa Westlands ambao wao ulikuwa mchache na katika kiwango cha neno. Harmer na Blanc (1989:35) katika Malmkjaer (1991:62) akinukuliwa na Mwandije (2004) anasema kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea katika sentensi, kishazi, kirai na maneno. Ubadilishaji huu huongozwa na kaida za wana uwililugha katika jamii tofauti tofauti.

4.1 UBADILISHAJI MSIMBO KATI YA SENTENSI

Aina hii ya ubadilishaji msimbo ilijitokeza kwa wingi sana katika utafiti huu.

Katika kanisa la Holy Spirit- Gilgil kasisi ambaye ndiye Paroko wa kanisa hili anasema,

Mfano [80]

Leo tunasherekea sikukuu ya Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwa lugha ya Kilatini tunaongea kuhusu *‘Corpus Christi’* na tena *‘body and blood of Christ’* lugha ya Kiingereza na kwa Kiitaliano *‘Corpodi Cristo’*.

Kasisi huyu amechanganya lugha zaidi ya lugha moja katika sentensi hii. Maneno aliyoyatumia yameundwa kwa kutumia sheria za kimofolojia za lugha nyingine kama inavyodhihirika. Lengo lake lilikuwa ni kuelezea ujumbe wake kiasi kuwa utaeleweka vilivyo.

Kasisi huyu alitumia aina hii ya ubadilishaji msimbo kwa wingi kwa kuwa hakuwa na kisawe na vile vile kwa nia ya kusisitiza alichokisema. Kwa mfano,

Mfano [81]

Tulivyo navyo tunavileta kwenye ‘*altar*’ ya Mungu ili kusaidia kanisa katika kueneza injili ‘*that is evangelization through social action*’ ili tuweze kujenga ‘*maternity*’ katika zahanati yetu, ili tuendeleza mjengo wa shule yetu, kusaidia askofu katika mradi wa ‘*Catholic Diocese of Nakuru Family Plaza*’ na ili tuweze kununua gari la kazi ya kichungaji kwa Parokia.

(Tulivyo navyo tunavileta kwenye altare ya Mungu ili kusaidia kanisa katika uinjilisti, uenezaji injili kupitia masuala ya kijamii ili tuweze kujenga chumba chetu cha kujifungulia cha akina mama, ili tuweze kununua gari la kazi ya kichungaji kwa Parokia, hiyo ndio tunaita maendeleo ya kijamii ama matendo ya kijamii katika uenezaji wa injili). Mifano mingine ni,

Mfano [82]

Na hata ukiingia katika ule mlango wetu wa kanisa, tena ukitazama pale kwenye shule yetu utaona ‘*logo*’ ya Jimbo la Nakuru ambayo imeandikwa ‘*ut unum sinti, ut unum sinti*’.

(Na hata ukiingia katika ule mlango wetu wa kanisa, tena ukitazama pale kwenye shule yetu utaona nembo ya Jimbo la Nakuru ambayo imeandikwa ili wote wawe kitu kimoja, ili wote wawe kitu kimoja).

Mfano [83]

'Finally I will speak about', nitaongea kuhusu Ekaristia Takatifu, yaani Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambayo ni sikukuu tunayoadhimisha siku ya leo.

(Mwisho nitaongea kuhusu, nitaongea kuhusu Ekaristia Takatifu, yaani Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambayo ni sikukuu tunayoadhimisha siku ya leo).

Mfano [84]

Kwa hivyo kuzaliwa kwa Bwana krisimasi huwa tunasherehekea *'the incarnation of the word of God'* ambapo katika sikukuu ile neno la Mungu alichukua mwili na akakaa kwetu .

(Kwa hivyo kuzaliwa kwa Bwana krisimasi huwa tunasherehekea kuzaliwa kwa neno la Mungu ambapo katika sikukuu ile neno la Mungu alichukua mwili na akakaa kwetu).

Mfano [85]

Baba Mtakatifu Yohana wa 2 ameandika kitabu *'The Theology of the body'*, na katika *'The Theology of the body'* anaeleza maana ya mwili wa mwanadamu, *'the beauty of human person, the beauty of human person in glorifying God, thus not indulging ourselves in immoralities'*.

(Baba Mtakatifu Yohana wa 2 ameandika kitabu *'Teolojia ya mwili'*, na katika *'Teolojia ya mwili'* anaeleza maana ya mwili wa mwanadamu, urembo wa mwanadamu, urembo wa

mwanadamu katika kumtukuza Mungu, hivyo kutojiingiza katika mambo ambayo hayampendezi Mungu).

Mfano [86]

Kuna msemu unaosema, *'cleanliness is second to Godliness'*.

(Kuna msemu unaosema, usafi ni jambo la pili linalofuata Uungu).

Uhusishaji hapa ni kuwa wale wote wanaomfuata Kristo inafaa wawe safi. Kuwa safi ni fadhila ya pili kutoka kwa ile ya kuupata Uungu. Hivyo, kasisi anawasihi wote wawe safi kama vile Mungu alivyo bila doa.

Mfano [87]

Sasa kwa nini wewe unajiachilia hata nikipita karibu nawe nashika pua kwa sababu *'you are all over sweating'*,

(Sasa kwa nini wewe unajiachilia hata nikipita karibu nawe nashika pua kwa sababu unatoa jasho kila mahali).

Mfano mwingine wa ubadilishaji msimbo kati ya sentensi ni,

Mfano [88]

Sisi sote tuko kitu kimoja lakini *'we are unique'* *'We are unique'*

(Sisi sote tuko kitu kimoja lakini tuko tofauti. Tuko tofauti).

Kasisi huyu alitumia kiwango kikubwa sana cha aina hii ya ubadilishaji msimbo. Aidha inavyodhihirika matumizi haya yake ya ubadilishaji msimbo yanadhihirisha matumizi ya takriri kwa nia ya kutaka kuisisitiza anachokisema. Ametumia pia kwa lengo la kunukuu au kurejelea.

Ubadilishaji msimbo huu pia umetumiwa na kasisi wa Holy Family Basilica anayesema;

Mfano [89]

Myahudi akajua kwamba, *'there is bad spirit in each one of us'*, kuna roho mbaya katika *'our minds'*.

(Myahudi akajua kwamba, kuna pepo mbaya, kuna roho mbaya katika akili zetu).

Mhubiri hapa anatoa dhana hasi kwa kuelezea Myahudi alivyoona roho mbaya. Anapotumia mtazamo huu hasi, anaachia hadhira kujitafutia wenyewe kilicho chanya. Hili linazingatia kaida ya namna na idadi kwa vile yeye anatoa habari toshelevu na hataki kutoa utata wowote. Anataka waumini wake wapate habari ambazo anaamini wana uwezo wa kuelewa anachokisema na kupata maana.

Mfano [90]

Tumesikia katika somo la pili Paulo akisema, akituambia kwamba karama ni nyingi *'but we are different'*.

(Tumesikia katika somo la pili Paulo akisema, akituambia kwamba karama ni nyingi lakini tuko tofauti).

Mfano [91]

Lakini lazima tuombe Roho Mtakatifu *'that we are able to appreciate one another'*.

(Lakini lazima tuombe Roho Mtakatifu kwamba tunaweza kupokeana jinsi tulivyo).

Mfano [92]

‘*You see*’ bila karama ya bibi yako utaaibika.

(Unaona, bila karama ya bibi yako utaaibika).

Mfano [93]

Wajua siku hizi watu wanajifanya wajuaji sana, lakini unajua ‘*that is why*’ wanasema ‘*little knowledge is dangerous*’.

(Wajua siku hizi watu wanajifanya wajuaji sana, lakini unajua, ndio sababu wanasema ujuzi kidogo ni mbaya).

Mfano [94]

Na watu wengine ‘*they take advantage*’ kwa sababu ya cheo chao.

(Na watu wengine wanachukulia mambo kwa sababu ya cheo chao).

Mfano [95]

Watu wengine ‘*they know it all*’, wanajua kila kitu.

(Watu wengine wanajua kila kitu, wanajua kila kitu).

Mifano [89-94] inadhihirisha ubadilishaji msimbo kati ya sentensi ambapo kila kishazi kimetumia lugha tofauti. Vishazi hivi vinaingiliana na kuunda sentensi kamilifu bila kuvunja sheria za uundaji wa sentensi.

Katika aina hii ya ubadilishaji msimbo, makasisi hawa wanachanganya Kiswahili na Kiingereza. Kuchanganya msimbo huku hakuvunji sheria za kisintaksia za lugha zote mbili. Poplack (1980:586) anaeleza kuwa kuna uwezekano wa kuchanganya lugha zote mbili ambapo kuingiliana kwa lugha zote mbili hakuvunji sheria za kisintaksia za lugha yoyote. Lugha zote ziliingiliana sawa katika sheria zake za kuunda sentensi. Kwa mfano katika mfano wa [84], sentensi zote mbili zimeingiliana vizuri katika sheria zake za uundaji wa sentensi. Kishazi cha Kiingereza na cha Kiswahili zimeingiliana vizuri na kuunda sentensi nzima.

4.2 UBADILISHAJI MSIMBO BAINA YA SENTENSI

Ubadilishaji msimbo huu pia ulitumiwa kwa wingi na makasisi wawili wa Holy Spirit Gilgil na Holy Family Basilica. Huu ni ubadilishaji msimbo ambao hujumuisha kubadilisha sentensi kwa namna ambayo kila kishazi au sentensi huwa katika lugha moja. Sentensi moja hugawanywa mara mbili na lugha zinazohusika. Kila sentensi huundwa kwa kuzingatia sheria za utunzi wa sentensi wa lugha husika.

Katika kanisa la Holy Spirit-Gilgil kasisi anasema,

Mfano [96]

Na basi siku hiyo kama kanisa tukaona rehema za Mungu zilitushukia kupitia kwa watu mia tatu arubaini na sita waliopewa sakramenti ya kipaimara. *'That's an indication and it's a sign of growing church'*.

(Na basi siku hiyo kama kanisa tukaona rehema za Mungu zilitushukia kupitia kwa watu mia tatu arubaini na sita waliopewa sakramenti ya kipaimara. Hiyo ni dalili na ishara ya kanisa linalokua).

Mfano [97]

Tumesikia ya kwamba Mungu alisema na sasa tuumbe mtu binadamu kwa sura na upendo wetu.

‘We are created in the image and likeness of God’.

(Tumesikia ya kwamba Mungu alisema na sasa tuumbe binadamu kwa sura na upendo wetu.

Tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu).

Mfano [98]

‘You are supposed to see God in that person.’ Unapomwona mtu unatakiwa kumwona Mungu ndani ya yule mtu.

(Unapaswa kumwona Mungu katika mtu huyo. Unapomwona mtu unatakiwa kumwona Mungu ndani ya yule mtu).

Mfano [99]

‘It is an imperative to ensure that you retain the dignity of your body, retain the beauty of your body, you ensure that your body is healthy’. Kwa sababu wengine wenu mnajiachilia vumbi, hauogi. Tumsafishe?

(Ni jambo muhimu kuhakikisha kuwa unadumisha heshima ya mwili wako, udumishe urembo wa mwili wako. Kwa sababu wengine wenu mnajiachilia vumbi, hauogi. Tumsafishe?)

Kasisi huyu alitumia ubadilishaji msimbo katika sentensi kwa kiwango cha juu sana ikilinganishwa na wenzake kama tulivyodokeza awali. Kutokana na ubadilishaji huu wake wa baina ya sentensi, sentensi zake zinatoa dhana ya uradidi. Anaonekana akirudiarudia anaposema jambo. Rayfields (1970:54) akinukuliwa na Ndungu (2001), katika lugha ya kuongea ya kisasa

kubadilisha msimbo kunakuwa dhana ya msisitizo kupitia kurudia katika lugha nyingine. Kasisi huyu ana msukumo wa kutaka ujumbe anaouwasilisha ueleweke ikiwa ni pamoja na kuwa anawaelewa waumini wake vema na hivyo kuna kile angetaka wanufaike nacho. Anauimarisha uhusiano wake na hadhira yake kwa kusisitiza.

Kitu kingine kimejitokeza ni kuwa nyingi ya sentensi alizozitumia zinatoa dhana ya urefu. Sentensi zake ni ndefu ziwe za baina ya sentensi au kati ya sentensi. Hili tutalikusisha na hali yake ya juu ya uwazaji wa kimantiki (Habwe, 1999). Kasisi huyu ni msomi na mwenye ulumbi wa lugha. Kiwango chake cha elimu na cheo chake kama paroko kinamsukuma kubadilisha msimbo kwa kutumia sentensi ndefu. Hili linachangiwa na kuwa anafahamu wale anaowahubiria. Kama paroko ana uhusiano wa karibu sana na wafuasi wake na hili linaonyesha hali ya utangamano aliyonayo.

Kasisi huyu wa Gilgil anasema ukweli na kuusema kwa njia inayofaa kwa kuzingatia mada husika. Uradidi huu unachangia katika kusisitiza hoja. Ubadilishaji msimbo huu pia unasaidia kueleweka kwa ujumbe kwa vile anaitumia lugha inayoeleweka vema na hadhira yake. Berk (1986:314) akinukuliwa na Ndungu (2001) anasema kuwa utafiti uliofanywa na Pfaff (1979) kuhusu ulumbi wa lugha wa watu wazima ulionyesha kuwa kuchanganya msimbo kwingi kati ya sentensi kunahusishwa na uwezo wa juu wa kuwa na ulumbi. Hivyo kubadilisha msimbo kati ya sentensi kunaweza kuchukuliwa kama kipimo cha uwezo wa kuwa na ulumbi. Hili limejitokeza waziwazi kwa kasisi wa Gilgil ambaye ametumia zaidi ya lugha moja (Kilatini, Kiswahili, Kiingereza na Kiitaliano).

Kasisi pia wa Holy Family Basilica ametumia aina hii ya ubadilishaji msimbo kwa kiasi kikubwa ila hakifikii cha kasisi aliyekwishatajwa.

Mfano [100]

Kama hujagundua hayo bado wewe hujajua. *‘That’s why people should pray for the gift of knowledge’.*

(Kama hujagundua hayo bado wewe hujajua. Ndio sababu watu wanatakiwa kuomba kipaji cha Roho Mtakatifu cha elimu).

Mfano [101]

Yesu itabidi amuinue kwa sababu ya utakatifu wake. *‘What are we doing?’*

(Yesu itabidi amuinue kwa sababu ya utakatifu wake. Tunafanya nini?)

Mfano [102]

Lakini lazima tuombe Roho Mtakatifu. *‘That we are able to appreciate one another’.*

(Lakini lazima tuombe Roho Mtakatifu. Kuwa tunaweza kudhaminiana).

Mfano [103]

Wako na zawadi zao. *‘They have their own gifts’.*

(Wako na zawadi zao. Wana vipaji vyao).

Ubadilishaji msimbo uliotumiwa na kasisi huyu unasisitiza hoja anayoitoa mhubiri. Athari yake kwa mhubiri ni kwamba inasisitiza anachokusudia kusema ikiwa ni pamoja na kuwaweka waumini wake wawe macho ili kufuatilia anachokisema.

Ubadilishaji msimbo katika sentensi unaweza kutokea katika kiwango kidogo cha neno, kirai, kishazi na sentensi kama ilivyodhihirika katika mifano ya awali. Ubadilishaji msimbo huu umedhihirisha utokeaji wake katika kiwango cha neno, kirai, na kishazi katika makanisa yaliyotafitiwa. Mawazo haya yanaoana na ya Poplack (1981), kuwa kuna aina tatu za ubadilishaji msimbo. Ubadilishaji msimbo unaotokea nje ya kishazi au sentensi, unaotokea katika mipaka ya sentensi au kishazi pamoja na ubadilishaji msimbo wa kiungo. Mifano tuliyotoa tayari imedhihirisha hili wazi wazi. Anaendelea kusema kuwa ubadilishaji msimbo unaotokea nje ya kishazi au sentensi ni ule unaotumia zaidi ya lugha moja katika sentensi au vishazi tofauti na hutokea mipakani mwa sentensi.

Kama ilivyodhihirika katika mifano yetu ni kuwa sentensi zenye ubadilishaji msimbo katika kishazi zilibadilisha lugha kutoka Kiswahili hadi Kiingereza, au Kiingereza hadi Kiswahili. Kulikuwa pia lugha za Kilatini na Kiitaliano. Lengo la ubadilishaji huu ni kutilia mkazo na kutaka kupata maoni kutoka kwa msikilizaji. Tuliona pia kuwa ubadilishaji msimbo huu unatokea nje ya kishazi au sentensi kwenye sentensi kamili wakati mpangilio wa elementi ni sawa katika lugha zote mbili.

Ubadilishaji msimbo unaotokea katika mipaka ya sentensi au kishazi hutokea pia katika kiwango cha neno, kirai, kishazi. Uchanganuzi wake unatambulikana kutokana na matumizi yake katika neno, kirai na kishazi kama vile mifano ilivyodhihirisha hapo awali. Kutokana na maelezo haya na mifano tuliokwisha kutoa imedhihirika kuwa ubadilishaji msimbo una majukumu mbalimbali kama vile ubadilishaji wa mada, kutilia mkazo ujumbe, kunukuu, kuonyesha ushirikiano,

kutafsiri, utoshelevu, utani, urudiaji na kadhalika. Pia imedhihirika kuwa hakuna kasisi aliyebadilisha msimbo hadi lugha asilia bali mwingi ulikuwa Kiswahili hadi Kiingereza au Kiingereza hadi Kiswahili kudhihirisha majukumu muhimu yanayotekelezwa na lugha hizi mbili katika mahubiri.

4.3 UHUSISHAJI

Dhana ya uhusishaji imechanganuliwa katika Nadharia ya Grice (1975), na kulingana na Kamusi ya Falsafa ya Staford (2005:44) akinukuliwa na Kariithi (2010), uhusishaji ni jambo lililomaanishwa, lililoangaziwa, lililopendekezwa na dhahiri kinyume na yaliyosemwa. Nadharia ya pili ya Grice aliyoiasisi kwa yakini ni nadharia inayohusu vile watu hutumia lugha. Mapendekezo yake ni kuwa kuna seti ya dhana inayozidi na kuongoza wakati wa mazungumzo. Haya huongozwa na kanuni nne za mazungumzo kama vile tulishakwisha zitaja hapo awali. Uhusishaji unadokeza vile mawasiliano yanavyoweza yakaafikiwa pale ambapo pana upungufu wa njia za makubaliano katika kuelezea ujumbe unaohitajika. Mengi huwasilishwa zaidi kulingana na vile yanavyodhihirika katika usemi. Kwa mfano,

Mfano [104]

Tumesikia ya kwamba Mungu alisema na sasa tumbe mtu binadamu kwa sura na upendo wetu.

'We are created in the image and likeness of God'.

(Tumesikia ya kwamba Mungu alisema na sasa tumbe mtu binadamu kwa sura na upendo wetu.

Tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu).

Mfano huu ulitolewa na kasisi wa Holy Spirit – Gilgil. Una uhusishaji kuwa, Mungu alisema na watu wengi (Mungu mwana na Mungu Roho) na imeonyeshwa kwa wingi (tumble mtu). Mtu aliyeumbwa na Mungu yuko katika sura yake, aidha waliokuwa wakiumba nao pia wana sura na

mfano wa Mungu mwenyewe. Hili lina maana kuwa hata sisi tuliombwa na mfano na sura yake basi haifai tuwe na wasiwasi kwa vile na sisi pia tunafanana na yeye. Mhubiri huyu anawahimiza waumini wake kufurahia kuwa wafuasi wa Mungu kwa sababu wana matumaini ya kufurahia sura waliyoipata kwake Mungu Muumba. Hivyo basi, kama kaida ya idadi haingekiukwa, ingekuwa vigumu kuelewa na kutimilika lengo la kuuwasilisha ujumbe.

Kaida ya namna haijaguswa katika mfano huu kwa vile kasisi huyu hajitengi kutokana na muktadha kwa vile anasema ‘tumeumbwa’. Hivyo sio suala la mtu mmoja ila jamii yote ya waumini yeye akiwa mmoja wao. Kaida ya uhusiano imejitokeza zaidi katika kuhusisha chochote wahubiri wanakusudia kuwasilisha kwa njia ya ubadilishaji msimbo.

Mfano [92] ukirudiwa hapa kama mfano [105]

Mfano [105]

‘*You see*’ bila karama ya bibi yako utaaibika.

(Unaona bila karama ya bibi yako utaaibika).

Mhubiri anategemea uelewa wa awali walionao waumini wake. Kuwa chochote kisemwacho kitachukuliwa kilicho na ukweli. Mtindo wa lugha unaotumiwa unakiuka kaida ya uhusiano lakini hata hivyo inasaidia kuunganisha ulimwengu wa kiungu na wa binadamu. Ukiukaji huu unamsaidia kuwasiliana na waumini kuamini kuwa ili kuishi bila taabu binadamu anahitaji karama.

Hivyo, licha ya kuwa kuna maana inayowasilishwa katika mawasiliano kupitia vipengele vya kisemantiki, kuna ukiukaji wa kanuni za Grice ili kutoa maana ya ziada na inayomaanishwa. Uhusishaji wa kimazungumzo unategemea muktadha husika sana na hali iliyopo pamoja na

uelewa wa awali kati ya mhubiri na hadhira yake. Ukiukaji wa kanuni hizi basi unasaidia mhubiri kupitisha ujumbe alionao vema hivyo kutimiza haja yake ya kuwasaidia waumini wake kubadili mienendo na kuishi maisha adilifu.

4.4 UBADILISHAJI MSIMBO NA UHUSISHAJI

Maswali ambayo tunaweza kujiuliza ya kipragmatiki ni kuwa, mbona wahubiri hawa wakatumia maneno haya ya Kiingereza wanapohubiri? Tunachokiona kwa hawa wote ni kuwa ni wasomi wa viwango vya juu na wenye uelewa wa hadhira yao. Hivyo basi, wanaweza kuwa wamechangiwa na uelewa kuwa wafuasi wao wanawaelewa vyema na wanauelewa mzuri wa lugha zote mbili wakitilia manani sehemu kanisa hizi ziliko. Matumizi ya Kiingereza yanaweza kuhusishwa na vyeo na uhusishaji wa wahubiri hawa. Wanataka kujihusisha na kile wanachokizungumza. Mfano mzuri ni kasisi wa Holy Family Basilica anayejihusisha na Baba Mtakatifu katika mwanzo wa ibada anapowasihi wote waunganike na Baba Mtakatifu kuombea amani. Vile vile anajua kuwa mahali kanisa lake liko ni mahali hata wana habari wanaweza kufika wakati wowote. Hivyo ujumbe huu wa imani anaukazia sana kasisi huyu na kuomba watu wa makabila yote kuishi kama ndugu. Hivyo anahubiri kama mzalendo sio tu kwa kabila au tabaka moja bali watu wenye michanganyiko ya kila namna. Kwa mfano.

Mfano [106]

Tumesikia katika somo la pili, Paulo akisema, akituambia ya kwamba karama ni nyingi *'but we are different'* lakini tukiunganishwa na roho mmoja, kwa sababu roho wa Mungu anatuunganisha pamoja ili karama hizi zote, tofauti hizi zote ziwe faida kwetu sisi wote.

(Tumesikia katika somo la pili, Paulo akisema, akituambia ya kwamba karama ni nyingi lakini tuko tofauti, lakini tukiunganishwa na roho mmoja, kwa sababu roho wa Mungu anatuunganisha pamoja ili karama hizi zote, tofauti hizi zote ziwe faida kwetu sisi wote).

Hali hii inajitokeza pia kwa askofu ambaye anaelewa kuwa yeye kama mchungaji mkuu anao wajibu wa kuwaunganisha watu wote. Kama kasisi wa Basilica pia anaanza kwa kuwasihi wote waunganike pia na Baba Mtakatifu kuombea na kudumisha amani. Vile vile anapaelewa vema mahali alipo. Sehemu ya Gilgil ina makabila yote ya watu na zaidi ya yote ina waumini askari wa Anti-Stock Theft Unit (ASTU) ambao makazi yao yako Gilgil na ni washiriki wa kanisa hili. Kundi hili la maaskari ni muhimu katika utafiti huu kwa vile ni kundi lenye mchanganyiko wa sifa za kuwa katika vyeo mbalimbali, makabila mbalimbali, tofauti za tajriba za kikazi ikiwa ni pamoja na hadhi mbalimbali za kikazi. Hoja hizi zinachangia katika namna mhubiri atawachukulia na kuwaelewa anapohubiri. Katika sehemu hizi basi za Gilgil na Nairobi tunagundua kwamba ubadilishaji msimbo uko katika Kiswahili na Kiingereza na wala hakuna matumizi ya lugha za wenyeji. Hii ni kwa sababu Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha zinazotumika kwa wingi wakati wa mahubiri. Kwa mfano, kasisi wa Holy Basilica anasema,

Mfano [107]

‘Watu wote wako na karama na kuna faida katika karama zao. Lakini ni lazima tuombe Roho Mtakatifu. *“that we are able to appreciate one another,”* kulingana na mimi wakati tutaweza wanakenya kuona hizi tofauti *“we don’t have to be the same”*’.

(Watu wote wako na karama na kuna faida katika karama zao. Lakini ni lazima tuombe Roho Mtakatifu, kuwa tunaweza kukubali kila mmoja wetu jinsi tulivyo, kulingana na mimi wakati tutaweza wanakenya kuona hizi tofauti na kwamba si lazima kuwa sawa).

Msukumo walio nao wahubiri huwa umechangiwa pakubwa na kutaka kudumisha mawasiliano na ushirikiano baina yao ambazo ni kaida za Grice wanazitimiza bila kukusudia. Kama ilivyodhihirika baadhi yao kama askofu anatumia neno '*prolife*' kwa vile hana kisawe chake na hivyo basi anabadilisha msimbo, Saville-Troike (1989) akinukuliwa na Habwe (1999).

La ajabu ni kwamba makasisi hawa na askofu hakuna hata mmoja wao aliyevutwa kuzungumza lugha ya kwanza. Kwa nini basi? Kwa vile matumizi ya lugha ya Kiswahili mijini inadhaminiwa kama lugha ya wanaojua kusoma na wenye vyeo sawia na Kiingereza. Sifa hizi za kipragmatiki zinajitokeza sio tu kwa askofu bali pia kwa makasisi waliotafitiwa hususan kasisi wa Holy Family anaporudia mara kwa mara huku akijirejelea '*Father*'. Katika kudhihirisha cheo chake na wajibu wake anarudiarudia neno hili '*Father*'. Jukumu la ubadilishaji msimbo hapa ni kutilia mkazo na kutia nguvu kile anachokisema. Kwa mfano kasisi wa Holy Basilica anasema,

Mfano [108]

Siku moja anasema '*aah father*' hapana wacha kuogopa unajua nyinyi mnaogopa sana. Wacha nikwambie siku moja hiyo nyumba yake kitanda yote, godoro yake ilishika moto akaniambia '*father*' si ni nyinyi hamkununua '*socket*'.

(Siku moja anasema aah padri hapana wacha kuogopa unajua nyinyi mnaogopa sana. Wacha nikwambie siku moja hiyo nyumba yake kitanda yote, godoro yake ilishika moto akaniambia padri si ni nyinyi hamkununua soketi).

Kutokana na hoja hizi ni wazi kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza zilitumika kubadilisha msimbo kama lugha kuu zinazotumika nchini na majukumu yake ya kuwa lugha rasmi na Kiswahili licha ya kutumika katika shughuli rasmi pia ni lugha ya kitaifa. Lililodhihirika ni kuwa labda kama wahubiri hawa wangetumia tu lugha moja iwe Kiswahili au Kiingereza huenda waumini wao wasielewe vilivyo kwani wataziona lugha hizo tu kama za wasomi wa tabaka la juu, Mutahi (1980) akinukuliwa na Habwe (1999). Hata hivyo, mhubiri kwa kutumia Kiswahili anaonekana anayeijali hadhira yake na kuonekana kama mwenye kuitumia lugha wanavyoielewa zaidi. Hata hivyo anayetumia Kiswahili bila kubadilisha chochote ataonekana kama ambaye kiwango chake ni cha chini kuliko anayebadilisha msimbo na kutumia Kiingereza.

4.5 HITIMISHO

Sehemu hii imeangazia ubadilishaji msimbo katika makanisa yaliyotafitiwa wakati wa mahubiri. Lililobainika wazi ni kuwa wahubiri hutumia ubadilishaji msimbo katika mahubiri yao. Tumedhihirisha kuwa kuna utofauti wa namna mhubiri hubadilisha msimbo kutegemea vipengele kama vile umri, hadhi ya mhubiri, tajriba yake, elimu, uhusiano na waumini wake miongoni mwa mengine. Kila kasisi basi hudhihirisha sifa zake za kipekee katika namna anavyoitumia lugha. Aidha wahubiri hawa huongozwa na huzingatia kaida za umaanisho hata bila hao kugundua.

Ubadilishaji huu pia umedhihirika kujitokeza katika kiwango cha sentensi. Madhumuni au umuhimu wa ubadilishaji msimbo umedhihirika pia ikiwa ni pamoja na kuuimarisha uhusiano kati ya mhubiri na waumini wake, kusisitiza hoja fulani, kunukuu jambo, kuwafanya waumini wawe macho wakati wa mahubiri na kadhalika.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO NA MUHTASARI

Mwanzoni mwa utafiti huu tulikuwa na haipotesia zifuatazo;

1. Ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu.
2. Wahubiri katika Kanisa Katoliki huchanganya msimbo.
3. Ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi.
4. Kiwango cha elimu, tabaka, cheo, tajriba na umri wa mhubiri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

Katika utafiti huu tuliweza kukusanya mahubiri saba katika majimbo yaliyoteuliwa ya Nairobi na Nakuru. Katika jimbo la Nairobi tuliweza kurekodi mahubiri manne; mawili kutoka kila kanisa na matatu kutoka jimbo la Nakuru katika kanisa moja lililoteuliwa. Mahubiri yote yalirekodiwa katika mwezi wa Juni. Hata hivyo, kati ya haya saba, mtafiti aliamua kutumia manne tu, mawili kutoka Nairobi na mawili kutoka Nakuru. Hii ni kwa sababu ingekuwa kazi nyingi sana kuyachanganua yote. Vile vile yaliyoteuliwa yalikitidhi mahitaji ya utafiti kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na yale tuliyoyaacha. Mahubiri haya yaliyoteuliwa ndiyo yaliyokitidhi mahitaji ya utafiti huu kwa kiasi kikubwa yakilinganishwa na yale mengine.

Makanisa haya yaliteuliwa kutokana na mchanganyiko mzuri uliomo wa watu wanaoishi katika sehemu hizi. Wanaoishi sehemu hizi wana vyeo mbalimbali, kazi mbalimbali, elimu ya viwango tofauti tofauti miongoni mwa mengine. Aidha lugha zinazotumika katika majimbo haya ni Kiswahili na Kiingereza. Utofauti wa majimbo haya kihadhi pia ulitiliwa maanani. Tuliamua

kurekodi mahubiri ya Jumapili na sio ya katikati mwa juma kwa vile kanisani Jumapili waumini huwa wengi na wenye sifa maridhawa ikilinganishwa na katikati ya juma.

Utafiti huu ulijikita katika kipengele cha ubadilishaji msimbo katika mahubiri ya Kanisa Katoliki. Tuliangalia vile ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu katika kiwango cha neno, kirai na sentensi. Pia tuliangalia jinsi wahubiri katika kanisa hili la Katoliki huchanganya msimbo na kuwa ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi. Vile vile tuliangalia kuwa kiwango cha elimu, tabaka, cheo, tajriba na umri wa mhubiri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umaanisho ya Grice (1975) inayobainisha uhusiano baina ya maana ya msemaji, maana inayotokana na vipashio vya sentensi na maana inayoibuka kulingana na maneno katika sentensi.

Katika sura ya pili tuliangalia uelewa wa kinadharia wa ubadilishaji msimbo. Tulianza kwa kutoa maelezo ya lugha wakati wa mahubiri. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa kilicho cha maana sana ni jinsi mhubiri anavyoitumia lugha yake kuhakikisha kuwa wanaohubiriwa wanayafuata mahubiri ili kuridhisha hamu yao ya kuunganika na Mungu. Vile vile tuliona kuwa kuchanganya msimbo ni tukio ambalo ni la kawaida nchini Kenya ambapo watu hubadilisha lugha moja hadi nyingine katika tukio la kiuzungumzaji. Tamko linalohusika hudhihirisha sifa za lugha tofauti zinazohusika. Imedhihirika pia kuwa misimbo inayochanganywa mara nyingi ni Kiswahili na Kiingereza ingawa wakati mwingine watu huchanganya msimbo wakitumia lugha zao za kiasili kama vile Kijaluo, Kimaasai, Kikamba na kadhalika. Katika utafiti huu tulizingatia ubadilishaji msimbo kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza au Kiingereza hadi Kiswahili na hakukuwa na ithibati ya ubadilishaji msimbo uliohusisha lugha za kiasili ila ulihusu Kiswahili,

Kiingereza, Kilatini na Kiitaliano kwa kiasi kidogo. Tumeona kuwa ubadilishaji msimbo ni jambo ambalo hujitokeza kanisani pia kwa vile yapo mazingira ya uwililugha. Aidha tulielezea sababu zinazowafanya wahubiri kubadilisha msimbo, na aina za ubadilishaji msimbo. Pamoja na haya tulielezea majukumu mbalimbali ya ubadilishaji msimbo na athari za ubadilishaji msimbo. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa ubadilishaji msimbo una majukumu mengi sana pamoja na athari ya jinsi maana inavyowasilishwa.

Katika sura ya tatu tulichanganua data tuliyoirekodi katika kiwango cha neno. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa wahubiri hubadilisha msimbo katika kiwango cha neno. Ubadilishaji huu unachangiwa na ushirikiano baina ya kasisi na waumini wake. Wahubiri walibadilisha msimbo kimpishano kati ya lugha mbili tofauti kwa nia ya kuhusisha wengine ili kutoa athari ya upekee au kuanzisha utangamano. Ubadilishaji msimbo huu ulilenga pia kudumisha na kuendeleza uhusiano wa mawasiliano kati ya wahubiri na waumini na hivyo basi kufanikisha upitishaji wa ujumbe kwa waumini wake. Wahubiri walionekana kubadilisha msimbo katika kiwango cha neno wakiwa na sababu mbalimbali kama vile kutaka kutumia muda au maneno machache kueleza jambo fulani, kunukuu kifungu fulani kutoka lugha nyingine, wahubiri kuwa na mielekeo hasi kuhusu baadhi ya istilahi za Kiswahili wanazozitumia, ukosefu wa kisawe kwa sababu ya msamiati wa kiteolojia na kadhalika.

Sura ya nne ilihusu uchanganuzi wa ubadilishaji msimbo katika kiwango cha sentensi. Ubadilishaji msimbo huu ulijitokeza sana kwa wingi kuliko ule wa neno hususan katika makanisa mawili ya Holy Family Basilica na Holy Spirit- Gilgil tofauti na kanisa la Consolata Westlands ambalo ubadilishaji wake mwingi ulikuwa katika kiwango cha neno na uliokuwa

asilimia ya chini sana. Wahubiri walizitumia aina mbili za viwango vya sentensi kwa wingi sana. Kulidhihirika ubadilishaji msimbo kati ya sentensi na ubadilishaji msimbo baina ya sentensi. Ubadilishaji msimbo katika sentensi ulidhihirika kutokea katika sentensi, kishazi, kirai na maneno. Ubadilishaji huu ulionekana kuongozwa na kaida za wana uwililugha katika jamii husika ya waumini iliyotafitiwa. Ubadilishaji msimbo kati ya sentensi ulijitokeza kwa wingi sana katika utafiti huu. Kasisi wa Gilgil alibadilisha msimbo katika lugha za Kiswahili, Kiingereza. Kiitaliano na Kilatini. Kasisi huyu alichanganya lugha zaidi ya moja katika sentensi moja. Maneno aliyoyatumia yameundwa kwa kutumia sheria za kimofolojia za lugha nyingine kama inavyodhihirika. Matumizi haya yalitokea kwa kuwa hakuwa na kisawe na vile vile alitaka kusesitiza alichokisema. Ubadilishaji msimbo huu ulidhihirisha matumizi ya takriri kwa nia ya kutaka kusesitiza kinachosemwa. Umetumika pia kwa lengo la kunukuu au kurejelea.

Katika hali ya ubadilishaji msimbo, makasisi hawa walichanganya Kiswahili na Kiingereza bila kuvunja sheria za kisintaksia za lugha zote mbili. Lugha zote ziliingiliana katika sheria zake za kuunda sentensi. Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi pia ulitumiwa kwa wingi na makasisi wawili wa Holy Spirit Gilgil na Holy Family Basilica. Ubadilishaji msimbo huu ulijumuisha kubadilisha sentensi kwa namna ambayo kila kishazi au sentensi kilikuwa katika lugha moja. Sentensi moja iligawanywa mara mbili na lugha zinazohusika. Kila sentensi iliundwa kwa kuzingatia sheria za utunzi wa sentensi wa lugha husika.

Ubadilishaji msimbo huu wa baina ya sentensi ulitoa dhana ya uradidi kwa nia ya kusesitiza kupitia kurudia katika lugha nyingine. Ubadilishaji huu pia ulionyesha matumizi ya sentensi ndefu ambazo tunaweza kuhusisha na hali ya juu ya uwazaji wa kimantiki. Ubadilishaji msimbo

katika kiwango cha sentensi ulidhihirisha kuzingatia kaida ya Grice ya ushirikiano pamoja na kudhihirisha kuwa wahubiri walidumisha uhusiano na waumini wao. Ubadilishaji msimbo huu pia ulisaidia kueleweka kwa ujumbe kwa vile wahubiri walitumia lugha inayoeleweka vema na hadhira yao. Ubadilishaji msimbo huu ulidhihirisha pia ulumbi wa lugha ulioonyesha kuwa kuchanganya msimbo kwingi kati ya sentensi kunahusishwa na uwezo wa juu wa kuwa na ulumbi. Hivyo kubadilisha msimbo kati ya sentensi kunaweza kuchukuliwa kama kipimo cha uwezo wa kuwa na ulumbi. Mawazo mazito na dhana ambazo hazingeweza kueleweka zilionekana kuwasilishwa kupitia ubadilishaji msimbo huu katika kiwango cha sentensi. Uhusishaji ulidhihirika kuwa muhimu katika kuielewa maana kama ilivyowasilishwa na jinsi wahubiri walivyoitumia lugha. Uhusishaji ulisaidia katika kudokeza vile mawasiliano yalivyoweza kuafikiwa pale ambapo palikuwa na upungufu wa njia za makubaliano katika kuelezea ujumbe uliohitajika. Kupitia uhusishaji mengi yaliweza kuwasilishwa zaidi kulingana na vile yalivyodhihirika katika usemi.

Hivyo, licha ya kuwa kuna maana inayowasilishwa katika mawasiliano kupitia vipengele vya kisemantiki, kulitokea ukiukaji wa kanuni za Grice ili kutoa maana ya ziada na inayomaanishwa. Uhusishaji wa kimazungumzo unategemea muktadha husika sana na hali iliyopo pamoja na uelewa wa awali kati ya mhubiri na hadhira yake. Ukiukaji wa kanuni hizi ulisaidia wahubiri kupitisha ujumbe waliokuwa nao vema hivyo kutimiza haja yao ya kuwasiliana. Wahubiri walibadilisha msimbo kwa kutumia lugha ya Kiingereza ambayo inahusishwa na vyeo na tajriba walionao katika kazi hii ya uendeshaji wa ibada. Ubadilishaji msimbo mwingi ulikuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza na wala hakukuwa na matumizi ya lugha za wenyeji. Hii ni kwa sababu Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha zinazotumika kwa wingi wakati wa mahubiri.

Kutokana na hoja hizi ni wazi kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza zilitumika kubadilisha msimbo kama lugha kuu zinazotumika nchini na majukumu yake ya kuwa lugha rasmi na Kiswahili licha ya kuwa inatumika pia katika shughuli rasmi pia ni lugha ya kitaifa. Lililodhihirika ni kuwa kama wahubiri wangetumia tu lugha moja iwe Kiswahili au Kiingereza huenda waumini wao wasielewe vilivyo kwani wataziona lugha hizo tu kama za wasomi wa tabaka la juu.

Kutokana na utafiti huu imedhihirika kuwa haipotesia nne tulizokusudia kuzipima zimetimilika kwa vile imebainika wazi kuwa wahubiri hutumia ubadilishaji msimbo katika mahubiri yao kwa wingi. Aidha ubadilishaji msimbo huu katika diskosi ya mahubiri unaathiri maana katika kiwango cha matumizi ya elementi za kiisimu kama vile sentensi na maneno.

Tuliona pia kuwa ubadilishaji msimbo katika diskosi ya mahubiri husababisha ukosefu wa urasmi ila ukosefu huu unachangia pakubwa namna maana inavyowasilishwa na vile ujumbe unavyopokelewa. Aidha imedhihirika kuwa kiwango cha elimu, tabaka, cheo, tajriba na umri wa mhubiri husababisha mabadiliko ya jinsi lugha inavyotumika.

5.1 MAONI NA MAPENDEKEZO

Utafiti huu ulijishughulisha na ubadilishaji msimbo katika mahubiri ya Kanisa Katoliki ambapo ilidhihirika matumizi mengi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza, Kilatini na Kiitaliano kwa kiasi kidogo. Tulifanikiwa kuyajibu baadhi ya maswali ilhali tulikumbana na mengine ambayo hayangejibiwa na utafiti huu kutokana na upeo na mipaka ya utafiti wenyewe. Hivyo basi tunatoa pendekezo kuwa tafiti zaidi zifanyike katika taaluma hii ya isimu kwa vile ilidhihirika

uhaba mkubwa hasa unaohusu mahubiri katika Kanisa Katoliki. Nyingi ya tafiti zilizofanywa zina mwegemeo wa kiteolojia na upande wa isimu umepuuzwa kwa kiasi kikubwa labda kwa vile linatazamwa kama suala la kiimani. Utafiti huu basi unafaa kuwa changamoto kwa watafiti wa baadaye kwa kugemea upande wa isimu na katika vipengele zaidi wakati wa ibada ya misa. Vile vile kwa sababu ya muda na wakati, tuliweza kurekodi mahubiri bila kuchukua video. Ni tumaini letu kuwa watafiti wajao wataweza kurekodi pamoja na kuchukua video kama njia ya kuwawezesha kuzielewa ishara mbalimbali wanazozitumia wahubiri katika ibada ya misa.

MAREJELEO

- Akinyi, J. na Kwach, E. (2012) *Manifesting of Formal and Informal Codeswitching*. Nairobi: Academic Research International (vol.2, No. 2).
- Andréia, C. (2002) *Power in Religious Discourse: A discourse analysis of two sermons from the Universal Church of the Kingdom of God*. PhD Dissertation. Universidade Federal de Santa Catarina.
- Bailey, Benjamin (2000) *Language and Negotiation of Ethnic/racial identity among Dominican Americans*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Bazerman, C. na Prior, P. (2008) *What Writing Does and Does it? An Introduction to Analyzing Texts and Textual Practices*. New Jersey: Lawrence Erlbaum Associates, Inc;
- Brown, H.C. na wengine (1963) *Steps to Sermon: A Plan for Sermon Preparation*. Nashville: TN Broadman Press.
- Brown na Yule (1983) *Discourse Analysis: The Sociolinguistic analysis of Natural Language*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Buliba na wenzake (2006) *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Chapman, G. (1994) *Catechism of the Catholic Church*. Great Britain: The Bath Press.
- Code of Canon Law (1975) *Canon Law Society of Great Britain and Ireland*: Harper Collins Publications.
- Crystal, D. (1965) *Linguistics, Language and Religion*. London: Burns na Oates.
- Crystal, D. (1997) *The Cambridge Encyclopaedia of Language*: Cambridge: Cambridge University Press.

Djoko Susanto (2006) *Codeswitching in Islamic Religious Discourse: The Role of Insha'Allah*

University of Queensland: Brisbane, Australia.

Edwards, V. (1983) *Language in multicultural classrooms*. Batsford: Academic & Educational

Limited.

Flannery, O.P. (1975) *Vatican Council 2 vol. 1 The Councillar and Post Concillar Documents:*

Mumbai: St. Paul's Publishers.

Fromkin, V. na Rodman, R. (1998) *An introduction to language*. Fort Worth: Hacourt Brace

College Publishers.

Furrakh, A. Ph.D. na wengine (2011) *Code-Mixing as a Communicative Strategy among the*

University Level Students in Pakistan. New York: Academic Press.

Grice, H. (1975) *Logic & Conversation*. In *Syntax & Semantics vol.3 Speech Acts*, ed Pole and J.

Morgan (Eds), New York: Academic.

Gumperz, J & Hymes (Eds) (1972) *Directions in Social Linguistics*. New York: Holt Renehart &

Winston.

Gumperz, J. J. (1982) *Discourse strategies*. Cambridge: Cambridge University Press.

Habwe, J. H. (1999) *A Discourse Analysis of Swahili Political Discourse*. Unpublished PhD

Thesis. Nairobi: University of Nairobi.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Halliday, Michael (1973) *Explorations in the Functions of Language*. London: Edward Arnold.

_____ (1994) *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

Hirst, G. (1986) *Semantics and Pragmatics*. United Kingdom: Cambridge University Press.

Hofmann, R. (1993) *Realms of Meaning*: London: Longman.

- Indede, N. (2007) *Lugha ya Kitamathali katika Mahubiri ya Dini ya Kikristu*. Ph.D. Dissertation, Chuo Kikuu cha Maseno.
- Ipara, I.O na Maina, G. (2008) *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kachru, B. (1983) *The Indianization of English: The English Language in India*. Delhi, India: Oxford University Press.
- Kanana, F. E. (2003) *Code Switching in Business Transactions: A case study of Repertoire in Maasai Market in Nairobi, Kenya*. M.A. Thesis, Kenyatta University: Nairobi.
- Kariithi (2010) *Mikakati ya Upole ya Lugha katika Matumizi ya Lugha ya Vijana*. M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- King'ati, J. (2002) *Discourse Analysis in Swahili Homilies*. Unpublished PhD Thesis. Nairobi: University of Nairobi.
- King'ei, K.G. (1992) *Language, Culture and Communication: The Role of Swahili Taarab Songs in Kenya, 1963-1990*, Ph.D. Dissertation, Howard University.
- Leech, G. (1983) *Principles of Pragmatics*. London: Longman Group Ltd.
- Linda, T. na Wareing, S. (1999) *Language, Society and Power*. London: Routledge.
- Magesa, L. (1993) *African Religion: The Moral Traditions of Abundant Life*. Nairobi: Pauline Publications.
- Malmamkjaer, K. (2004) *Linguistics Encyclopedia 2nd Edition*. New York: Routledge.
- Massey, J. (1980) *Designing the Sermon: Order and Movement in Preaching*. Nashville: Abingdon Press.
- Mghambi, S. (1991) *Ukiushi katika Lugha ya Kimaongezi Dhidi ya Kanuni za Kiswahili Sanifu*. Tasnifu, Chuo Kikuu cha Nairobi: Nairobi.

- Mroso, J. (1995) *The Church in Africa and New Evangelisation: A Theologico- Pastoral Study of the Orientations of John Paul 2*. Italy: Gregorian University Press.
- Muthuri D. (2000) *Functions of Code switching among multilingual students at Kenyatta University*, Unpublished Master's Thesis, Kenyatta University: Nairobi.
- Mwandije, M. (2004) *English - Kiswahili Code Switching in Easy FM; Markedness Model*. University of Nairobi.
- Ndung'u, V. (2001) *Uchanganuzi wa Usemi katika Sajili ya Dini: Sifa bainifu za Lugha ya Mahubiri*. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Nairobi.
- New Catholic Encyclopedia* Vol. V11 (1967) The Catholic University of America: Washington.
- Ogechi, N.O. (2002) *Codeswitching in Kenya Evidence from Ekegusi, Kiswahili, English and Sheng*: Doctoral Dissertation, University of Hamburg.
- Ogula, P. (1998) *A Handbook on Educational Research*. Nairobi: New Kemit Publishers.
- Poplack, S. (1980) '*Sometimes I will start a Sentence in Spanish y termino en Espanol*' Toward a typology of Code Switching. *Linguistics* 18 (pp.581-618).
- Poplack, S. (1981) *Syntactic structure and social function of codeswitching*. Norwood, NJ: ABLEX, pp. 169-184. Canada.
- Pride, J. B. (1971) *The Social Meaning of a Language*. New York: Oxford University Press.
- Romaine, S. (1994) *Language in Society: An Introduction to Sociolinguistics*. Oxford: Oxford Press.
- Scotton, M. (1993) *Social Motivations for Code Switching: Evidence from Africa*. Oxford: Oxford University Press.
- Shaimaa, E. (2012) *Critical Approaches to Discourse Analysis across Disciplines*: Lancaster University and Fayoum University. Vol. 6 (1): 76 – 95.

Suwito (1985) *Background of code mixing...* [www.http:// infoskripsi.com/](http://infoskripsi.com/) Article

The Herald online. Harare: Zimpapers. Available at [www. herald.co.zw](http://www.herald.co.zw)). Accessed 13, 14, 15,

16, 17, 19, 20 September 2011.

Turnbull, R. (1967) *Baker's Dictionary of Practical Theology*. Michigan: Oxford University Press.

Wanjugu, V. (2010) *Sababu na Athari za Ubadilishaji Msimbo Shuleni: Utafiti katika Shule ya*

Upili ya Akiba. M, A Thesis. Chuo cha Nairobi.

VIAMBATISHO

MAHUBIRI YA 1- KANISA LA HOLY SPIRIT - GILGIL (NA ASKOFU) SIKUKUU YA PENTEKOSTE

Hi, hamjui Ndingi aliondoka? [Utani alioufanya Baba Askofu kwa sababu paa la jukwaa alimosimama lilikuwa fupi sana, ilhali yeye ni mrefu kuliko aliyemtangulia] [Watu waliangua kicheko].

Askofu: Tumsifu Yesu Kristo,

Waumini : Daima na milele.

Leo tunasherekea sikukuu ya *'Pentecost'*, vile nilisema mwanzo wa misa, Baba Mtakatifu ameomba tushirikiane na yeye kanisa zima ulimwenguni mwote ili kuombea amani. Amani katika mashariki ya kati, kati ya nchi ya Israeli na nchi ya Palestina. Lakini pia amani ulimwenguni kote. Tuombe amani katika nchi yetu ya Kenya ili sote tuweze kuishi kama ndugu bila kuzozana, bila kuuana, na bila kugombana.

Leo ni sikukuu ya Roho Mtakatifu. Na leo ni sikukuu ambapo, tunaona dhahiri uwepo wa Roho Mtakatifu katika maisha ya waumini. Roho Mtakatifu amekuwapo tangu mwanzo sio kwamba Roho Mtakatifu ameanza kuwepo wakati wa Pentekoste. Roho Mtakatifu amekuwapo tangu kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Kulipoumbwa ulimwengu, Roho Mtakatifu alikuwepo. Tunaelewa vizuri hata Mungu alimuumbia binadamu, Adamu na Awa, Roho Mtakatifu alikuwapo, na Mungu alimvuvia Adamu na Awa, maanake aliwapa Roho, wakaanza kuishi kwa Roho wa Mungu kwa hivyo Roho Mtakatifu amekuwapo tangu mwanzo. Lakini sherehe ya leo, inatupa funzo la kipekee juu ya uwepo huu wa Roho Mtakatifu wakati wa kanisa baada ya kifo na ufufuko wake Yesu Kristo. Leo ni siku inayokamilisha kipindi cha pasaka. Tumeanza tangu

ufufuko, tumekuja kupaa kwa Bwana mbinguni, leo ni sikukuu ya Roho Mtakatifu, siku inayokamilisha kipindi cha pasaka. Maanake leo, sikukuu ya Roho Mtakatifu ni sikukuu inayodhihirisha utimilifu wa ufufuko, wa Bwana wetu Yesu Kristo, na ni vizuri kuelewa sote kama ni sherehe zinazofanywa sehemu za fumbo moja, fumbo la pasaka.

Tulipokuwa tunasherehekea pasaka, tunakumbuka vizuri, pasaka ya kikristo, ilifananishwa kwa njia ya kipekee na pasaka ya Kiyahudi. Wayahudi walisherehekea pasaka ili kukumbuka, jinsi walivyoondolewa kutoka katika utumwa Misri, na kuingia Kanani nchi ya ahadi. Hiyo ndiyo ilikuwa maana ya pasaka kwa Wayahudi. Kwa wakristo pia, kusherehekea pasaka ilikuwa kukumbuka, au kusheherekea kuondolewa kwa wakristo kutoka utumwa, lakini wakati huu sio Wamisri, lakini ni utumwa wa dhambi, na utumwa wa mauti. Katika sherehe ya Pentekoste, Wayahudi walisherehekea jinsi wao walifanywa, na kuundwa kama taifa. Walipotoka Misri, wakafika Mlima Sinai, Mungu akawapa amri kumi, hapo ndipo walipoundwa kama taifa, kwa kupokea amri kumi za Mungu kupitia kwa Musa. Kwa hivyo '*Pentecost*', ilikuwa sherehe ya kukumbuka kupokea sheria, amri ya Mungu. Na wakristo je? Hivyo hivyo. Katika agano jipya, kile ambacho tunasherehekea leo, tunapokea sheria mpya, ambayo ni Roho Mtakatifu, kupitia kwa Musa wa agano jipya, ambaye ni Yesu Kristo. *[Askofu akamwambia mtumishi wa misa aliyekuwa amesimama kando yake: "Keti tafadhali, unaweza kuanguka ukamlaumu askofu"- Askofu alifanya utani).*

Kwa hivyo leo tunasherehekea Pentekoste. Wao walipokea amri kumi, nasi tunapokea amri pia ya Mungu, Roho Mtakatifu, kupitia kwa Musa wa agano jipya, ambaye ni Yesu Kristo. Na katika sheria hii, ya kupokea Roho Mtakatifu, agano jipya, nini kinafanyika? Katika agano la kale,

Mungu alipowaumba Adamu na Awa, akawavuvia, nini kilifanyika kwao? (*KIMYA KIDOGO*) Walikuwa na uhai. Wakaanza kutembea hapa na pale. Wakaweza kutenda hiki na hicho, maana yake, ni kwa nguvu za uwezo wa Mungu peke yake, ndipo Adamu an Awa, waliweza baada ya kupokea roho wa Mungu, kuvuviwa, walipokea uhai, walipokea uzima, wakaanza kuishi. Kwa Roho Mtakatifu, roho wa Mungu, kwa sababu walivuviwa na Mungu. Na katika agano jipya, nini kinafanyika? Tunasherehekea nini leo? Tunasherehekea kile ambacho kimependeka katika injili, Yesu Kristo wanafunzi wakiwa pamoja, ametokezea kwao akawaambia amani iwe kwenu, akawaambia pokeeni Roho Mtakatifu. Tunaambiwa akavuvia, jinsi Mungu alivyowavuvia Adamu na Awa katika kitabu cha mwanzo. Hapa kuna mwanzo mpya, mwanzo wa agano jipya. Yesu Kristo anawavuvia wanafunzi wake, mitume, na jinsi Adamu na Awa walipokea uhai, kwa uwezo wa kuvuviwa na Mungu, mitume wa Yesu Kristo katika injili ya leo, wanapata uzima. Lakini uzima gani? Uzima wa milele. Adamu na Awa walipokea uzima, uhai, *'life'*. Katika agano jipya, Yesu Kristo anapowavuvia mitume, hao pia wanapata uzima, uhai, lakini uzima wa milele, *'eternal life, this is celebration of Pentecost'*.

Katika Kanisa Katoliki kuna kikundi ambacho kinaitwa *'pro-life'*, wale watu ambao wanaoendeleza mambo ya uhai wa binadamu, na kutilia maanani haki za uhai wa binadamu, *'pro-life'*. Leo tunazungumzia sio tu *'pro-life'*, tunazungumzia *'pro-life eternal'*. Hao ambao huwa wanazungumzia *'prolife'*, wanaitwa *'pro-lifers'*. Lakini sisi tunaazungumzia siku ya leo, tunaitwa, *'eternal pro-lifers'*. Mnaelewa wakristo? (*watu wanacheka*). Hiyo ndio maana ya sherehe ya leo. Kwamba Adamu na Awa walipokea uzima na uhai, kwa nguvu za roho wa Mungu.

Leo tunasherehekea jambo kwamba Kristo alipofufuka, aliwawuvia wanafunzi wake, nao wakapokea uhai mpya wa uzima wa milele. Kwa hivyo sherehe ya ufufuko, sherehe ya kupaa na sherehe ya Roho Mtakatifu ni sherehe moja. Yesu Kristo aliwawuvia Roho Mtakatifu punde baada ya kufufuka, hakungojea siku hamsini ndio wawuvie Roho Mtakatifu, hapana! Kwa sababu sherehe ya kufa na kufufuka kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ndio ilikuwa sherehe ya kuingia katika utukufu wa baba, na kuingia katika utukufu wa baba, ndiko kulikokuwa kupaa mbinguni, na katika kupaa mbinguni utukufu wa baba, ndiko kuwawuvia wanafunzi wake Roho Mtakatifu, kwa sababu yeye hayupo tena, hayupo tena katika mwili, lakini yupo katika wanafunzi wake. Ndio sababu aliwawuvia wanafunzi wake Roho Mtakatifu, ili kwamba ingawa yeye hayupo katika mwili wake, yeye atakuwepo katika miili ya wanafunzi wake, na hili ndilo fumbo la paska, fumbo la Pentekoste ambalo tunasherehekea leo.

Yesu Kristo kawavuvia Roho Mtakatifu, yeye hayupo katika mwili wake, lakini yeye yupo katika miili ya mitume wake. [*Bwana Luka Kiiru akamwaga maji yaliyokuwa yamelowa kwenye hema naye askofu akafanya mzaha na kusema: “hawa wamepokea Roho Mtakatifu kwa maji ya ubatizo kutoka juu!” Nao umati wa watu ukaangua kicheko*]. Kwa hivyo kila mkristo anatembea katika ulimwengu, akijua kwamba, amefanya nini, amevuvi...amevuviwa! Nimepokea Roho Mtakatifu! Kristo amesambaa ulimwenguni kote, hayuko Israeli pekee yake tena. Kristo ameenda mahali popote kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ambaye ameingia katika wafuasi wote wa Yesu Kristo, hivi kwamba kila mfuasi wa Kristo ni kweli anaitwa mkristo, kwa sababu anaendeleza ujumbe wa Kristo mahali anapoenda.

Tumepokea Roho Mtakatifu. Katika kupokea Roho Mtakatifu, unapokea uzima wa milele, na tunaendelea namna gani kupokea uzima wa milele? Katika maisha ya sakramenti. Katika sakramenti ya ubatizo, tunaanza maisha mapya. Maisha ya Roho Mtakatifu, maisha ya uzima wa milele, maisha ya kuondolewa dhambi ya asili, na dhambi ya kale, na kuingizwa katika uhai mpya, kwa wale ambao uhai wao unadumu milele. Katika ubatizo, ni dhahirisho kwamba hatuwezi kufa tena. Ndiposa kitabu cha Matendo ya Mitume, ambacho tumesoma somo la kwanza leo, huitwa wakati mwingine injili ya Roho Mtakatifu. Matendo ya Mitume ni injili ya Roho Mtakatifu ambayo ni injili ya kanisa, kwa sababu matendo ya mitume, kwa sababu ni injili ya Roho Mtakatifu, basi ni matendo ya Roho Mtakatifu, lakini matendo ya Roho Mtakatifu, kwa sababu Roho ni wa Kristo, ni matendo ya Kristo.

Kwa hivyo Matendo ya Mitume, ni matendo ya Roho Mtakatifu, ni matendo ya Yesu Kristo, kwa sababu ni matendo ya wafuasi wa Kristo. Matendo yako, na matendo yangu, yanafaa yawe matendo ya Roho Mtakatifu, kwa sababu tumevuviwa, ili tuweze kutenda jinsi Kristo mwenyewe angetenda kama angekuwepo leo. Hii ndio changamoto tulionayo wakristo wapendwa.

Wakristo wenzangu, tumepokea Roho Mtakatifu, tunaishi maisha mapya, tumefanywa viumbe vya Roho Mtakatifu, katika Roho Mtakatifu, siku ya leo jinsi wana wa Israeli waliundwa taifa mpya, '*one nation*', taifa la Roho Mtakatifu, taifa la uzima wa milele, hivi kwamba yeyote anayeingia humo ameambiwa na Kristo, nimewatengenezea mahali, na katika nyumba ya baba yangu, kuna makao mengi. Jinsi tumeketi hapa leo.

Leo kuna baadhi ya ndugu zetu ambao watapokea sakramenti ya kipaimara. Na inafaa kupokea sakramenti ya kipaimara, sio siku yeyote, lakini kwa njia ya kipekee sana, siku ya leo, ambapo

tunasherekea Pentekoste, kushuka kwa Roho Mtakatifu. Sio kwamba Roho Mtakatifu hakuwepo. Maanake ni kwamba, kazi ya Roho Mtakatifu, na uwepo wa Roho Mtakatifu, unadhihirika zaidi, baada ya Yesu Kristo kupaa mbinguni. Unadhihirika zaidi, kwa sababu tumeanza ukurasa mpya katika uenezaji wa injili, ukurasa wa kanisa, ukurasa wetu, ukurasa wa Roho Mtakatifu.

Leo tunaposheherekea sikukuu ya parokia yenu, nyingi ambao mnaitwa wa Roho Mtakatifu, wakristo wa Gilgil, nawatakia kila la heri, kwa sababu mmepewa jina la Mungu mwenyewe nyinyi na *'Cathedral'* ni karibu sawa. Kwa sababu *'Cathedral'* wanaitwa, kanisa la Kristo Mfalme. Na ninyi mnaitwa kanisa la Roho Mtakatifu. Nani ana nguvu kuliko mwingine? Kristo au Roho Mtakatifu? Sawa! Kwa sababu wote ni Mungu. Mungu mmoja, Baba, Mwana na Roho Mtakati...Mtakatifu! Kwa hivyo ninyi, kila mmoja wenu anaitwa 'mroho', *'spiritan'*, si ndio? *'You are all spiritans because you belong to the parish of the Holy...Holy Spirit'*. Na mtu ambaye ni *'spiritan'*, tunamwita 'mro...mroho', lakini sio mkono biri.... sio mkono birika! (KICHEKO) Watu wa roho, watu ambao wameingiwa na Roho Mtakatifu, lakini ionekane katika vitendo. Ili matendo yenu, na vitendo vyenu, viweze kufananishwa na vitendo vya mitume katika kitabu cha Matendo ya Mitume. Ili tuweze kuzungumzia, matendo ya *'Wagilgil'*. Na matendo ya *'Wagilgil'*, ni matendo ambayo yanafanana na matendo gani? Ambayo yanafanana na matendo ya Roho Mtakatifu, yale ya mitume.

Tuombe katika misa hii, tuombe amani ya kweli. Kwa sababu amani ya kweli ndio Roho Mtakatifu aliwaletea mitume, Yesu Kristo aliwaambia, anawavuvia Roho Mtakatifu, amani kwenu. Yeyote tutakayekutana naye, tumpelekee amani ya Yesu Kristo. Sisi wakristo wakatoliki,

tueneze amani, katika nchi yetu, katika familia zetu, katika mahali petu pa kazi, kuwepo na umoja, kuwepo na ushirikiano, tusiwe na kisasi, hata ukitendewa mabaya, usiwe na kisasi, tuendeleze amani, kama watu wa Roho Mtakatifu, kanisa takatifu, watu ambao wamepokea, wamevuviwa na Yesu Kristo, ili waendeleo kueneza injili yake. Kila mmoja wetu, kila mmoja wenu, wewe na mimi, anastahili kuitwa Kristo mwingine! Kristo mwingine! Kristo mwingine! kwa sababu tunatembea katika ubatizo, na kipaimara, na Roho wa Kristo. Na Kristo hayupo katika mwili wake, lakini Kristo yupo katika miili yetu. Lazima kila mmoja wetu afahamu, na kukumbuka, kile ambacho Kristo angetenda katika mwili wake, hayupo sasa, Kristo anaweza kukitenda katika mwili wangu, kwa sababu yumo ndani yangu.

Tumsifu Yesu Kristo.(Daima na milele)

**MAHUBIRI YA 2 -KANISA LA HOLY SPIRIT– GILGIL (NA KASISI)
SIKUKUU YA ‘CORPUS CHRISTI’**

Padri: Hamjambo nyote,

Waumini: Hatujambo.

Padri: Natumsifu Yesu Kristo

Waumini: Daima na milele

Mwanzo wa ibada hii ya misa takatifu, nimewambia ya kwamba, leo tunasherehekea sikukuu ya **Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo**, kwa Kilatini tunasema ‘*Corpus Christi*’ na tena kwa lugha ya Kiingereza ni ‘*The Body and the Blood of our Lord Jesus Christ*’ na kwa Kiitaliano ni ‘*il Santissimo Corpo e Sangue di Cristo.*’ Hivi majuzi tumekuwa tukisherehekea sikukuu tofauti tofauti. Kwa mfano: sikukuu ya Pasaka ambayo ni kuhusu ufufuko wake Bwana wetu Yesu Kristo; sikukuu ya kupaa kwake Bwana wetu Yesu Kristo kwenda mbinguni; na Jumapili ya tarehe 8-6-2014 tulisheherekea sikukuu ya Pentekoste, yaani ujio wa Roho Mtakatifu, ambayo pia ni sikukuu ya parokia yetu ambapo Roho Mtakatifu ndiye somo wetu. Kwa kweli Pentekoste ni siku kubwa sana kwetu kwa sababu, tukisheherekea ujio wa Roho Mtakatifu, huwa pia tunakumbuka kuzaliwa kwa kanisa. Na kwetu katika parokia yetu, tukisherehekea Pentekoste ya mwaka huu, tuliona rehema za Mwenyezi Mungu zikitushukia kupitia kwa watu mia tatu arubaini na sita, waliopewa sakramenti ya kipaimara. ‘*This is a sign of a growing church*’. Ni ishara na matunda ya kanisa ambalo linaendelea kukua. Tena tukawaona wanafamilia ambao wameitika wito wa kuendeleza mafundisho kuhusu maisha ya familia. Wanafamilia hawa walifanya ahadi zao mbele yake baba askofu. Tena tukawa na mchango wa pili, ishara ya kujitoa pamoja na mali na vitu vingine vyote tulivyo navyo.

Tulivyo navyo tunavileta kwenye *‘altar’* ya Mungu ili kusaidia kanisa katika kueneza injili, *‘that is evangelization through social action’* ili tuendeleza mjengo wa shule yetu, kusaidia askofu katika mradi wa *‘Catholic Diocese of Nakuru Family Plaza’*; ili tuweze kujenga *‘maternity’* katika zahanati yetu; na kununua gari la kazi ya kichungaji katika parokia yetu. *‘Pursuing all those activities is what is called social development or evangelization through social action’*. Nayo Jumapili iliyopita, tukasherehekea sikukuu ya Utatu Mtakatifu. Hapa tunaongea kuhusu nafsi tatu katika Mungu mmoja. Nafsi hizo ni zipi? Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Umoja ulioko katika hizo nafsi tatu, ndio umoja kila mmoja wetu ama sisi kama kanisa, sisi kama familia, sisi kama taifa na ulimwengu mzima tunahitaji kuwa nao. Ukiingia katika mlango ule wetu wa kanisa, tena ukitazama pale kwenye maandishi ya jina la shule yetu, utaona *‘logo’* ya jimbo Katoliki la Nakuru iliyo na maandishi ya Kilatini, *‘ut unum sint’*, meaning, *‘that all may be one, the prayer that our Lord Jesus Christ prayed before getting into passion or before leaving this world that his desire and command to us is that we maybe one (John 17:21)’*.

Siku ya leo tunasherehekea sikukuu ya **Mwili na Damu Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo** ambako ninataka kuongea kuhusu vitu vitatu. Vitu hivi ni vipi?

- Kwanza nataka kuongea kuhusu miili yetu ama mwili wa mwanadamu, *‘our bodies’*.
- Pili nataka kuongea kuhusu *‘The Mystical body of Christ’*.
- *‘Finally I will speak about’*, nitaongea kuhusu Ekaristia Takatifu, yaani Mwili na Damu

Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambayo ni sikukuu tunayoadhimisha siku ya leo.

Nikiongea kuhusu miili yetu, katika kitabu cha Mwanzo, tunasikia ya kwamba ni Mungu aliyetuumba. Katika sura ya kwanza mstari wa ishirini na sita, tumesikia ya kwamba, Mungu

alisema na sasa tumbe binadamu kwa sura na upendo wetu. *‘We are created in the image and likeness of God. You are supposed to see the image of God in that person’*. Unapomwona mtu, unatakiwa kumwona Mungu ndani ya mtu huyo. Baada ya Mungu kutuumba kutoka kwa ardhi, alimvuvia roho wake ndani yetu, ili tukapate uhai. Miili yetu ni mfano, ama ni kielelezo, ama ni picha ya kuona vile Mungu alivyo.

Kwa hivyo kuzaliwa kwa Bwana krisimasi huwa tunasherehekea *‘the incarnation of the word of God’* ambapo katika sikukuu ile neno la Mungu alichukua mwili na akakaa kwetu. *‘The word of God took the human flesh so that human beings can understand God better. Incarnation is the mystery of the word of God taking human flesh’*. Kwa hivyo, ukiongea kuhusu mwili wa Yesu, lazima pia utaongea kuhusu mwili wa mwanadamu. Kwa sababu tumeumbwa na upendo na sura yake Mungu. Sisi sote ni kitu kimoja, *‘but we are unique’*. Tuko sawa lakini hakuna vile unaweza kumkosanisha mtu mwingine na mwingine. Ndio sababu tunatofautisha tunasema huyu Gladys huyu ni Evaline, huyu ni Maryanne, huyu ni Mrs Kariuki, na huyu ni Jacinta. Lakini kuna kile kinakufanya uweze kuwatofautisha *‘that is the uniqueness of human beings’*. Kufikia sasa natumaini mnaelewa ni kwa nini ninasema hauwezi ukaongea kuhusu mwili wa Yesu Kristo, au vile Mungu alivyoumba, na ukose kuongea kuhusu maumbile yetu kama wanadamu.

Baba Mtakatifu, Yohane Paulo II ameandika kitabu: *‘Theology of the body’* na katika *‘The Theology of the body’*, anaeleza maana ya mwili wa mwanadamu, *‘the beauty of the human person, the beauty of human person in glorifying God, thus not indulging ourselves in immoralities’*. Leo katika misa ya kwanza, nilikuwa nikiwauliza, mmeshawaona watu warembo? *Have you ever seen a beautiful person? ‘Nyinyi’ Are you beautiful person yourself? Why do*

you say that? And have you ever seen an ugly person? Mama anasema (kabisa) Nakumbuka siku moja kuna mwalimu Padre Serge Propst aliyetufunza huko ‘*seminary*’. Alitufunza somo la ‘*Justice and Allied Virtues*’. Alikuwa anatuambia ya kwamba hajaona ‘*anything beautiful like the human body. There is nothing beautiful like the human body*’. Hata mimi sijaona kitu kingine kizuri na kirembo kama wanadamu. Wafikiri nini kuhusu urembo huo? Ngozi nzuri, kucha nzuri, mikono mizuri, nywele maridadi, na kama umenyolewa kipara bado ni maridadi, meno ya kupendeza, miguu, mapua, na masikio! Yote yanarembesha kwa sababu mtu ameumbwa hivyo na Mungu. Na hakuna kiumbe kingine kinachomkaribia Mungu ulimwenguni isipokuwa mwanadamu ambaye amepewa kipaji cha akili. ‘*That is the gift of intellect*’.

Mwili wa binadamu una viungo vingi. Kila kiungo kina umuhimu wake katika kuendeleza kazi ambayo Mungu ametupa. Kwa hivyo, tukielewa tumeumbwa na sura na upendo wa Mungu, hakuna haja ya kuharibu mwili wako. ‘*It is an imperative to ensure that you retain the dignity of your body, retain the beauty of your body, you ensure that your body is healthy*’. Jambo la kusikitisha ni kuwa, wengine wenu mnajiwachilia vumbi, uchafu mwingi kupindukia. Unakuta mtu amechakaa ajabu! Hata kama uko mrembo, unakuta urembo huo hauonekani. Hebu niulize: nani katika kanisa hili haogi, tumsafishe? ‘**And you know**’ hata wale watoto wanaoitwa ‘*street children*’ ukijiachilia wakati mwingine wanakushika, wanakusafisha kwa nguvu. ‘*Simply because they want cleanliness*’. Kuna msemo wa kiingereza unaosema, ‘*cleanliness is next to Godliness so they don’t want you to be dirty. It is good to take care of our physical bodies; it is good to take care of your physical bodies. You are all aware of the programme regarding Female Genital Mutilation (FGM) campaigning against women’s cutting. Genital mutilation*

is against human dignity and respect for women. As such it is evil! So it is so important to underscore the dignity of the human body'.

Tena kuna wengine wetu tunatumia miili yetu vibaya sana. Ukitembea katika miji, unakutana na wasichana na wanaume mitaani wakiuza miili yao. Na sisi wapumbavu tunaenda kununua. *'So, who keeps those person's there, who keeps those person's there, do they keep themselves or it is those who go to buy sex from them. Let us take an example of buying and selling of items in a shop. Even if you open the shop, and you have commodities, yet there are no customers, that business will not be viable. It is only yesterday that I saw on the TV that unfortunately, now the increase of homosexuality in this country is high. It is very sad to see that people are getting out of their proper way of life, getting into deviations such as homosexuality, yet you all know such are ways which are spreading HIV/AIDS seriously. To make the matter worse, a man could be married, leaves the wife at home and goes to have sex with a fellow man! What a hell is that?'* Simseme hiyo pepo mbaya ishindwe (ishindwe)! Tumsifu Yesu Kristo.

Tunahitaji kuheshimu miili yetu. Mtakatifu Paulo anasema miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anafaa akae ndani ya mwili wako, ili umtukuze Mungu. Miili yetu sio ya kutumika kufanya mambo machafu, inahitaji itumike kumtukuza Mungu. Inafaa ule chakula cha kujenga mwili sio kudhoofisha mwili. Kinywaji unachokunywa kisiwe cha kudhoofisha afya yako. Lakini jambo la sikitisha ni kuwa, wengine wetu tukienda huko mitaani tunakunywa pombe ile iitwayo 'kalikali', tukisema: *'we are taking one for the road. Which later turns to be one for the ditch'*. Haina haja kula vitu vya kuharibu miili yetu. Injili ya Mtakatifu Yohane inatwambia, anayekula mwili wangu, na kuinywa damu yangu, anao uzima wa milele (Yohane

6:54). Kwa hivyo tule chakula ambacho kinafanya tuwe na uzima wa milele. Tunapoomba, sala ya Baba yetu tunasema utupe mkate wetu wa kila siku (Mathayo 6:11).

Basi tunahitaji kula chakula ambacho tumewekewa na Mungu. Tusile chakula ambacho tumewekewa na ibilisi. Hiyo pombe tunaenda kunywa huko, nyama ya ng'ombe aliyekufa kwa sababu ya ugonjwa, hicho sio chakula kutoka kwa Mungu. Hoja ninayo jaribu kuelezea hapa ni vile vyakula ambavyo tunahitaji kutumia ili kuhifadhi miili yetu kwa sababu ni mitakatifu. Tumsifu Yesu Kristo. *'That is point number one'. 'Now I want to elaborate point number two which I have said is the Mystical Body of Christ. In other words, the mystical body of Christ is the church. This congregation gathered here. And why is it that we are called the mystical body of Christ? It is because we believe in the presence of Jesus Christ in the Eucharist. Therefore in the Eucharist, Jesus Christ comes to us and we go to him'.*

Kama vile ngano inasiagwa halafu inaunda mkate mmoja, mkate ambao unatuimarisha, basi na sisi katika imani tunakuwa mwili wa Kristo, ambao ni kanisa. Cha maana kuelewa hapa ni kuwa watu wote ni wa Mungu. Kadinari Henry de Lubach ameandika kitabu ambacho kichwa chake ni *'Catholicism.'* Katika kitabu hicho de Lubach anaelezea vile tangu kuumbwa, watu wote ni wakatoliki. Neno katoliki linamaanisha ulimwengu wote, *'that is universal.'* Ninyi mwasema mtu huwa mkatoliki lini? **'When did you become a catholic?'** Wakati ulibatizwa? Na wewe je? Ulikuwa mkatoliki lini, wakati ulibatizwa, unasema hivyo kwa sababu ni hivyo ama mwenzako amesema hivyo? Cecilia ulikuwa mkatoliki lini? Margaret umekuwa mkatoliki lini, *'or when does one become a catholic?'* (wakati mtu anapokea mwili wa Yesu Kristo). *'Are you a catholic?'* (Baada ya kubatizwa na kupokea mwili wa Yesu Kristo) nyinyi mmesema wakati wa

ubatizo. ‘Ulikuwa kwa **‘ministry?’** Kadinari de Lubach anasema tunakuwa wakatoliki tangu kuumbwa na kuzaliwa kwetu, tulipoingia katika ulimwengu huu. *‘His argument is based in the meaning of the word Catholic. What is the meaning of the word Catholic? It means universal. So we became Catholics after God endorsed his breath in us. That is from the beginning of life’.*

Tulikuwa wakatoliki wakati Mungu alivuvia uhai ndani yetu. Kwa hivyo hatukuwa wakatoliki wakati tulibatizwa, kupokea ekaristia au kipaimara. Hapana, kwa kupokea sakramenti hizo, tukawa tunapiga hatua mbele, kuthibitisha ukatoliki wetu. Kwa hivyo unapopokea ekaristia, unakubali kuwa unasadiki vile Mungu anasema ya kwamba, anayekula mwili wangu na kuinywa damu yangu, huyo yuko ndani yangu, nami ndani yake. Nasisitiza tena ya kwamba tunakuwa wakatoliki tangu kuzaliwa, na ndio unakuta kwa mfano tukitoa huduma zetu kama kanisa, hatubagui huyu ni Mkatoliki ama huyu ni Muislamu. Ama huyu ni Muibrania, ama huyu ni wa dini nyingine.

Kwa mfano, ukija kwa hospitali yetu hapa, hautaulizwa dini yako ni ipi. Unatibiwa mara moja kwa sababu *‘our objective is to serve the whole human race, to serve the whole human race, to serve all people of God, who are all the same as is underscored in the meaning of the etymology of the word catholic or universal. The fact that somebody has gone to another denomination, the fact that somebody is in another religion, is an indication that we need to proclaim the gospel to the end of the world. We need to tell and demonstrate in actions, because we say that actions speaks louder than words, that we need to bear in mind that we are all brothers and sisters’.* Kwa sababu hii tunawahudumia watu wote bila ubaguzi. Ndani ya

kila mtu kuna roho wa Mungu. Na Mungu alituumba na kutuita ili tuweze kumtukua kwa kuwahudumia watu wote. Kwa mfano, hata ukiwasikiliza watu wote hata waislamu, wananiita *‘father’*, *‘Thus as the mystical body of Christ, that is the church, we need to be good to each other. I have now finished elaborating point number two and go to point number three as underscored in today’s readings’*.

Masomo ya leo yanaongea juu ya nini? Katika somo la kwanza tumesikia vile Mungu aliwapa wana wa Israeli mana kama chakula baada ya kutaabika kule jangwani kwa njaa. Mungu aliwapa mana kutoka mbinguni. Hayo mana sio tu chakula cha kulisha miili tu, mbalii ni ishara ya Mungu akiandamana na taifa teule katika shida zao na ugumu wa maisha ya hapa ulimwenguni. Ni ishara ya chakula kinachotoka juu mbinguni, kinapewa mwanadamu na Mwenyezi Mungu. Katika sala ya Baba yetu, tunamwomba Mungu atupe leo mkate wetu wa kila siku, ambacho ni chakula kutoka mbinguni. Basi ukila chakula kutoka mbinguni, usile kama mnyama asiyekuwa na ufahamu, kula kama mwandamu ambaye amepewa ufahamu au akili ni Mungu. *‘We have just spoken about the human dignity’*.

Kwa hivyo kabla hujala, sema sala kabla ya chakula. Sisi wote natusemeni sala kabla ya chakula (Utubariki Mungu wetu, sisi na chakula chetu, ili tukila tupate nguvu za kukutumikia vyema, kwa njia ya Kristo Bwana wetu, amina). Na baada ya kumaliza kula, tunahitaji tena kusali sala baada ya chakula. Na tuiseme hiyo sala sasa (Tunakushukuru ee Mungu wetu, kwa sababu ya chakula tulichokula, ili tupate nguvu za kukutumikia vyema, kwa njia ya Kristo Bwana wetu, amina). Kwa hivyo, tukila chakula chetu kila siku, tukumbuke mana kutoka mbinguni, ambako vyote vinahitaji kutuelekeza kwenye chakula cha uzima wa milele, Ekaristi takatifu. Katika somo

la pili la leo, mtakatifu Paulo anauliza: Je mkate ule tuubarikio, na kikombe kile tukibarikio, sio ushirika wa mwili na damu ya Kristo?’ *‘What do we now need to do? We need to answer those questions saying’*, kweli ni mwili na damu ya Yesu Kristo.

Na hata leo utakapokuja hapa mbele kupokea Ekaristia, padre akikwambia, mwili wa Kristo, jibu kwa sauti kubwa, amina. Unajua kuna wengine ukiwaambia, mwili wa Kristo, ee? Unarudia tena, mwili wa Kristo, nao wanakuuliza, umesema nini? *‘Then there are those you will say to them, the body of Christ, instead of them responding, ‘amen’, they say, ‘thank you.’ As a matter of faith and doctrines of the Church you need not to say ‘thank you’ but ‘amen’ affirming truly that as the priest has said, you are receiving the body and blood of Christ’*. Tatizo linguine nikuwa, ukiwapa wengine wetu Ekaristia, badala ya kufumbua mikono vizuri, na kwa unyenyekevu, wapokea mikono ikiwa imefumbwa. Wengine wanapokea Ekaristia kutoka mikononi mwa padre badala ya kumwacha padre ailaze viganjani mwao.

Siku ya krisimasi niliwaambia ya kwamba, tunaponyosha mikono yetu kupokea Ekaristia takatifu, viganja vyetu vinakua kama hori alimolazwa mtoto Yesu alipozaliwa. Kwa hivyo, tunapofumbua mikono yetu kumpokea Yesu Kristo, viganja vyetu vinahitaji kufumbuliwa vizuri kwa njia inayoonyesha unyenyekevu na heshima. Pia tukisema tuweka bahasha za zaka mikononi mwetu, tunahitaji kuzishika vizuri kama tumenyosha na kuinua mikono yetu juu vizuri, tayari kupoea baraka. *‘It is important to sanctify ourselves, and present our offertory to God in faith and dignity. Inspired by the words of our Lord Jesus Christ during the institution of the Holy Eucharist when he said:’* “Twaeni mle wote, huu ndio mwili wangu utakaotolewa kwa ajili yenu”. Tena akachukua kikombe cha divai, akakibariki akisema, “twaeni mnywe wote,

hiki ni kikombe cha damu yangu, damu ya agano jipya la milele, itayomwagika kwa ajili yenu na kwa ajili ya wengi, kwa maondoleo ya dhambi, fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi” (Mathayo 26: 26-29).

‘Now here comes the conclusion of which is a warning to those who don’t receive the Eucharist.’ Ndugu na dada zangu, kama hupokei Ekaristia, unahitaji kujiuliza maswali mengi, kwa sababu kuna kitu kisicho sambamba maishani mwako. *‘There is something wrong in your life. It is not enough to say you receive in desire. To be in true communion with the church, Catholics are required to receive the Eucharist in the real presence not in desire. Catholics who are absent at mass, and non-catholics who attend our service, it is acceptable that those can receive in desire. Otherwise for Catholics who are present at mass yet they don’t come forward to receive the Eucharist, I repeat to tell you that there is something seriously wrong. To remain seated singing and dancing, “twendeni kwa karamu ya Bwana tumeitwa”, yet you are not waking up, you are there warming your seat, that is a very clear indication that there is something wrong’.*

Mwisho kabisa, leo tukimega mkate na kugawana kikombe cha damu ya wokovu, na tukileta sadaka zetu kwenye madhebahu ya Bwana, tulilete kanisa letu, na pia miili yetu, ili vyote viimarishwe na mwili na damu takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo, na kutuwezesha kupata uzima wa milele. *Na tumsifu Yesu Kristo (Daima na milele).*

MAHUBIRI YA 3- CONSOLATA WESTLANDS
SIKUKUU YA PENTEKOSTE

Ndugu wapenzi hamjamboni tena? *'God is good?'* (Kasisi) *'All the time'*. (Waumini)

Ninakaribisha kila mmoja wetu kanisani kwa hii sherehe muhimu katika kanisa letu. Leo ni siku hamsini tangu tusherekee sherehe ya ufufuko wa Bwana Yesu Kristo. Na kwa siku tisa zilizopita sisi tumekuwa tukijiandaa kwa hii sherehe. Ili Mwenyezi Mungu aweze kutujalia Roho Mtakatifu na kwa njia ya pekee kwa neema zake atuwezeshe kufanya utafiti na makadirio ya jinsi tunavyoishi maisha yetu ya kikristo, *'self-evaluation'*. Kwa sababu yeye ndiye tegemeo letu na hakuna chochote kile tunaweza kufanya duniani bila msaada wake. Na kwa sababu hiyo wewe na mimi kama wakristo wakatoliki, tunaamini Mungu mmoja katika utatu mtakatifu. *'Holy Trinity'*.

Hiyo ni kumaanisha kanisa inatupatia kutafakari juu ya kazi ile ya utatu Mtakatifu kwa njia ya kipekee Mungu Baba ni muumba *'creator'* na sisi wote tunaamini ya kwamba hakuna kitu ambacho kinaishi duniani ambaye haikuumbwa. Na ndio tunamtukuza Mungu kwa njia zote sisi kama binadamu. Na ndio sisi tunamtegemea yeye kwa sababu ametupatia akili kuliko viumbe vingine *'intellect'*.

Hapo basi ndio tunamtukuza Mungu Mwana siku ya pasaka kwa njia ya kipekee. Ati ndiye yule Mungu alituma kati ya binadamu baada ya kumuasi yeye ili aweze kuleta upatanisho kati ya Mungu na wana wake wapenzi. Na siku ya leo, ya *'Pentecost'*, tunazingatia zaidi kuona kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu ni muhimu, sisi tumeandaa kwa siku tisa ili tuone ya kwamba Mungu Baba, Mungu Mwana wanahitaji ushirikiano wa Roho Mtakatifu ili waendeleze

kutujalia njia ya kutafuta wokovu kwa msaada wa huyu Roho Mtakatifu. Katika Jumapili iliyopita wewe na mimi tulisherehekea sherehe ya kupaa Bwana wetu Kristo, *'Ascension day'*. Alipopaa, alituhakikishia kwamba hatatuacha yatima. Hiyo ni kumaanisha katika hii sherehe, anatamatisha yale yote aliyotuahidia ya kwamba tunahitaji msaidizi na huyu msaidizi si mwingine bali ni Mungu Roho Mtakatifu.

Leo basi tumesikia kutoka somo la kwanza iliyotoka katika kitabu cha matendo ya mitume ati kuna ishara ya Roho Mtakatifu. Na hata mababu zetu na sisi wote ambao sasa tunakili Mungu mmoja kama wakatoliki wema tunamtambua Roho wa Mungu Roho Mtakatifu katika ishara mbalimbali. Ya kwanza ni nguvu ya upepo, *'wind'*, na ya pili ni ndimi za moto, *'tongues of fire'*, na ya tatu ni njiwa, *'dove'* na ya nne ni maji, *'water'*. Hizo ndizo ishara ambayo binadamu wote katika makabila mbalimbali katika makanisa yao wametambua ya kwamba hizo ndizo ishara za Mungu Roho Mtakatifu.

Na mimi basi, leo nina furaha siku ya leo kwa sababu mlifika kanisani ambapo kunanyesha lakini kwa sababu wewe na mimi tunaamini ya kwamba Mungu ana ishara zake za baraka kati yetu ndiposa haukuona sababu ya kubaki nyumbani mbali tulijitolea kwa imani ya kwamba mvua sio kizuio cha sisi kuja ushirikiano na Mungu wetu mbali ni baraka kwetu. Sasa basi tuko leo hapa tuone ya kwamba Mungu yuko pamoja nasi katika ishara mbalimbali. Na katika somo la pili ambayo imetolewa waraka wa mitume Paulo kwa Wakorintho Paulo anasisitiza kwa jamii ya wana wa Mungu ya kwamba Roho Mtakatifu ndiwe msingi wa karama na huduma na kazi zote ambazo sisi tunafanya. *What does that mean?* Ya kwamba Mungu aliyetuumba kila mmoja wetu ametujalia karama ya kipekee ambaye ni tofauti na wenzake. Na pia katika maisha yetu ya kila

siku tunatoa huduma mbalimbali hatuwezi kukamilisha huduma hizi bila msaada wa Roho Mtakatifu. Na katika kazi zetu ambazo tunajishughulisha kila siku hio kazi tunafanya kwa msaada wa Roho Mtakatifu ambaye ni vipaji vya Roho Mtakatifu. Ili tufanye kazi zetu kwa njia ya kipekee kwa ajili ya kutoa huduma kwa ndugu zetu na kujijenga sisi wenyewe ili ufalme wa Mungu iendelee katika dunia tukijiandaa kupokea ufalme wa Mungu pamoja naye katika siku za usoni.

Na katika injili tumesikia jinsi tumeelezewa ya kwamba Kristo mwenyewe aliwawuvia mitume wake Roho Mtakatifu. Ati mpokee Roho Mtakatifu ili iwapatie ujasiri ya kuendeleza kazi. Yale mazuri nimeyafanya hapa duniani ya kuleta amani kati yenu na pia matumaini ya kwamba nyinyi mko na Mungu kila wakati. Akawapatia hakikisho lingine ati wale wote mtaamini yale nitakayohubiri wakiwa wameanguka katika dhambi mwatolee dhambi zao kwa nguvu ambaye mimi ninawapatia nguvu ya Roho Mtakatifu. Wale ambao wanakuwa na ugumu kati yao, msiwalazimishe kwa sababu wokovu ni kitu cha hiari mmoja kupokea mwaruhusu wabaki katika hali yao. Hapo nikumaanisha ya kwamba pengine wakati huo watu au yule ambaye amelikwa kukiri Kristo kama Mwokozi hajapata kuguswa na Roho Mtakatifu ili aweze kuokoka.

Ndugu wakristo tusherehekee siku ya leo tukiamini ya kuwa Roho Mtakatifu anafanya kazi katika maishani yetu na hakuna kile tutaweza kukamilisha duniani hii bila msaada ya Roho Mtakatifu ndiye yule atawezesha kupendana kati yetu na kuamini ya kwamba kuna kujaliwa kulingana na vipaji vya Mwenyezi Mungu na kuvitumia kwa ajili ya kuwatumikia ndugu zetu. Ndiye yule Roho Mtakatifu atakayetuzalia matunda ya Roho Mtakatifu *'fruits of the Holy Spirit'* ili tuishi kama wana wa Mungu.

Tusali basi siku ya leo tukiombeana na kuamini ya kwamba Mungu ametuonyesha ishara zake kila siku ambaye zinatufanya sisi kumfahamu na kumkubali na kumkiri kwa imani anatumjalia karama katika maisha yetu anatusaidia kutoa huduma kwa wenzetu anatumpatia njia ya kuishi maisha kulingana na mapenzi yake. Tumsifu Yesu Kristu. *'God is good?' 'All the time'*.

MAHUBIRI YA 4 - HOLY FAMILY BASILICA

SIKUKUU YA PENTEKOSTE

Basi wakristo karibuni katika tafakari ya leo tukisherekea sikukuu ya muhimu sana ya *'Pentecost'* maanake ni siku hamsini baada ya ufufuko wa Bwana Yesu Kristo, leo ni siku ya hamsini tangu tulisherekea ujio wa Roho Mtakatifu kwa hivyo tuliwakisha huo mshumaa wa Roho Mtakatifu. Katika masomo yetu tumesikia na tumeelewa kazi ya Roho Mtakatifu na vile inatakiwa kazi ya Roho Mtakatifu kufanyika katika maisha ya kila mmoja wetu kama wafuasi wakristo ambaye alituahidia yeye mwenyewe kwamba atatuletea Roho Mtakatifu yeye mwenyewe.

Wayahudi, historia ya siku ya leo yatokana na Wayahudi wenyewe, ya kwamba Wayahudi walikuwa wanasherehekea siku hamsini baada ya kukombolewa kutoka huko Misri. Basi wao ilikuwa desturi yao kusherehekea uhuru wao, kusherehekea siku hiyo baada ya siku hamsini. Basi hiyo ndio historia ya Pentekoste na sisi kama wakristo tunasherehekea siku hamsini baada ya kukombolewa kutoka dhambi kwa sababu Yesu alikufa juu ya dhambi zetu na akafufuka, akashinda dhambi ili tuondolewe katika utumwa wa dhambi kwa hivyo unaona hayo mambo mawili yanafanana ya kwamba ni utumwa.

Wayahudi walisherehekea siku hamsini baada ya kutolewa huko Misri utumwani na basi sisi tunasherehekea siku hamsini baada ya kuondolewa katika dhambi. Kuna sherehe tatu za umuhimu sana katika maisha ya kanisa letu. Kwanza kuzaliwa kwake Kristo *'incarnation'* pili kufufuka *'resurrection'* na tatu *'Pentecost'*, wakati tunasema ya kwamba ni siku ya kuzaliwa kwa kanisa, kanisa linazaliwa siku ya leo ndio unaona inawekwa nguvu mpya kabisa.

Tunafunuliwa, tunaletewa uso mpya katika maisha ya mwanadamu na kwa hivyo sisi wote wakristo leo ni siku ya muhimu sana kwetu na tumefungua, tumekuwa tukijitayarisha kufungua roho zetu. Tumefanya hata maombi ya novena siku tisa tukijaribu kujiweka katika hiyo hali ya kupokea Roho Mtakatifu. Pia Wayahudi walikuwa na swala lilikuwa linawasumbua, walikuwa wakijiuliza kwa nini mwanadamu anafanya au anatenda vitendo ambavyo vinaleta usumbuvu katika maisha yake, yeye mwenyewe na maisha ya mwanadamu mwenzake.

Kwa nini mwanadamu anatoa matamshi ambayo yanatenganisha watu? *'Why eh why?'* Kwa nini tunatenda dhambi? Kwa nini familia zinavunjika? *'Why?'* Na sisi sote tunajua umuhimu wa familia? Unashindwa tukiwa katika Parokia kama hii hata kanisani, *'surely'* kwa nini? Tutengane? *'Why?'* Tuseme maneno ambayo inafanya watu kutengana zaidi na zaidi. Tunafanya mambo ambayo inaondoa amani yetu ambayo tungetaka tukiwa pamoja tungefurahia zaidi na tungekuwa na nguvu zaidi. Kwa nini? Basi Myahudi akajua kuna kitu kinasababisha, kuna kitu kinaleta sasa mambo haya mabaya katika maisha ya mwanadamu. Myahudi akajua kuna roho mbaya na kwa hivyo akaona kuwa wakati wowote mtu fulani ama watu fulani wanaelekezwa na huyu roho mbaya *'bad spirit'*.

Basi ndiyo unaona ya kwamba shida zote zinatokea kwa sababu roho mbaya wa shetani kazi yake ni kutenganisha watu, kazi ya huyu pepo mbaya hata mnasema ashindwe, watu wanasema ati ishindwe tunaseme ashindwe na tunaendelea kufanya kazi zake na kwa hivyo Myahudi akajua ya kwamba *'there is a bad spirit in each one of us'* kuna roho mbaya katika *'minds'* zetu. Kuna roho mbaya na kwa hivyo Myahudi kulingana na vile alivyolelewa *'imagine'* alikuwa anatoboa kichwa. *'Imagine'* anaweka shimo kwa kichwa anaondoa pepo hii mbaya, halafu katika hilo

shimo anaingizwa, hiyo ndio historia sasa ya siku ya leo na kwa hivyo kila mmoja wetu tunataka kutoboa katika roho zetu shimo. Tunataka kuweka shimo katika fikira zetu ili roho mbaya ituondokee ili roho wa Mungu siku ya leo aweze kuingia na ndiyo maana tumesikia katika somo la kwanza hakuna mtu ambaye atamtambua Kristo atasema ataungama Yesu Kristo kama mwokozi wa maisha yake kama hajaongozwa na Roho Mtakatifu ndiye anayetuelekeza kwa mambo yote mazuri hata vile umetoka nyumbani siku ya leo na tuko hapa kanisani.

Siku ya leo ni roho wa Mungu amekuelekeza. Ni roho wa Mungu amenielekeza na ametuelekeza sisi sote kuja kumtukua Mwenyezi Mungu kwa sababu tunatambua Mungu kwa sababu huyo roho ametuwezeshwa kumtambua Mungu kama muumba wetu, kama Mungu wetu sisi wanadamu. Kwa hivyo wakati wowote unafanya kitendo kizuri wakati unatamka matamshi mazuri ya kuleta watu pamoja mpaka watu wanaishi kwa amani basi huyu ni Roho Mtakatifu. Ndio maana katika injili Yesu Kristo, anasema ya kwamba jambo la kwanza amani iwe nanyi, itakuwaje, litakuwaje, itakuwaje, *'how?'*. Kutakuwaje na amani katika hiyo familia kama Roho Mtakatifu hatakuwa akiliongoza.

Tuangalie sana tujiulize kwa nini hata wanakenya hata siku ya leo tunatengana. Tumesikia katika somo la pili, Paulo akisema, akituambia ya kwamba karama ni nyingi *'but we are different'* lakini tukiunganishwa na roho mmoja, kwa sababu roho wa Mungu anatuunganisha pamoja ili karama hizi zote, tofauti hizi zote ziwe faida kwetu sisi wote. Na ndio maana unaona katika somo la pili na la kwanza hao watu walikuwa makabila wengi sana lakini wakati roho wa Mungu aliwaelekeza wote wakasikizana, wakaelewana, wote wakapatana na wakawa na nguvu zaidi kwa sababu roho wa Mungu aliwaelekeza na kwa hivyo hata sisi wakenya tutaweza tu

kupatana, kuelewana, kupendana wakati Roho Mtakatifu atatuelekeza, wakati Roho Mtakatifu atatuelekeza ndio tutapatana, bila kuwa na Roho Mtakatifu hakuna vita, hatutaelewana hata kidogo, karama ni nyingi. Paulo anasema kwamba sisi wote ni tofauti ukiangalia utaona ya kwamba makabila yetu arubaini, sisi wanakenya, kila kabila liko na karama zake. ***‘They have their own gifts’***, kila kabila ukiangalia enda kwa Wajaluo utaona wana karama zao, enda kwa Wakikuyu wako na vipaji vyao. Enda kwa Wakamba wako na karama zao. Enda kwa Wakalenjin wako na karama zao kwa kila kabila.

Watu wote wako na karama na kuna faida katika karama zao. Lakini ni lazima tuombe Roho Mtakatifu ***‘that we are able to appreciate one another’***, kulingana na mimi wakati tutaweza wanakenya kuona hizi tofauti ***‘we don’t have to be the same’***. Si lazima tuwe watu wote tuwe wajaluo. ***‘No!’*** Haitawezekana. ***‘There is no way, it will be reasonable’***, katika hii nchi watu wote watakuwa Wakamba. Ni Roho Mtakatifu atatupatia hekima ya kuheshimu karama za watu wengine. Uwe Masaai, wamaasai wako na karama zao na zinapendeza na si tu zao binafsi lakini ni za kufaidi jamii, kufaidi wanadamu kwa hivyo ukiona wakati watu wanaringia karama zao yaani mtu anashikwa na maringo kwa sababu ana kipaji hiki au ako na karama. Basi maringo ni ya nini? Mbona mnaringa? Ni shetani anayeleta maringo, wakati unaona unaringia watu unaringa na hata hizo karama ulitoa wapi? Na kwa hivyo ukiona mtu anaringa mwombee Mungu. Hata wazungu walisema kwamba maringo ndiyo inayotangulia kabla ya kuanguka kwamba ***‘pride comes before a fall’***. Kwa sababu maringo ni ya yule mwovu na huyu mwovu atakuelekeza wapi? Anakuelekeza kudhuru maisha yako.

Ni lazima tutambue ya kwamba tunahitajiana “*we need one another*” bibi anahitaji bwana, ‘*Am I right*’. Bibi anahitaji bwana yake. Kama hajagundua hivyo bado wewe hujajua. ‘*That’s why you should pray for the gift of knowledge*’, na bwana anahitaji bibi yake. Kama bwana mmoja alikuwa anafanya nini? Kila asubuhi soksi zake alikuwa wakati mwingine anavaa moja ya “*red*” na nyingine ya “*black*” bibi yake ndiye aliyekuwa akimkumbusha kila asubuhi kwamba hizo soksi mbili hazifanani . ‘*You see*’ bila karama ya bibi yako utaaibika. Ona pengine vile umevaa kama uko na bwana na mlikuwa na yeye asubuhi vile umevaa bibi yako alikuona na akaridhika. Lakini kama hamkuwa pamoja pengine umevaa shati, umevaa vibaya lakini hakukwambia kwa sababu hamjaunganishwa na roho wa Mungu, roho wa Mungu anayeleta umoja anayeleta amani kwa hivyo tuombe sisi sote wanakenya tuwe na amani katika hii nchi yetu.

Tutaendelea kusikiza hawa viongozi wetu wote kwa jumla lazima tuwe na hekima ya kuelewa wanatupatia ukweli, ukweli ni wa Mungu na kwa hivyo kama unataka kujua ukweli basi fuata Roho Mtakatifu ndiye atakayekuelekeza katika ukweli na kwa hivyo tuombe. Tuombee hata watoto wetu, vijana wetu hawa chipukizi waweze kuwa na Roho Mtakatifu ili waweze kuelewa kwamba ni roho tu wa Mungu atakayewaelekeza kwenye maisha mema wasijifanye wajuaji. Wajua siku hizi watu wanajifanya wajuaji sana, lakini unajua ‘*that’s why*’ wanasema ‘*little knowledge is dangerous*’. Huyu kijana katika nyumba yake ya kulala ameanza, unajua vile vijana wanaweka ‘*wire*’ za stima anatoanisha hii anatoanisha hii, hii iko wazi hii ni ‘*naked*’, hii ni ‘*naked*’ anaweka kwa simu yake hivi namuuliza wewe unajua hii itakuchoma? Siku moja anasema ‘*aah father*’ hapana wacha kuogopa unajua nyinyi mnaogopa sana. Wacha nikwambie siku moja hiyo nyumba yake kitanda, yote, godoro yake ilishika moto akaniambia ‘*father*’ si ni nyinyi hamkununua ‘*socket*’. Sasa unaona ‘*little knowledge*’ si angechomeka hapo ndani kwa

sababu tunajifanya wajuaji sana katika maisha. Tujiachilie kwa Roho Mtakatifu atuelekeze. Halafu huyu kijana hata alinifanya nicheke. *'Father'* unajua hata kama ningechomoka mngnilipa. Namuuliza 'sasa ungelipwa ukiwa wapi wewe?' Ati tungemlipa na mama, ati *'insurance'* ingekuwa imefuata sana. Sasa *'imagine'* na angekuwa amekufa? *'Anyway'* tuombe sana ndugu zangu Mungu atuelekeze. Hata sikumwambia kitu na nikaenda, nikamwekea *'socket'* zote kwa sababu niliona kweli haelewi. *'Nikaconnect.'*

Kuna mambo mengi sana ambayo hatuelewi na ni lazima tuombe Mungu tukiwa wazazi tujiulize kwa nini ndoa hizi zinavunjika kila wakati. Ni kwa sababu bibi ako na roho nzuri lakini pengine bwana ako na roho mbaya, ama bwana ana Roho Mtakatifu na bibi ni sumbua, si mnajua sumbua? Nasikia siku hizi kuna mabibi sumbua, ati bibi ni sumbua hata una majina, huyu bibi ni sumbua kwa nini unaitwa sumbua? Yaani kunaweza kuwa na mtu sumbua na anaelekezwa na Roho Mtakatifu la sivyo unasikia mtoto akiitwa Sumbua. *'Father'* huyu mtoto wangu ni sumbua tumebandikiwa majina siku hizi kwa sababu tunaelekezwa na roho mbaya. Ukiwa na roho mbaya utakuwa sumbua kwa watu, ukiwa na roho mbaya utakuwa na ufisadi sana, kupokea hongo kila wakati, kwa sababu ya ubinafsi, shetani mwovu na ashindwe kabisa anafanya watu kuwa na ufisadi. Na watu wengine *'they take the advantage'* kwa sababu ya cheo chao, kwa hivyo Mwenyezi Mungu atusaidie sisi wote hata tukiwa hapa kanisani.

Kwa nini katika vikundi vyetu tunazozana, kwa nini wakati mwingine tunazozana sisi wenyewe na tuko hapa kanisani? Na utaona kila mtu akijifanya mtakatifu sana mwingine hataki kupanua mdomo sana ili apokee Yesu itabidi amuinue kwa sababu ya utakatifi wake. *'What are we doing?'* Ni nini tunafanya? *'Are we honest'* hata vikundi vya kanisa tunapigana na watu

hawataki kukaa pamoja hata katika familia tunazozan tu, tunaleta mambo yote sisi wote mpaka tunachanganyikiwa. Ni kwa sababu tuna roho mbaya na ndio maana katika injili Yesu amesema akavuvia mitume Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu akawaambia wale mtaondolea dhambi, dhambi ni upepo mbaya watakuwa safi watakuwa wameondolewa na wale mtafungia dhambi wataendelea kupelekewa na roho mbaya katika dhambi zao.

Ndio maana ya sakramenti ya kitubio sisi wote ni wadhaifu hata mimi lakini kama unaelekezwa na Roho Mtakatifu ukifanya kitendo kibaya unaelewa umefanya kitendo kibaya na ukijua umeleta hitilafu maisha yako na ya watu kwa sababu ya dhambi yako unaenda unatubu yaani unaondoa pepo mbaya katika masiha yako, katika roho yako. Lakini angalia siku hizi watu wengi mtu anakosa na anasema ya kwamba hajakosa. Watu wengine *'they know it all'*, wanajau kila kitu. Wanajua mtu anakosa lakini kwake ni sawa. Mtu anavuruga watu lakini kwake ni sawa kwa sababu *'you have been possessed by the evil spirit. Let us pray that we can be possessed by the Holyspirit'*.

Ya kwamba mara moja ukitenda kitendo kibaya *'your conscious'* mara moja *'because it is clear'* mara moja unatubu kwa sababu *'that is not your life'*, maisha yetu ni ya kiroho, ni ya Roho Mtakatifu. Mungu basi atusaidie sisi sote ili tuweze kuelekezwa ukitaka kujua ukweli, akuelekeze kwa ukweli wacha kusikiza wanadamu wenzako sikiza Roho wa Mungu ukitaka kufanya mambo mazuri fuata Roho Mtakatifu akuelekeze, akuangazie ili uweze kuwa hata na hekima. Mungu Mwenyezi atubariki wakristo wenzangu, atubariki hata sisi wote na atushushie Roho Mtakatifu ili tuweze kuheshimiana ya kwamba *'we recognize and acknowledge'* ya kwamba sisi sote ni watoto wa Mungu na kila kabila lina uzuri wake na ubaya wake lakini

wakati utanza kusikia watu wakisema ya kwamba hawa wako namna hii, hawa ni wezi, hawa ni ‘*mawatchmen*’ hawa ni nini? Huyu ni shetani anayetutawala tuombe roho wa Mungu atutawale. Tukitawaliwa na roho wa Mungu tutapendana zaidi na tukipendana sisi wakenya tutajenga nchi yetu lakini tukiendelea kutengana tunaendelea kuweka udhaifu unyonge wetu. Hata katika familia tukipendana mtajenga hiyo familia na mtakuwa na nguvu zaidi na watu wote watanawiri katika maisha yao. *Kwa jina la baba la mwana na Roho Mtakatifu. Amina.*